**7 NOVEMBA, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

### Kikao cha Nane – Tarehe 7 Novemba, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Minza Simon Mjika.

Na. 124

### Ujenzi wa Zahanati Kata ya Binza – Maswa

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga zahanati katika Kata ya Binza – Maswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Binza wameanza ujenzi wa zahanati katika Kijiji cha Matarambuli. Aidha, halmashauri inaendelea kuhamasisha wananchi wa Kata ya Binza kuendelea na ujenzi mpaka hatua ya boma na Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, kwanza ninapenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali langu la kwanza; Kata ya Binza ina vijiji saba, vile vijiji saba vina idadi ya watu 8,787 hawana kituo cha afya kabisa na wanahangaika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wale wamejitahidi wana kiwanja na wamesomba tripu 30 za mawe. Je, Serikali inawasaidiaje kuhusu kukamilisha? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninawapongeza sana wananchi wa Kata ya Binza kwa kuanza kuchangia michango yao kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imeweka vigezo vya muhimu ili eneo liwe lina sifa ya kuwa na kituo cha afya; moja ni idadi ya wananchi na mbili ni umbali kutoka kituo cha afya cha jirani zaidi. Kwa hiyo, ikiwa kata hii inakidhi hivyo vigezo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, nitafuatilia na niweze kuona namna ambayo tutaweka kwenye mpango kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninashukuru Serikali ilitoa fedha kujenga Kituo cha Afya cha Mswaki, lakini kwa bahati mbaya ni kwamba fedha zilizotolewa hazijakamilisha kituo hicho. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kutuma watu wako kwenda

kuangalia ni kiasi gani kinatakiwa ili kituo cha afya kikamilike? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa fedha kwa awamu mbili; vipo vituo vya afya ambavyo vilipewa shilingi milioni 250; lakini kuna vituo vya afya ambavyo vimepewa milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha majengo yaliyoelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kigua, kwamba ikiwa kituo hicho cha afya kimepewa milioni 500 na majengo yale yana mapungufu hayajakamilika tutakwenda kufanyia tathmini; kwanza kujiridhisha na thamani ya fedha. Pili, kuona kiasi gani cha fedha kinahitajika kwa ajili ya ukamilishaji ili tupate ndani ya mapato ya ndani ya halmashauri au tupate Serikali Kuu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kituo kinakuwa na ukamilifu unaotakiwa.

**NAIBU SPIKA:** Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, eneo la Old Moshi lina kata nne na halina kituo cha afya kabisa. Katika vile vituo vya kimkakati kila jimbo nilipendekeza kituo cha afya kijengwe katika Kata ya Old Moshi, Mashariki. Je, ni lini Serikali itatoa pesa kujenga kituo hiki cha kimkakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli eneo la Old Moshi ambalo Mheshimiwa Profesa Ndakidemi amekuwa akifuatilia mara kadhaa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata kituo cha afya na aliwasilisha katika orodha ya vituo vya afya 214, katika eneo hilo la Old Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo ili fedha ipelekwe kwenye kila jimbo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati na kwa hivyo na sisi tutahakikisha kwamba fedha zikitoka tunapeleka kwenye Kata ya Old Moshi kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaunga mkono jitihada za wananchi wa Kata ya Masqaroda, Wilaya ya Hanang kwa kuwa kwa sasa wana jengo la *OPD* pekee yake na jengo la mama na mtoto na majengo mengine hamna?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha vituo vyote vya afya vinakuwa na miundombinu toshelevu kwa ajili ya kutoa huduma za afya ngazi ya kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kata ya Masqaroda katika Halmashauri ya Hanang, lakini niwahakikishie tu kwamba ikiwa wameanza kwa ujenzi wa jengo la *OPD,* Serikali itawaunga mkono kukamilisha majengo mengine ili kile kituo cha afya kiwe na majengo yanayotosha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimerejea Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza, kwa kuwa tuna vijiji zaidi ya 6,000 hapa Tanzania havina zahanati. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka sana wa kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata huduma za matibabu kwa kujenga zahanati na

kumalizia zahanati ambazo wananchi walishajitolea kwa nguvu kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ina thamini sana huduma za afya kusogezwa karibu na wananchi na ndio maana kupitia mpango wa maendeleo ya Afya ya Msingi tuliainisha maeneo yote ya vijiji na mitaa yenye sifa ya kujenga vituo vya afya. Katika miaka hii mitatu ya fedha tangu mwaka 2021/2022 mpaka sasa Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa jumla ya maboma 1,254 ya zahanati nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunahakikisha vijiji vyote vyenye sifa ya kupata zahanati vinaendelea kujengewa zahanati, lakini mitaa yote yenye sifa ya kupata zahanati pia inaendelea kujengewa zahanati hizo kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Mpakate.

Na. 125

**Kuboresha Kituo cha Afya Mtina – Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha Kituo cha Afya Mtina ili kitoe huduma za upasuaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Mtina kilijengwa mwaka 1976 na ni moja ya vituo vya afya Kongwe 212 ambavyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI imevibainisha kwa ajili ya ukarabati

utakaoanza baada ya kukamilisha ukarabati wa hospitali kongwe za halmashauri. Hivyo Kituo cha Afya cha Mtina kitakarabatiwa wakati huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Kituo cha Afya cha Mchesi ni kituo cha kimkakati kilichoanza kufanya kazi mwishoni mwa Desemba, 2023, lakini mpaka sasa kina mtu mmoja tu ambaye anatoa huduma. Mganga huyo huyo, *Nurse* huyo huyo na mhudumu ni huyo huyo. Ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha ili kile Kituo cha Afya cha Mchesi kifanye kazi kama kituo cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kituo cha Afya Nalasi ni kituo cha afya kilichojengwa na halmashauri kwa milioni zaidi ya 600 na vifaatiba kupelekwa katika kituo kile, lakini mpaka leo vile vifaa havijafungwa, ni lini Serikali itafunga vifaa vile na kupeleka watu ambao watatoa huduma sahihi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo wamefanikiwa kufuatilia na kuanza huduma katika Kituo cha Afya cha Mchesi, Jimbo la Tunduru Kusini, lakini nimhakikishie tu kwamba, Serikali imeweka kwanza utaratibu wa kufanya msawazo wa ndani wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, kuhakikisha anaangalia namna ambavyo anaweza akapata watumishi ndani ya mkoa kwa ajili ya kuwapeleka kwenye Kituo hiko cha Afya cha Mchesi angalau kuongeza nguvu wakati tunasubiri ajira hizi ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa hivi karibuni na tuko hatua za mwisho za kupeleka watumishi kwenye vituo hivyo ili kupunguza upungufu wa

watumishi katika kituo hicho. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo hicho kitapata watumishi na kitaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na vifaatiba katika kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja. Ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali imeshapeleka vifaatiba na kwa bahati njema umesema, lakini ni muhimu kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tunduru na Mganga Mkuu wa Mkoa kuhakikisha wanawasiliana mara moja na wale Wazabuni walioleta vile vifaa kwa ajili ya kufunga vifaa hivyo mapema iwezekanavyo ili vianze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapa muda wa wiki mbili na tutafuatilia kuona kwamba wameshafunga vifaa hivyo na vimeanza kutumika katika kituo hicho cha afya. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati na kuweka jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya cha *Round Table* Mbagala Kizuiani? Kituo hicho ni cha muda mrefu, mama anapozidiwa inabidi atafutiwe gari kupelekwa Temeke au Zakiem, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweka jengo la upasuaji?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Afya cha *Round Table* kule Mbagala ni kituo cha muda mrefu na ni kituo ambacho kinahudumia wananchi wengi. Serikali tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye vituo vya afya ambavyo vina uhitaji mkubwa wa majengo, kama Kituo cha *Round Table* kule Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inalichukua jambo hili kwa uzito unaostahili, lakini nimuagize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwenda kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha ambazo zinatakiwa kuboresha kituo hicho cha afya, kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini pia kufanya tathmini ya uwezo wa mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuanza ukarabati wa kituo hicho cha afya mapema iwezekanavyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Gekul.

Na. 126

**Ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi – Babati**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa stendi kuu ya mabasi Babati ambayo ni Stendi Kuu ya Mkoa wa Manyara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi katika Halmashauri ya Mji wa Babati unafanyika chini ya Mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Miji ya Tanzania kwa Kuhusisha Ushindani *"Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness'' (TACTIC)* awamu ya Pili. Utekelezaji wa mradi huo unaendelea ambapo kazi ya usanifu imekamilika na sasa maandalizi ya zabuni yanafanyika kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Umma wa *NeST* kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mshauri Msimamizi kwa lengo la kuanza kazi za ujenzi. Ujenzi unatarajiwa kuanza Februari, 2025 baada ya kukamilika kwa taratibu za kumpata Mkandarasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali kutupatia fedha hizi zaidi ya bilioni 17 kwa ajili ya ujenzi huu naamini utakamilika. Nina swali moja tu, Mji wa Babati ni Makao Makuu ya Mkoa tuna uhitaji mkubwa wa ujenzi wa soko kuu. Je, Serikali iko tayari kututengea fedha kwa ajili ya soko kuu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Mji wa Babati ni mji ambao unakua haraka, lakini una uhitaji mkubwa wa soko. Mheshimiwa Mbunge Gekul amefuatilia mara nyingi sana Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuona namna ambavyo wananchi wa Babati Mjini wanapata Soko Kuu. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wetu wa Miji na Halmashauri kuweka vipaumbele katika ujenzi wa masoko, lakini pia kuandika maandiko maalum kwa ajili ya maombi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Hamalshauri ya Mji wa Babati waandike andiko la mahitaji ya soko hilo na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuingizwa kwenye miradi ya kimkakati ili itafutiwe fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wingi wa watu katika Jimbo la Mbagala, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Stendi ya Mabasi ya Kusini pamoja na mabasi ya kwenda katikati ya Jiji la Dar es Salaam?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote

ambayo yana sifa na yanahitajika kujenga stendi kwa ajili ya kusogeza huduma za jamii karibu zaidi na wananchi, kuongeza mapato ya halmashauri kwa kujenga stendi hizo. Ni kweli kwamba Jimbo la Mbagala ni moja ya majimbo yenye idadi kubwa ya wananchi na uhitaji wa stendi ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishaanza kufanya utaratibu wa kutafuta eneo, lakini pia kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga stendi ya mabasi ya Kusini, lakini pia mabasi yanayokwenda katikati ya mji. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala hilo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize pia kwa Mkurugenzi kuweka kipaumbele kwenye bajeti za mapato ya ndani ya Manispaa ya Temeke ili kushirikiana na Serikali Kuu tuone namna nzuri ya kujenga stendi hiyo kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Chemba unakua kwa kasi sana. Ninataka kujua ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi, ambapo tayari andiko tumeshaleta kwenye Ofisi ya TAMISEMI.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Chemba walishawasilisha andiko la ujenzi wa stendi na tayari limeshafanyiwa uchambuzi katika ngazi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na limeshawasilishwa Hazina. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Chemba kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hilo la stendi ya Chemba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mkoa katika Mji wa Vwawa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hasunga na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Songwe mara nyingi wameulizia kuhusiana na ujenzi wa stendi ya Mkoa wa Songwe na Serikali siku zote tumewahakikishia kwamba, ni kipaumbele cha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mipango ya Serikali bado inaendelea na tunahakikisha kwamba tutapata fedha kwa ajili ya ujenzi wa Stendi ya Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mkundi.

Na. 127

**Walimu Kuchelewa Kubadili Muundo baada ya Kujiendeleza**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, nini husababisha kuchelewa kubadilishiwa Muundo wa Utumishi kwa Walimu mara baada ya kujiendeleza kitaaluma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewa kubadilishiwa Muundo wa Utumishi kwa Walimu mara baada ya kujiendeleza kitaaluma husababishwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:-

(i) Walimu husika kuchelewa kuwasilisha vyeti vya taaluma kwa wakati mara baada ya kuhitimu;

(ii) Baadhi ya Walimu kujiendeleza kitaaluma bila mwajiri kuwa na taarifa hali inayosababisha kutoingizwa kwenye Bajeti na Ikama kwa ajili ya kubadilishiwa miundo ya utumishi kwa wakati; na

(iii) Walimu kutowasilisha vyeti vya taaluma kwa kuhofia kutumikia cheo kimoja chenye mshahara ule ule kwa muda mrefu kabla ya kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, walimu 4,917 kati ya watumishi 5,110, sawa na 96% wamebadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza kitaaluma. Aidha, walimu 156,162 kati ya watumishi 227,290 sawa na 69% wamepandishwa cheo. Ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini pamoja na majibu hayo kuna ukweli kwamba kuna baadhi ya matatizo kwa watumishi wetu yanasababishwa na uzembe au kukosa weledi kwa baadhi ya Maafisa Utumishi. Kwa mfano, kuna walimu walioajiriwa mwaka 2018 mwezi Aprili, wamepandishwa madaraja mwaka 2021/2022, lakini mwaka huo huo kuna baadhi ya walimu wamepandishwa madaraja mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kwamba walimu wameajiriwa mwaka mmoja lakini wanatofautiana sana kimuundo na kimaslahi. Je, Serikali haioni kwamba inawakatisha tamaa walimu hawa na kwa hiyo ina wajibu wa kuchukua hatua kufanya marekebisho hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna walimu walioajiriwa kabla ya mwaka 2018, lakini wana sifa zilezile sawa na wale walioajiriwa mwaka 2018 kuendelea na wamepandishwa madaraja, wale walioajiriwa kabla hawajapandishwa madaraja.

Serikali inasemaje katika kuwarekebishia muundo walimu hawa walioajiriwa kabla ya mwaka huu? Ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mkundi kwa namna ambavyo anawasemea walimu wa Tanzania, lakini kipekee walimu wake katika Jimbo la Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja, kwanza ninaomba nimwondoe shaka, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, haina nia na wala kwa wakati wowote haitawakatisha tamaa walimu wa Tanzania kwa sababu wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada kubwa imefanyika, kwa Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni 252.7 kwa ajili ya kutatua changamoto hizo ikiwemo kuwabadilishia miundo wale waliocheleweshewa na wale ambao walistahili kupandishwa vyeo ambapo Maafisa Utumishi hawakuleta taarifa Ofisi ya Rais Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupitia Bunge hili, nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuwaelekeza waajiri kwa maana ya Wakurugenzi, wakishirikiana na *TSC*, kuhakikisha walimu wote waliosahaulika kwenye suala la miundo na *promotion*, walete taarifa hizo Ofisi ya Rais Utumishi ili tuweze kutatua changamoto hii. Ninashukuru. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri anasema, walimu wanaenda kujiendeleza bila mwajiri kujua ndiyo maana inakuwa ngumu kwa Serikali kuweza kuwapandisha. Hamwoni kama

mnawakatisha tamaa kwa kuwa Serikali haina fedha ya kuwasomesha au kuwaendeleza walimu hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Nitoe ufafanuzi, kwenye hili, walimu ninaowaongelea ni wale ambao hawakuomba ruhusa wakajiendeleza bila mwajiri kufahamu, lakini hata hivyo baada ya kujiendeleza Serikali inatambua jitihada kwa kuwa tunaamini mwalimu anapojiendeleza anakuwa na tija katika kazi yake. Kwa hiyo ninaomba nimwondoe shaka Mheshimiwa Sophia kwamba hata hawa baada ya kutambulika, tayari Serikali kama nilivyosema imeandaa bajeti nao watapewa kipaumbele, hakuna mwalimu atakayesahaulika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Tamima Haji Abass.

Na. 128

**Utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kaskazini "A" Zanzibar**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kupitia mfumo ekolojia Wilaya ya Kaskazini "A" Zanzibar umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo ya Ekolojia Vijijini *(Ecosystem-based Adaptation for Rural Resilience - EBARR)* unaotekelezwa

katika Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa kwa upande wa Tanzania Bara na Kaskazini A - Unguja upande wa Zanzibar. Mradi huu unaratibiwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kaskazini *A* – Unguja, mradi huu unatekelezwa na umefikia katika 95% ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.4 zimetolewa. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaliwa kwa Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika Shehia za Matemwe Kijini, Mbuyutende na Jugakuu; uchimbaji na ujenzi wa visima sita; ujenzi wa vitalunyumba *(Greenhouse)* vitatu kwa ajili ya kilimo cha mbogamboga; ununuzi wa boti sita za kisasa na vifaa vya uvuvi; ujenzi wa vituo vitatu vya ufugaji, utengenezaji wa sabuni na ushonaji; ununuzi wa vyerehani 42 kwa ajili ya vikundi vya ushoni na upakasaji; ununuzi wa mizinga ya nyuki 200; mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vyote; kuanzishwa kwa vitalu vya miche 56,000; na utengezaji wa majiko banifu kwa kaya 125. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tamima.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninashukuru kwa majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha miradi hii inaifuatilia ili kuona kama inadumu na inawanufaisha wananchi baada ya kukamilika kwake?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha inapotoa miradi ya mabadiliko ya tabianchi inakuwa inatumia vigezo gani? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tamima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote tunapokuwa tunaanzisha miradi lazima tunakuwa tunafanya ufuatiliaji. Hatua ya kwanza inakuwa ni hatua ya kufanya tathmini na ufuatiliaji ili kujua mradi huo umefikia wapi na umenufaisha wananchi ama walengwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanzisha ama tunao uwepo na maafisa wetu viungo, wapo huko katika wilaya, mikoa na kwenye halmashauri. Tuna Maafisa wa Mazingira wa Mikoa, tuna Maafisa wa Mazingira katika wilaya ambao pia huwa tunawatumia katika kufuatilia miradi hiyo na kujua imewanufaisha wananchi kiasi gani, lakini hata kupitia ziara za viongozi kwa mfano Kamati za Waheshimiwa Wabunge, Kamati za Wawakilishi. Binafsi, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira tulishawahi kuutembelea mradi huu na tukajiridhisha tukaona mradi huu umefikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa vigezo gani tunatumia, kwanza tunafanya tathmini za kitaalam ili kujua wapi panahitajika kipi kwa ajili ya kuondosha changamoto ya athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, lakini kikubwa kupitia Mpango wetu, Mpango kabambe wa Mazingira wa miaka 10 ambao ndani yake umeeleza maeneo ambayo yameathirika kimazingira na hatua ambazo tunaweza tukazichukua. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Usonge.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano na wadau wa maendeleo *(Global Environment Facility)*, mradi huu ulitakiwa ukamilike ndani ya kipindi cha miaka mitano tokea mwaka 2018 – 2022, lakini mpaka leo hii na umekiri hapo kwenye maelezo yako, umeshafikia 95%. Je, ni ipi *commitment* ya Serikali kukamilisha mradi huu ambapo tayari umeshavuka malengo na muda uliopangwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotoa melezo katika majibu yangu ya msingi kwamba kwa sasa tumefikia 95%. Sasa inawezekana kwa 95% maana yake bado ziko asilimia tano zimebakia. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba hapa katikati kuna mambo kidogo yalitokea, changamoto za miradi kama unavyojua lakini ninamwahidi Mheshimiwa kwamba mradi huu tunakwenda kuumaliza ili sasa uweze kukamilika 100% kama ambavyo unatakiwa ili sasa wananchi waendelee kunufaika na mradi huu kama tulivyoeleza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mwenisongole.

Na. 129

**Kumpata Mkandarasi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, lini mchakato wa kumpata mkandarasi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba utaanza ili ijengwe kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba yenye urefu wa kilometa 130 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Tayari Serikali imekamilisha ujenzi wa Daraja la Momba lenye urefu wa meta 84 na imesaini mkataba na Mkandarasi tarehe 21 Oktoba, 2024 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mpapa- Mkonko lenye urefu wa meta 60. Aidha, taratibu za manunuzi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa tano kuanzia Mlowo kuelekea Kamsamba na nyingine tano kuanzia Kamsamba kuelekea Mlowo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, hii barabara ilikuwa ni kilio kikubwa sana cha Wananchi wa Mbozi na Mkoa mzima wa Songwe. Sasa Mheshimiwa Waziri unasema taratibu za manunuzi zinaendelea; sasa, ni lini hizo taratibu zitakamilika kwa sababu tunaelekea kwenye masika ili mkandarasi aanze kazi haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari *tender* ilishatangazwa na zabuni zimeshafunguliwa na tunavyoongea sasa hivi wako kwenye tathmini *(evaluation)* ili kumpata mkandarasi ambaye atajenga hiyo barabara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, Barabara ya Singida – Kwa Mtoro – Kiberashi (Tanga) ni barabara ambayo ilisainiwa mkataba mwaka jana mwezi wa sita kwa Mfumo wa *EPC+F*. Nini tamko la Serikali kuhusiana na barabara hiyo maana wananchi wanaisubiria kwa hamu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote ambazo zilikuwa kwenye Mpango wa *EPC+F,* ninadhani nimejibu mara ya pili ama ya tatu sasa hivi kwamba Serikali imeamua kuunda timu maalum ambayo itapitia ile mikataba na kuja na utaratibu mpya ili kwanza tuhakikishe kwamba barabara hizo zinaendelea kutengenezwa na tuje na utaratibu mpya wa kuzijenga hizo barabara ikiwepo na hiyo Barabara ya Kiberashi – Kwa Mtoro ambayo Mheshimiwa Mbunge ameulizia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Wakati Serikali inaendelea kuweka sawa na mkandarasi wa zege sehemu ya Njombe – Lusitu, upi mpango wa Serikali kutengeneza kwa changarawe sehemu ambayo wananchi wataweza kupita masika ikizingatiwa mvua imekaribia kuanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kandarasi zote za barabara, pale ambapo mkandarasi ameshapewa kazi, anakuwa na wajibu pia wa kuhakikisha kwamba barabara zile zote ambazo ni za mchepuko kwa maana zinatumika wakati ile barabara kubwa inajengwa, lazima ahakikishe kwamba hizo barabara zinapitika. Kwa hiyo mkandarasi aliyepo ndiye atakayejenga ile barabara ya muda wakati anajenga ile barabara ya kudumu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Toufiq Turky, kwa niaba yake Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 130

**Kudhibiti Ukuaji wa Makazi katika Maeneo ambayo Hayajapimwa**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti ukuaji wa makazi katika maeneo ambayo hayajapimwa na kupangwa kuwa makazi ya wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika kukabiliana na ukuaji wa makazi yasiyopangwa, imeendelea kuchukua hatua mbalilmbali ambazo ni pamoja na kuendelea kuandaa Mipango Kabambe *(Masterplan)* yenye dira ya kusimamia ukuaji wa miji. Aidha, Wizara imeanzisha miradi na programu mbalimbali kwa ajili ya kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa mpango huu ambao Serikali inauita KKK, ilikuwa ni programu ambayo Serikali imetoa pesa nyingi, lakini inavyoonekana hakuna ufuatiliaji mkubwa wa pesa hizi kiasi kwamba kwenye halmashauri zetu miradi hii haifanyiki kwa ufanisi. Je, Serikali ina mpango gani mahsusi kuhakikisha kwamba miradi hii inakwenda kutekelezwa kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wananchi wa Kata ya Pugu Jimbo la Ukonga wako katika mpango huu na wengi wameshalipa pesa takribani shilingi 250,000/= kwa kila kaya, lakini mpaka sasa mpango ule umesimama. Ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wale wanarasimishiwa ardhi yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwanza la KKK, ni kweli Serikali hasa hii Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka fedha nyingi sana katika mradi huu wa KKK. Tulishirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na fedha hii ikaenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilichagua wao maeneo ambayo walitaka kuyapanga, kuyapima na kumilikisha. Sasa, fedha hii kuna maeneo ninakiri kwamba ilienda na badala ya kutumia fedha hii kwa ajili ya kupima, kupanga na kumilikisha, walipeleka fedha hii kwenye shughuli nyingine. Hata hivyo, kwa sasa ninawasifu na kuwapongeza wenzetu wa TAMISEMI, wamekuwa wakishirikiana nasi kwa karibu sana, vilevile kupitia Kamati ya Bunge ya TAMISEMI katika kuhakikisha halmashauri zinarejesha fedha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali la pili la Pugu – Ukonga, Manispaa au Jiji la Dar es Salaam ambayo ni Ilala iliingia mkataba na kampuni za urasimishaji ambapo kampuni hiyo ilienda, ilichukua fedha kwa wananchi lakini hawakukamilisha kazi ile. Ninampa taarifa tu Mheshimiwa Shangazi kwamba Wizara sasa imeona tuingilie hili kuhakikisha kwamba wananchi wale waliotoa fedha yao, wanapata ule urasimishaji walioutarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunafanya kazi kwa karibu sana na Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha kwamba tunawapa wananchi hawa urasimishaji waliokuwa wanautarajia. Niseme tu mwishoni, kwamba vilevile tumeanza kufanya *audit* ya hizi kampuni zote za urasimishaji ili tuweze kuona uwezo wao wa kutekeleza majukumu ambayo wanaenda kuyaomba kule kwenye halmashauri mbalimbali hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kule Musoma kwenye hili zoezi la urasimishaji unakuta watu waliotarajiwa kupimiwa kwenye hilo eneo labda walipaswa kuchanga watu 100 na kila mmoja akachanga labda shilingi 150,000/=, lakini kati ya hao, wamechanga nusu na nusu wengine hawakuchanga na kutokana na hali hiyo yale maeneo yameshindwa kupimwa, lakini na wale waliokwishachanga fedha zao zimekaa kule…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** … tunawasaidiaje watu kama hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishasema wakati najibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi na kwa Mheshimiwa Manyinyi kule kunafanana, kwamba ni zile kampuni ambazo ziliingia makubaliano na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwenye kesi ya Mheshimiwa Manyinyi ina maana na Manispaa ya Musoma ndizo ambazo zilileta changamoto hizi kwa wananchi. Kwa hiyo ndiyo maana tunaangalia upya utaratibu wa kampuni hizo kufanya kazi katika urasimishaji kwenye halmashauri mbalimbali hapa nchini na baada ya hapo ninaamini changamoto hizi zitaisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Hivi ni kwa nini Makao Makuu kwa mfano hapa Dodoma wananchi bado wanafanya ujenzi holela wakati hapa ndiyo uso wa nchi na ni makao ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, narejea kwenye majibu yangu ya msingi nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tendega kwamba sasa Wizara tunahakikisha tunafanya kazi kwa karibu sana na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuhakikisha tunapanga, tunapima na kumilikisha. Tunawasisitiza sana wenzetu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha watu wanaojenga wawe na vibali vya ujenzi. Vibali vile vinatokana na maeneo ambayo yameshapimwa na kurasimishwa kwa hiyo tunaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na wenzetu wa Mkoa wa Dodoma na Jiji la Dodoma kuhakikisha kwamba changamoto hizi sasa zinaendakwisha kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

Na. 131

**Raia wa Kigeni Kutoshiriki Uchaguzi Nchini**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Raia wa Kigeni hawashiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 na kanuni zake za mwaka 2024, raia wa Tanzania ndio wenye haki ya kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu kwa kupiga kura au kuchaguliwa kuwa Viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia vipindi vyote wakati wa uchaguzi, Serikali imekuwa ikitoa elimu ya uraia kwa watendaji (waandikishaji na wasimamizi wa uchaguzi) ili kuhakikisha raia wa Tanzania wenye sifa ndio wanaoshiriki katika chaguzi na sio raia wa kigeni. Aidha, inapobainika kwamba kuna mtu anadiriki kujiandikisha ama kutafuta fursa ya kugombea na zipo taarifa au tuhuma, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uchaguzi, mhusika huyo huwekewa pingamizi na ikithibitika mtu huyo huchukuliwa hatua za kisheria ikiwepo kuondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura sanjari na kufikishwa Mahakamani, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; nchi yetu imekuwa na matukio ya wananchi kuchonganishwa hasa Jeshi la Polisi lakini kweli ni kwamba wanaofanya matukio ni watu wengine wakitumia mgongo wa Jeshi la Polisi. Ni ipi kauli yako ya kuhakikisha kwamba unawalinda Askari na kuondoa utapeli unaofanya na watu wabovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi. Kwenye sheria zetu, maandamano na mikutano ni vitu vinaruhusiwa zinapoanza kampeni. Mmejipangaje kuhakikisha kwamba wanasiasa tunalindwa kikamilifu na kuhakikisha tunamaliza mikutano salama na maandamano yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, swali la pili halitajibiwa, halipo kwenye swali la msingi. Mheshimiwa Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inaongozwa kwa mujibu sheria na taratibu kwa hiyo kama wapo watu ambao wanafanya fujo au kuchonganisha wananchi kwa kutumia Jeshi la Polisi, ninaomba kutoa wito kwa watu hao waache tabia hiyo mara moja na watakaobainika sheria itachukua mkondo wake ikiwepo kufikishwa Mahakamani. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Hussein Amar.

Na. 132

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Ujenzi wa Gereza Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia ya shilingi 236,000,000 kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Nyang'hwale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua madai ya Shilingi 235,271,532.30 kama fidia ya wananchi 31 wa Kijiji cha Busengwa, Kata ya Kharuma, kwa ajili ya kupisha eneo la ujenzi wa Gereza la Wilaya Nyang'hwale. Madai haya hayakuingizwa kwenye Mpango wa Bajeti wa mwaka 2024/2025 kutokana na kutokamilika kwa daftari la orodha ya wanufaika kwa wakati na badala yake fedha hiyo itaingizwa katika Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ili kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi husika kama mapendekezo ya taarifa ya Mthamini Mteule yalivyowasilishwa, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nianze kuipongeza Serikali kwa kutambua fidia ile ya wananchi 31 ya Kijiji cha Busengwa. Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja ya kuanza kuandaa michoro ya gereza hilo ili fidia hiyo itakapolipwa ujenzi uanze?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali haioni kufanya ujenzi huo kwa haraka, ili kuokoa gharama za wananchi kufuata huduma hiyo ya magereza kutoka Nyang'hwale kwenda Geita zaidi ya kilometa 130?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuandaa michoro. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, michoro itaandaliwa haraka iwezekanavyo lengo letu ni tuhakikishe kwamba, gereza hili linajengwa haraka, ili kuhudumia wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu ujenzi kuanza haraka. Kama nilivyosema, baada ya kukamilisha michoro hatua inayofuata ni tutatenga fedha kwenye Mwaka 2025/2026, baada ya hapo ni kuanza ujenzi mara moja, ili wananchi wasipate tabu ya kutoka Nyang'hwale kwenda Geita ambako ni umbali mrefu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Gereza la Wilaya ya Liwale limejengwa Mwaka 1982, lakini wananchi waliopisha ujenzi wa gereza lile mpaka leo hawajapata fidia. Nini Kauli ya Serikali ya kuwapatia fidia wananchi wale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jambo hili nilichukue na niagize Jeshi la Magereza kwenda kufanya tathmini katika eneo hilo, ili wananchi hawa wapate fidia, kama ambavyo walitoa eneo hilo, kwa ajili ya ujenzi wa magereza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu ametoka? Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itatoa majibu kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa Gereza la Keko kwa sababu, Gereza la Keko wanalalamika ni eneo lao, lakini wananchi wanaozunguka hapo

wana vithibitisho maalum kabisa kwamba ni eneo lao. Je, ni lini Serikali itaenda kutatua tatizo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mgogoro huo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaenda.

**NAIBU SPIKA:** Eeh, fanyeni mpango Mbunge na Mheshimiwa mkatembelee eneo hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Kishapu wamechangia jumla ya shilingi milioni 250, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Wilaya. Ni lini Serikali itatimiza ahadi iliyoahidi kwa ajili ya kuwachangia ili wakamilishe mradi huo na uweze kufanya kazi? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu rudia tena swali lako.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya ya Kishapu wameshapata eneo, kwa ajili ya ujenzi wa magereza na tayari taratibu zote za fidia zimeshafanyika na Serikali ilishaahidi kwamba, itakwenda kutekeleza ujenzi huo kuanzia Mwaka wa Fedha 2024/2025. Je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa? Ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Naliruhusu kwa upendeleo, Mheshimiwa Naibu Waziri mjibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshatenga fedha kwenye Mwaka huu wa Fedha 2024/2025. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, *as long as* tumeshatenga fedha na bado mwaka wa fedha unaendelea, basi tutatekeleza mradi huo kwa ujenzi wa magereza katika jimbo lake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Tadayo.

Na.133

**Kufunguliwa kwa Lango la Kaskazini la Hifadhi ya Taifa Mkomazi, Mwanga**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafungua na kuanza kutumia Lango la Kaskazini la Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, lililojengwa Ndea, Mwanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ipo katika hatua mbalimbali za kufanya maboresho ya miundombinu ya utalii pamoja na kuongeza malango ya wageni ili kufanikisha watalii kufika katika vivutio vilivyopo kwenye Hifadhi za Taifa Tanzania, ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Kwa sasa ujenzi wa lango la kupokelea wageni katika eneo la Ndea, ndani ya Hifadhi ya Taifa Mkomazi umekamilika. Pia, barabara inayounganisha Hifadhi ya Taifa Mkomazi kupitia lango hilo na Wilaya ya Mwanga hadi kufika katika Kijiji cha Karamba, Ndea, yenye urefu wa kilometa 18 imeshafunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 78, kwa ajili ya kuiboresha barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, ili iweze kutumika kwa shughuli za utalii katika msimu mzima wa mwaka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja tu la nyongeza. Tarehe 27 na 28 Disemba, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mwanga na Ofisi ya Mbunge wa Mwanga ikishirikiana na Kampuni ya *Kisangara Tours* tumeandaa tamasha la utalii, ambapo mojawapo ya maeneo yatakayopitiwa katika marathoni ni lango hili la Ndea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, lango liko tayari na barabara iko tayari kilichobaki ni kuimarisha tu ipitike misimu yote. Je, yuko tayari kuwahakikishia wananchi wa Mwanga kwamba, kabla ya tarehe 27 na 28 Disemba lango hilo litafunguliwa ili tamasha letu la marathoni liweze kufika kwenye lango la Ndea? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, timu yetu inayoshirikiana na wilaya kufanya maandalizi, ikiwemo Ofisi ya Mbunge, inashughulikia jambo hili. Nimhakikishie kwamba, uzinduzi wa lango hili utakuwa sehemu ya shughuli hiyo ya tamasha kuanzia tarehe 27 na 28 Disemba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Nini mkakati wa Serikali wa kuimarisha barabara

zilizoko ndani ya hifadhi zetu, kwa mfano, Barabara ya kutoka Ngorongoro kuelekea Serengeti ambayo ni mbovu sana?

**NAIBU SPIKA:** Swali lilikuwa mlango; barabara, haya, Mheshimiwa Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inafanya kazi ya kuboresha kilometa 400 zilizoko ndani ya hifadhi zetu. Nimhakikishie kwamba, barabara aliyoitaja tunaipa kipaumbele kwa sababu, ni barabara muhimu sana kwa ukuaji wa utalii wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wizara ya Maliasili, Waziri aliahidi kutuletea mizinga ya nyuki, Yaeda Chini, je, ni lini ahadi hii itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usambazaji wa mizinga ya nyuki linashughulikiwa na litakapokuwa tayari tutawataarifu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itafungua barabara na lango la Seleto kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wa Kata za Leguruki na King'ori kiuchumi? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, ameuliza ni lini, naomba baada ya hapa tukutane na Mheshimiwa Mbunge, ili tuweze kulijadili jambo hili. Tuweze kumpa majibu ya uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wapo wageni 10 wa Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu Rajabu Abrahman, Mwenyekiti wa CCM Mkoa. *(Makofi)*

Wageni sita wa Bunge, Kamati ya Kampeni ya Kitaifa ya Mtoto Mboni Yangu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka Zanzibar, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti, Ndugu Daima Mkalimoto.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 109 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, wanafunzi 99 na Walimu 10 wa *Nyangao High School* kutoka Mtama Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika. Wanafunzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Ujenzi, Wajumbe wa Bodi ya Karagwe *District Cooperation Union Limited* kutoka Karagwe, Mkoa wa Kagera, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Mwandishi wa kitabu maarufu kiitwacho “Uongozi Wako Historia Yako” kutoka Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndigo, mpiga kura wake kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, ambaye pia, ni mpiga kura wake kutoka Kigoma Kusini. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Daktari Ritta Kabati, Mchungaji Kiongozi wa kanisa la *Enlighted Christian Gathering (ECG)* kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kachauka, mke wake ameambatana na shemeji yake kutoka Liwale, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa haya makofi ya mke au shemeji? *(Kicheko/Makofi)*

Tuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, rafiki zake kutoka Jijini Dodoma. Wapo wawili wa Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, hawa ni Wenyeviti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Kigoma na Manyara. *(Makofi)*

Tuna mgeni mmoja vile vile wa Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, wananchi kutoka Kibaha. *(Makofi)*

Kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Katibu wake ambaye ameambatana na wapigakura wake kutoka Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, hawa ni watoto na shangazi yake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Jafari Chege Wambura ambao ni wapigakura wake kutoka Rorya Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni wengine 29 wa Mheshimiwa Jafari Chege Wambura, hawa Walimu wa Shule ya Sekondari na Msingi kutoka Rorya Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ambao ni familia yake, wameambatana na ndugu zake kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, hawa ni Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Muuzaji wa Vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya matone kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Mariam Omar Said, shemeji yake kutoka Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; wageni wawili ambao ni watumishi wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 12 wa *Bunge Sports Club* ambao ni Makocha wa Timu za Michezo za Bunge. *(Makofi)*

Tuna pia wanafunzi 35 na Walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi *Saint Mattie* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wajumbe wa Kamati ya Kampeni ya Kitaifa inayoitwa Mtoto Mboni Yangu, yenye lengo la kuhamasisha wananchi kuwalinda watoto dhidi ya mmomonyoko wa maadili pamoja na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar, wanawaalika Waheshimiwa Wabunge, kukutana na kamati hiyo katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge leo saa saba mchana, ili kupata elimu

kuhusiana na kampeni hiyo. Waheshimiwa Wabunge, wote wenye nafasi wanaombwa kukutana na kamati hiyo muhimu, kwa ajili ya ustawi wa watoto, wanawake na wazee. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL Mpanda – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**
**na**
**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, wajiandae Mheshimiwa Muhongo na Mheshimiwa Ntara.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi ili niweze kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwapongeze sana Mawaziri wawili waliohusika kabisa kwenye matayarisho haya ya awali ya mapendekezo haya yaliyopo mbele yetu. Hali yetu ya uchumi, kama nchi, ina mwelekeo mzuri na kwa kweli, ukilinganisha na majirani zetu Tanzania tuna kila sababu ya

kusema tuna uongozi bora na imara wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi sana kutotambua au kuona mambo yanakwenda kawaida, lakini ukitaka ujipime kama unafanya vizuri, jilinganishe na wenzako katika eneo ambalo unafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo letu sisi tunaangalia Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za *SADC*. Kwa ujumla wake Tanzania kiuwekezaji ni nchi ambayo inafanya vizuri zaidi kuliko nchi karibu zote za *East Africa* ukiacha Rwanda ambayo ina sababu zake maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia mpango na mapendekezo ya mpango huu kuna mambo mengi ambayo yanajitokeza. Mpango huu dhima yake kubwa ni uchumi shirikishi na shindanishi na mimi ndipo mahali ambapo napenda hasa niweze kuongelea angalau kwa kifupi kwa muda ambao nimepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna sekta ambayo tunatakiwa tuiangalie kwa makini sana katika kuangalia dhima hii ambayo tunaingalia iko mbele yetu ni Sekta ya Kilimo. Sekta hii mchango wake kwenye pato la Taifa ni 26.5% wote tunafahamu ni sekta ambayo inakua na imekua mpaka kufikia kama asilimia nne, lakini bado ina *potential* ya kukua. Muhimu zaidi ni kwamba sekta hii asilimia kubwa ya Watanzania iko huko 45.9% ya wananchi wa Tanzania kwa sensa iliyopita wote ni wakulima, humu ndani sisi Wabunge ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu zaidi mchango wake kwenye uchumi kwa maana ya *export* ni kubwa. Kwa hiyo, ushauri wangu mkubwa na hasa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo ni kwamba kwa kweli tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba miradi yote ya kilimo ambayo inaenda kubadilisha au kushirikisha wananchi walio wengi ni lazima katika mpango unaokuja tuhakikishe kwamba inapewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umwagiliaji ninapenda kusema kwamba ina gharama kubwa, lakini tukubaliane kwamba kilimo kina changamoto nyingi sana. Moja ya changamoto kubwa ambayo tunayo kwa nini hatuwezi kuwa na tija ni umwagiliaji. Kwa hiyo, tuombe sana tumeanza kuona dalili kwamba pembeni mambo ni mengi, lakini fedha hazitoshi. Kwa hiyo, tuangalie mambo ambayo ni msingi kwa kilimo ni mengi, umwagiliaji ni mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Miradi ya *BBT*. Hii ni miradi ambayo inawaleta vijana kupata ajira, miradi ambayo inawaondoa vijana na tushukuru Serikali kwamba ilibadilisha mfumo mwanzoni tulikuwa na wasiwasi, sasa hivi wanachukuliwa vijana ambao tayari wako kwenye kilimo kwenye maeneo ya halmashauri zetu. Halmashauri zilizotenga maeneo tayari zimeingizwa kwenye miradi hiyo, kwa hiyo niombe Serikali isisite kuendelea kutoa fedha katika Miradi ya *BBT* kwa sababu ni miradi ambayo itatubadilishia maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu tukaliangalia ni eneo la uzalishaji wa viwanda. Tukiangalia Nchi kama Korea miaka 60 iliyopita Korea Kusini haikuwa tofauti na Tanzania, mchango wake kwenye pato la Taifa haukutofautiana na Tanzania na Tanganyika wakati ule na baadaye Tanzania, lakini ukweli ni kwamba *South* Korea imetuacha mbali sana. Ukifuata wanazuoni wa Korea na Watafiti wanasema ni mambo kama matatu tu, lakini kubwa kuliko yote ambayo ilifanya *transformation* hiyo ni kuingia kwenye viwanda na uzalishaji wa mazao ya kilimo kwenda kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *agro-processing* kwetu sisi ni jambo ambalo ni lazima tulitilie maanani sana na ninaomba tunapoangalia *agro-processing* tuangalie viwanda vingi kwa ukubwa wake. Ukiangalia viwanda kama vya *TBL* au viwanda bia kwa ujumla wake, tutasema ni bia vinatupa mapato lakini vina *impact* kubwa sana kwa wakulima wetu kule katika maeneo yetu. Kwa hiyo, tujitahidi kuhakikisha kwamba tunaondoa changamoto ambazo viwanda vikubwa vyenye *impact* kwenye wazalishaji wakulima vinaondolewa changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tumeanza kuona polepole kwamba Serikali inatakiwa itoe msukumo mkubwa sana kwenye kuboresha mazingira ya uwekezaji na niseme wazi naishukuru Serikali, tuseme na tuwe wakweli kwamba kwa kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tumeona kwa kiasi kikubwa, hatua kubwa za uboreshaji wa mazingira ya biashara, sisi tuitie moyo Serikali na tuwaombe kwenye mpango huu bado tuendelee kutatua mambo ambayo yanaweza yakaturudisha nyuma na kwa kweli yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme machache ukiangalia moja ya vihatarishi ninavyoviona mimi ni jambo tunaloliita *uniformity* ya mifumo ya kodi katika nchi zetu za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ukiangalia kwa kiasi kikubwa tuna mikataba ambayo tumekwishaingia kwamba baadhi ya maeneo ya *customs duty* tutaendelea kuyaboresha na tutakuwa na *harmonization.* Napenda kutoa ushauri tuwe makini sana na *commitment* tunazozifanya kule, kwa sababu tuelewe kwamba sisi tuna *advantage* au tuna *competitive advantage* kwenye baadhi ya vitu. Kwa hiyo, tunapokwenda kuweka *commitment* kule tuangalie zisituondolee *competitive advantage* zetu na tuhakikishe kwamba maeneo ambayo tuna faida au tunaweza tukasukuma uchumi zaidi tuwe makini zaidi na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu nipende kulisema mojawapo, kuna mpango kwa mfano kwenye maeneo ya sigara ambako nako tuna uzalishaji mkubwa na mchango mkubwa katika uchumi wetu kwa upande wa mapato. Sasa ukienda kule kinachoongelewa sasa kupitia kwa *multi-lateral organization* kuna mpango wa ku-*harmonize excise duty* kwamba Tanzania tuna-*charge* kidogo sana ukitulinganisha na wenzetu juu ya Mlima wa Kilimanjaro, kwamba wao wako juu sana kwenye *excise duty,* kwa hiyo na sisi na nchi nyingine zote tupande tuwafikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wako katika mazingira tofauti, sisi tutapata hasara kwenye makusanyo yetu kama tukienda tukalingana au tukataka kulingana na wao na mfano tumeuona tumeongeza *excise duty* hapa karibuni. Sasa hivi

makusanyo ya Makampuni ya Bia yamekwishateremka kwa *almost* 20%, kwa sababu wanywaji wa bia wamepungua lakini siyo hilo tu, lina madhara mengine makubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Watu wengi ambao hawawezi ku-*afford* kunywa bia wanakwenda kuanza kunywa vinywaji vingine ambavyo vinawaletea madhara makubwa katika afya zao, jambo hili linaendelea kutuumiza kwenye kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakimbia, hivyo niongelee kwa haraka sana kuhusu miradi mingine mikubwa. Dira ya Taifa ya Mwaka 2025 ilisema wazi na wote tunajua ili tuweze kutoa umaskini ni lazima tuhakikishe kwamba uchumi wetu unakua kwa kiwango cha asilimia nane mpaka asilimia tisa, siyo jambo jipya lipo ndani ya dira ambayo tumeifanya miaka 25 iliyopita. Ili tuweze na wengine wanauliza kwamba hii haiwezekani, inawezekana kukuza uchumi wetu kuufikisha hapo kwenye asilimia 10. Tukitekeleza miradi mikubwa miwili miwili tu tayari tuko kwenye asilimia tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uchakataji wa Gesi *(LNG)* kule Lindi ni mradi wa kimkakati ni mradi ambao tusione haya. Sasa nafahamu wenzetu ndani ya Serikali wanaendelea na majadiliano, sisi tuwatie moyo na kuwasukuma wajitihadi ili tuweze kukamilisha. Nitoe angalizo na nimelitoa angalizo hilo kabla, kwamba wenzetu wanaowekeza lazima tuangalie tuna Serikali tuna wawekezaji, tuna wanahisa na tuna Watanzania kwa ujumla wetu, lakini tukumbuke kwamba uwekezaji mkubwa wa dola bilioni 40 utategemeana sana vilevile na soko la *LNG* gesi katika soko la duniani. Wenzetu kama hatufanyi maamuzi ambayo yanaendana na wakati tutafika mahali kutakuwa na *over supply* ya *LNG*. Miradi ya *LNG* haipo Tanzania peke yake, kwa hiyo tuombe sana Serikali ilisukume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa kumalizia kuhusu Liganga na Mchuchuma. Mradi huu umeongelewa na kila mtu, sisi tunaiomba Serikali kila mtu sasa anafahamu mradi huu hauongelewi tu na Wabunge wa Njombe, mradi huu unaongelewa na Wabunge wa Tanzania, mradi huu unatakiwa tufike mahali tufanye maamuzi. Tunatambua ugumu na *complexity* ya kukamilisha majadiliano, mimi kama Mwenyekiti wa

Kamati ya Viwanda na Biashara nafahamu tu mwelekeo ni mzuri, lakini hatuna muda. Hatuna muda kwenye huu Mradi wa Liganga na Mchuchuma, ni mradi wa muda mrefu, ni mradi ambao utabadilisha kabisa uchumi wa nchi yetu. Utafanya *growth* ya *economy* yetu, uki-*combine* hii miwili peke yake, ukaongezea na kukamilisha kwa reli, ukaongezea na reli ya *TAZARA* tayari tuko kwenye 12% ya *growth* na tunaanza kupunguza umaskini, shida yetu kubwa ni umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema Wizara ya Kilimo wanahitaji kuongezewa fedha za utafiti, kule Njombe *avocado* inaanza kupata shida kwa sababu ya magonjwa na utafiti unahitaji uwe mkubwa katika zao la *avocado.* Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Profesa Muhongo, ajiandae Dkt. Ntara, na Mheshimiwa Mulamula.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi, naomba nianze kwanza kuongea kwa kifupi ya Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuwa Musoma Vijijini nilimwomba miradi miwili mikubwa ya barabara ya kilometa 92 na kufufua kilimo kikubwa cha umwagiliaji. Nashukuru kwamba vyote nimefanikiwa, pongezi kwake na pongezi kwa *TANROADS*. Barabara wakati huo ilikuwa na gharama ya dola milioni 50, matangazo yametoka, wakandarasi wengi wameshabikia tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi. Barabara hiyo lina daraja vilevile ambalo litagharamiwa na *World Bank* nako manunuzi yanakamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji nashukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe na Wizara wanaenda vizuri hivi karibuni nadhani mwakani tunaanza kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Kwa hiyo, kutokana na hayo mapendekezo haya nayaunga mkono yote kwa sababu yana mambo ya Musoma Vijijini, baada ya hiyo sasa nije kwenye mambo makubwa ya kitaifa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mapendekezo nayaunga mkono na ninaboresha, huko vijijini kwa wakati huu hii bajeti tunayoitayarisha mwakani, maeneo matatu lazima tuyawekee mkazo sana nayo ni maji, umeme na barabara. Hivi vitatu vinahitajika kwelikweli na nadhani bajeti tutakayoitayarisha mwakani itazingatia hayo, lakini fedha itakua ni tatizo kwa sababu tuna miradi mingi huenda fedha zisitoshe. Napendekeza kwamba mbali ya vyanzo vya fedha za *TRA,* tuanze kufanya majadiliano ya kimkakati na benki zetu ili tuweze kupata *concessional rates* yaani tukope kwa riba ndogo ya asilimia mbili ili kusudi tuweze kutekeleza miradi ya maji, umeme na barabara. Vilevile tutumie *stock exchanges* kupata fedha huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa vipaumbele vinne ambavyo ni muhimu kweli tukiwa tunamalizia miaka mitano na tunaanza miaka mitano kuelekea 2050. Kipaumbele cha kwanza ambacho naomba tuzingatie ni uhusiano wa elimu na ajira na ajira tuzipate ndani ya nchi na nje ya nchi. Sasa ninafuatilia sana ajira nchi za nje, kuna upungufu mkubwa sana karibu nchi zote hata uchaguzi uliopita wa Marekani jana usidhani kwamba Wamarekani hawataki wageni, hapana! Wanataka wageni mabingwa wenye utaalam hawataki hawa *economic refugees* wataendelea kutakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Nchi kama Ulaya wameanzisha kitu kinaitwa *U Blue Card, blue card* ni kama ile *green card* ya Marekani, watahitaji watu. Nchi kama Ujerumani inahitaji wageni, wataalam wageni wa kaliba mbalimbali laki nne kila mwaka, laki nne kwa uchumi wa Wajerumani inahitaji watu, sasa maeneo ambayo yanahitajika nimeyaweka pamoja ni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni kwenye sekta ya *manufacturing;* eneo la pili, *IT;* ya tatu, *Health Care;* ya nne, *Engineering;* ya tano, *Constructions and Building Trades;* yaani wanahitajika hata hawa wajenzi, waashi na kadhalika wanahitajika nchi huko; na sita ni *Agriculture* na *Forestry*. Ukichukua Nchi kama Ufaransa unahitaji zaidi maeneo zaidi ya 25, sasa Watanzania tusing'ang'anie kazi nchini hapa, lazima tuzitafute na za huko nje, lakini lazima elimu yetu, lazima elimu yetu iendane na mahitaji ya huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hapa peke yake lazima tuwekeze kwenye masomo ya sayansi na watu wetu wajue lugha. Kuna lugha hii ya Kiingereza hata kama unashabikia sijui lugha gani huwezi ukakikwepa Kiingereza na huko wanakotangaza kazi Kiingereza ndiyo kinatumika, hakuna lugha nyingine, sana Kiingereza na Kifaransa. Sasa sayansi hapa Tanzania ndiyo wakati ule niliongelea kuhusu mitaala lazima tuirudie. Masomo ndugu zangu yanayohitajika ili hawa watu wapate hizo *skills* unahitaji *mathematics, physics…*

*(Hapa Simu Iliita)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kuna mtu anani-*disturb* na simu hapa, hebu mkate huyo, Dokta kata simu, kuna mtu alitaka kusikiliza wakati naongea siyo vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo yanayohitajika ni *mathematics, physics, chemistry, biology*, hayo hayo ni lazima tuyawekee mkazo kwenye *O-level,* halafu na lugha tuwekee mkazo *English* na *French*. Sasa tunachohitajika bajeti hii tunayoitengeneza ya mwakani, ninapendekeza tujenge maabara nyingi na tujenge na maktaba nyingi. Haiwezekani tupate *skilled workers* ikiwa kama sekondari zetu hazina maktaba, hazina maabara za sayansi. Mimi Musoma Vijijini nimeanza kujenga, lakini naomba Serikali iwekee mkazo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuonyesha jinsi ambavyo hatujafanya vizuri kwenye sayansi..,

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, looh! Tayari muda?

**MJUMBE FULANI:** Bado, endelea…

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *form four* mwaka jana walikuwa wanafunzi zaidi ya laki tano waliochukua *physics* ni 25%, *chemistry* 31%, *agriculture*

ambapo tumewekeza sana *1.6 percent*. Kwa hiyo, mipango yetu ya uchumi haiendani na mipango ya elimu ndiyo hii inaonyesha hapa. Walioenda *form six* mwaka jana, waliomaliza *form six* bila kujali ushindi wao walikuwa karibu 97,000. *Physics* 23%, *chemistry* 36%, *math's* 14%, *biology* 29%, *agriculture* tulipowekeza *one percent* kwa hiyo unaona mipango yetu haiendani na maeneo. Kwa hiyo tuweke bajeti kubwa kwenye masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili nitaenda sasa kwa haraka ili twende 10% *growth* ni uchumi wa gesi asilia na *helium*, hili nimeshawahi kuliongelea na mfano hapa natoa ni Algeria inayoongoza kwa Afrika. Algeria wana *GDP per capital ya five thousand two hundred and sixty dollars* kutokana na mambo ya gesi, wana *export* gesi kwenye *pipe* kwenda *Europe* halafu wana *export LNG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni uchumi wa kilimo. Nimechukua nchi kama Vietnam iliyokuwa vitani toka mwaka 1955 mpaka 1975, miaka 20 ya vita, leo Vietnam mwaka huu inazalisha mpunga tani milioni 27, Tanzania ambayo hatujaingia vita ya miaka 20 tunazalisha tani milioni 2.5, *GDP* ya Vietnam iliyokuwa vitani ni *four thousand three hundred forty-six US Dollars per person per annum*. Sisi ni *one thousand two hundred eleven dollars per person per annum,* kwa hiyo tuwekeze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne ni uchumi wa madini. Hili nimeshaliongelea sana, *critical minerals* na *strategic minerals*. Marekani wanahitaji aina hamsini, *European Union* aina thelathini na nne, lakini kufanikiwa hapa ni lazima *geological survey* tuiwezeshe na tuwekeze hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano ambayo itatufikisha kwenye uchumi wa 10% ni uchumi wa utalii. Hapa nimeangalia watalii kutoka nchi za nje waliokuja Barani Afrika, watalii wa nje siyo wa ndani. Egypt ilikuwa na watalii milioni 13.1, South Africa milioni 10.2 ya tatu ilikuwa Morocco ya nne ilikuwa Tunisia ya tano ilikuwa Kenya 5.6 *million,* nasi Tanzania tulikuwa wa sita, lakini ukichukua utalii maana ya utalii, ukachukua nchi inayoongoza kama Ufaransa ambayo yenyewe mwaka jana ilikuwa na watalii

zaidi ya bilioni 100 na fedha ilizoziingiza zilikuwa karibu *70 billion US Dollars* na mtu alitumia karibu Dola 700 kwa siku kwenda kufanya utalii Nchini Ufaransa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani nia yetu hapa ni kujitayarisha kutoka kwenye ukuaji wa uchumi wa asilimia tano au asilimia sita twende 10%. Kwenda huko 10% ni lazima tuwekeze kwenye hayo maeneo manne kwamba, elimu iendane na ajira, halafu ya pili tuwekeze kwenye uchumi wa gesi na *helium*. Halafu tuwekeze kwenye kilimo *(agricultural businesses),* tuwekeze kwenye madini, tuwekeze kwenye utalii. Tukifanya hivyo ile tunayopanga kwamba ikifika mwaka 2050 tufikishe dola ziadi ya 4,500 itawezekana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Profesa. Mheshimiwa Dkt. Ntara, wajiandae Mheshimiwa Balozi Mulamula na Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nitaanza kwa kuzungumzia suala zima la utafiti. Utafiti pia ni chanzo cha mapato. Ninasema hivyo kwa sababu mara nyingi tafiti zinapofanyika tunategemea iwe mikoani ama kwenye halmashauri kule, tunategemea kwamba, wale wanaopata nafasi ya kufanya tafiti warudishe majibu *(dissemination)* katika mikoa au wilaya wanazofanya. Vibali vinatolewa, wanapewa vibali, lakini mara nyingi unakuta hawarudishi ripoti kwenye wilaya au mkoa ule ambao wamefanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, eneo ninalotaka kulizungumzia hasa ni tafiti zifanyike, kubwa kwenye eneo la vifaa vya watu wenye ulemavu wa aina zote. Utafiti wa kina ufanyike na ukishafanyika tutatambua vifaa gani vinahitajika kwa aina za watu wenye ulemavu waliopo nchini. Wakishafanya hivyo ndipo tutawapatia jukumu Wizara ya Fedha au Serikali kuondoa kodi kwenye hivyo vifaa vya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo vifaa huko mitani ni ghali mno, lakini Serikali ikiondoa kodi, hawa watu wanaweza

wakapata hivyo vifaa na zile tafiti zitaonesha faida. Pia, vile vifa tutajua vya aina mbalimbali katika makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninataka kulizungumzia hapa ni kuangalia majengo yetu kwa hao watu wenye ulemavu pia.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Sheria ya Mwaka 2018 ya Umoja wa Mataifa, imetoa maelekezo katika nchi zote ambazo ni Wanachama wa Umoja wa Mataifa kutoa *exemption* kwa vifaa vya watu wenye ulemavu vikiwemo vitendea kazi kama kompyuta zao, baiskeli zao na vifaa vingine. Ninampongeza sana mtoa hoja hii kuwa amelenga malengo ambayo ni mazuri na tunamwomba Waziri wa Fedha alisimamie hili kwa kupitia *TRA* itoe suala la *exemption* kwa vifaa vya watu wenye ulemavu. Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaipokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye majengo. Haya majengo pia yanapojengwa unakuta zile sehemu za kupandia watu wenye ulemavu wanalijenga ile kitu mnaita *loop*, ile *slope* au mnaita *lamp*. Sasa ile *lamp* inajengwa…

**MWENYEKITI:** Siyo *lamp* ni *ramp*.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *that's why I was asking because I don't know*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta kwamba kwenye ghorofa la chini utaiona hiyo *ramp* imejengwa. Ghorofa ya pili,

tatu na ya nne huko juu hakuna. Kwa hiyo, mara nyingi ujenzi ule wafanye ukaguzi kuona kwamba yanajengwa katika ghorofa zote. Kama zipo tatu au nne basi yajengwe kote, yasijengwe tu hapa chini kwa kuonesha halafu yanabaki kule juu hakuna kitu.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Ikupa.

**TAARIFA**

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza mchangiaji anayeendelea kuchangia. Kwa upande wa miundombinu, siyo tu *ramp*, pia hata sehemu za vyoo siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu na hasa ukiingia kwenye hoteli unakuta choo ni kidogo sana hata mtu akiwa na *wheel chair* hawezi kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wakati anazungumzia suala la vifaa vya watu wenye ulemavu. Vifaa vya watu wenye ulemavu viliondolewa kodi, lakini unakuta bado ni ghali. Kwa hiyo, Serikali labda iendelee kufuatilia kwa nini kodi iliondolewa, lakini bado vifaa hivi vinapatikana kwa bei kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vifaa vingine kwa mfano kama zile *quick* (baiskeli za mota) zinapatikana kwa bei kubwa, lakini pia mtu akinunua…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ikupa, sasa unachangia. *(Makofi)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Amenisaidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa.

Mheshimiwa Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote anayosema Mheshimiwa Ikupa, ninaomba Waziri wa Fedha na Mipango wayachukue hayo, ndiyo imekuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninataka kulizungumzia ni kuhusu Kiswahili. Kiswahili ni bidhaa na sasa hivi tunatangaza Kiswahili ni bidhaa na inatumika huko *SADC, East Africa* na *AU* kote huko tunatumia. Sasa hivi kuna idadi ya watu karibu milioni 500 wanatumia Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wakati mwingine nilishangaa hapa walikuja Wabunge wanaomba Ubunge *East Africa*, badala ya kukitangaza Kiswahili sasa ninarudi ninaona tuliwapa *interview* kwa Kiingereza. Sasa ninasema hivi tunafanya nini? Huko ukienda kwenye haya Mabunge yote unakuta mtu Kiingereza chenyewe hajui, lakini wanaongea hivyo hivyo, wanachotafuta kule ni utaalam. Sasa sisi tujiandae, hivi ni lazima tuwapatie *interview* ya Kiingereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninataka niombe tafiti iendelee ndani ya kuona kwamba hicho Kiswahili tumekwenda nacho kiasi gani, ili tutoe elimu kwa wahadhiri wapate umahiri kamili wa kuweza kufundisha hicho Kiswahili hasa eneo la ukalimani. Hilo eneo linaonekana bado hatuna wataalam wa kutoa ukalimani pia maarifa ndani ya Kiswahili chenyewe ili iwe bidhaa kama ambavyo sasa hivi tunataka Kiswahili hicho kiwe bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ntara. Mheshimiwa Balozi Mulamula, wajiandae Mheshimiwa Kunambi na Mheshimiwa Ezra.

Washa *mic* yako.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *oh,* samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili nichangie kwenye Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, hoja mbili zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa wasilisho lao nzuri sana ambayo imetupatia faraja kubwa kutokana na taarifa kwamba uchumi wetu umeendelea kuimarika na kuhimili vyema changamoto za dunia zilizojitokeza hivi karibuni. Hii inatupatia matumaini kwamba huko tunapokwenda katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi, tunapata matumaini makubwa. Ninapenda kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uamuzi wake wa kuunda Wizara na Tume ya Mipango. Hakika inafurahisha kuona kwamba mpango na bajeti vinasomana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na timu yake kwa kutushirikisha kama Wabunge kwenye semina maalum ya kuweza kuchangia na kutoa mchango wetu katika maandalizi ya Dira ya Mpango wa Maendeleo Mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuipongeza Kamati ya Bajeti ambayo imedadavua vizuri Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti na ambayo wamewasilisha mapendekezo yao mazuri nitakuja kurudia huko baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri wa Mipango kabla sijaendelea arejee kwenye ukurasa wa 17 mwishoni na 18. Kwenye vishkwambi vyetu inasomeka ukurasa wa 17 kwenye *paragraph* ya mwisho na 18 mwishoni wa mapendekezo ya maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025. Sijui kama *document* yake inasoma kurasa hizo, lakini kitu ambacho ninataka tu ku-*bring* kwenye *attention* ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba, takwimu zilizotolewa kuhusu hali ya umaskini nchini ni za nyuma sana. Hapa zinatajwa ni za mwaka 2011/2012, 2017/2018 ambapo katika hiyo taarifa mnasema kwamba, hali ya umasikini inakadiriwa kupungua kwa 25.7% kwa mwaka huu 2020 na kwamba umasikini wa chakula unakadiriwa kupungua hadi 7.3% mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa ninauliza kwamba, kwa leo tunavyoangalia mpango huu wa 2025/2026 takwimu hizo

zinaonekana ni za nyuma na pengine zilinyofolewa kutoka kwenye maandalizi ya mpango wa malengo kipindi cha tatu cha mpango wa miaka mitano. (2021/2022 – 2025/2026). Ninaomba waangalie tu hiyo labda kuweza kusahihisha hizo takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilifarijika kusikia kwenye taarifa ya habari kulikuwa na tukio ambalo Naibu Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo alizindua rasmi ripoti au chapisho la takwimu kuhusu kipato cha mtu mmoja mmoja na fursa za uchumi na uwekezaji kwenye Mkoa wa Dodoma. Ninawapongeza kwa tukio hilo, lakini kama Naibu Waziri alivyosema ni vizuri na mikoa mingine iige mfano wa Dodoma kuchapisha ripoti hizo ambazo zitatoa uhalisia wa kila mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba kwa Mkoa wa Kagera kuna Taasisi Isiyo ya Kiserikali, ni *think tank* inayojulikana kama *Kagera Development Foundation (KADEFO)*. Imeundwa na wataalam wabobezi wa masuala ya uchumi, ustawi wa jamii na inajumuisha pia wana-*diaspora*. Pia, inashirikiana kwa karibu na Mamlaka za Mkoa na Wizara ya Mipango kutoa chapisho kama hilo. Inaweza kufanya hivyo na mimi ni mdau na mshiriki kwenye taasisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Ujenzi ni mmoja wa walezi wa taasisi hiyo. Ninapenda pia nimpongeze Mheshimiwa Hajat Fatma Mwasa, Mkuu wa Mkoa wa Kagera ameanzisha *initiative* ya *Ijuk'omuka* maana yake kumbuka nyumbani. Katika tukio hilo amekuwa anahamasisha uwekezaji. Kitu ninachoomba ni kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Bajeti kwamba ni vyema Serikali itenge bajeti kwa ajili ya kufanya utafiti wa mapato na matumizi kwa kila kaya ili kupata takwimu ya hali halisi ya umaskini nchini na maendeleo ya watu kwa kutumia taasisi kama hiyo niliyoisema ya *KADEFO*. Kwa hiyo, ninaunga hilo pendekezo la Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka pia Mzee wangu Marehemu Mwalimu Nobert Rutageruka alikuwa kila mara

akinisikia ninaongea ni kwenye majukwaa au warsha alikuwa ananiambia, "Liberata ninasikia unatoa takwimu, unazipata wapi mbona hamtuulizi?" Kwa hiyo, ninadhani tukifanya hizo tafiti zitaweza kujumlisha wananchi kwa upana na wigo mpana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba niongelee kuhusu vipaumbele vya bajeti ambavyo ni vya mpango mzima, ambapo pamoja na mambo mengine ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara na uwekezaji na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu maeneo haya yakisimamiwa vizuri yanaweza kuwatoa Watanzania wengi kwenye wimbi la umaskini na kutuvusha kama Taifa kuelekea kwenye maendeleo makubwa na endelevu. Swali ni nini kifanyike? Kumekuwa na maelezo mengi kwenye hayo mapendekezo lakini tunasema *we need to put money where our mouth is.* Utaona kwamba mchango wa viwanda ni mdogo sana wakati tumesema ni Tanzania ya viwanda. Kwa hiyo, nimekuwa ninaiongelea sana. Ninaomba hili liangaliwe na hasa ukiangalia mikoa ambayo ina rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama Kagera kuna Kagera Kabanga *Nickel*. Ikipewa kipaumbele na msukumo wa uwekezaji katika hili viwanda vya kuchenjua madini haya, kwa kweli itatuvusha sana Mkoa wa Kagera na inaweza ikawa kitovu cha uchumi wa nishati na viwanda vya madini ya nishati. Ninajua *of course* kuna Liganga na Mchuchuma imeongelewa sana lakini ninaomba niongelee madini ya *Nickel* ya Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaomba nigusie kidogo Diplomasia ya Uchumi ambayo ninashukuru sana kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais kama mwanadiplomasia namba moja ametufungulia fursa nyingi na watendaji wakuu ni Ofisi zetu za Ubalozi. Kama Kamati ilivyosema kwamba, Ofisi za Ubalozi hazipewi fedha za kutosha kuweza kufanya na kutekeleza Diplomasia ya Uchumi na hatutumii vizuri fursa ya kusafirisha Walimu na wataalamu wa Kiswahili nje ya nchi. Ninaomba nimpongeze hapa kwa dhati sana Balozi wetu wa Cuba

Mheshimiwa Polepole, kwa kuandaa Tamasha kubwa la Kiswahili Mjini Havana Cuba, ambalo litafunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye yupo kwenye ziara katika nchi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba mfuatilie tarehe 8 Novemba pia atazindua Kamusi ya Kiswahili na Kihispania siku hiyo. Kwa hiyo, huu ni mfano wa kuigwa, lakini vema Balozi zetu ziwezeshwe, ziweze kufanya haya ambayo kwa kweli ndio yanasukuma Diplomasia yetu ya Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme katika mpango wa bajeti uliopita Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema; "kusudi tuwe na matokeo chanya, inabidi tuwe na mfumo thabiti na endelevu wa ufuatiliaji na tathmini *(monitoring and evaluation)* na utolewaji wa taarifa." Pamoja na kutambua azma ya Waziri wa Fedha kuviongezea nguvu vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ninakumbuka huko nyuma Kamati ya Bajeti ilishauri kuwepo sera malum na sheria ambazo zimebainisha kwamba msingi wa….

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Balozi Mulamula.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kurudia hiyo na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, wajiandae Mheshimiwa *Engineer* Ezra na Mheshimiwa Kuchauka. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nianze na utangulizi. Katika utangulizi wangu nitaanza na shukrani. Ninaomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo mawili. Jambo la kwanza; alipokuwa amefanya ziara Wilaya ya Kilombero kwa maana pia na Jimbo la Mlimba kwa sababu lipo ndani ya Wilaya ya Kilombero, tulipewa fursa Wabunge kuzungumza changamoto za wananchi. Pamoja na mambo ambayo nilizungumza kwa niaba ya wananchi wa Mlimba, nilimwomba Mheshimiwa Rais atusaidie kupitia Wizara ya Kilimo, *NFRA* waanze kununua mpunga jimboni kwangu Mlimba. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais mpaka sasa

wananchi wanapata huduma hiyo. *NFRA* inanunua mpunga jimboni kwangu na wananchi wamekuwa wakinufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wananchi wa Mlimba wamenipatia salamu niwashukuru sana Mheshimiwa Rais, Waziri wa Kilimo na Mtendaji Mkuu wa *NFRA* katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninamshukuru Mheshimiwa Rais. Bunge lililopita wakati wa bajeti nilieleza kwa habari ya fedha za mradi wa shilingi bilioni 345. Mimi na wananchi wa Mlimba, kwa kuwa sisi ni wazalendo kweli kweli kwenye nchi hii tulipinga zile fedha shilingi bilioni 345 ambazo zilikuwa zipo chini ya Wizara ya Ardhi na kupinga kwangu kumeleta matokeo chanya na hapa ninampongeza Mheshimiwa Rais; amechukua hatua, amebadilisha matumizi ya fedha zile. Ninamshukuru Waziri wa Fedha kwa kubadilisha zile fedha shilingi bilioni 345 ambazo zilikuwa zinakwenda kuliwa na wajanja wachache. Ninamwomba, kwa kuwa zile fedha zimerudi Wizara ya Fedha, ni muhimu sasa zikawekezwa kwenye sekta muhimu hasa barabara. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais, sasa ninaanza kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza mchango wangu kwa Sekta ya Kilimo na hapa ninaomba nirejee Azimio la Iringa, mwaka 1972. Baada ya Azimio la Arusha kuboresha Azimio la Arusha mwaka 1972, mwaka 1971 tulikuwa na Azimio la *TANU*, ambalo lenyewe lilikuwa linasema, "Uhuru wetu siyo Uhuru wa Bendera. Hata Wimbo wa Taifa siyo uhuru wa kweli, bali mali zote tuzimiliki sisi Watanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Mwaka 1972 pale Iringa, lilikuwa ni mahususi kwa ajili ya kilimo. Lenyewe lilikuwa linasema "Siasa ni Kilimo", sasa ninazungumzia Sekta muhimu ya Kilimo. Ni kweli Taifa letu Mungu ametujaalia rasilimali nyingi kama Taifa, lakini kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, kwenye mipango ya Serikali wawekeze kwenye kilimo, kwa nini kwenye kilimo, kwa sababu Watanzania walio wengi wanajishughulisha na kilimo. Tunaambiwa hapa takwimu, 75% ya Watanzania

wanafanya kilimo. Kwa hiyo, tukiwekeza kwenye kilimo maana yake mapato yataongezeka, lakini pia tutauza nje ya nchi mazao yanayotokana na kilimo na tukapata fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe takwimu kidogo kwenye Sekta hii ya Kilimo, mwaka 2020/2021, Wizara ya Kilimo iliweza kusimamia mauzo ya nje Dola za Kimarekani *(USD)* bilioni 2.3. Zilikuwa zimetokana na mauzo ya nje kutokana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze matarajio ya Sekta ya Kilimo na hii ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango unisaidie na unisikilize vizuri eneo hili. Wenzetu wa Kilimo wamekutangulia; Kilimo wamekuja na mpango wa *vision 2030*. Wao wanasema, wanataka ifikapo mwaka 2030 mauzo yatokanayo na kilimo yawe Dola za Kimarekani bilioni tano. Sasa wewe unapaswa kuwawezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unawawezeshaji? Ni kuchukua mpango wao kuuleta kwako na kuuchakata na kuuboresha zaidi ili Wizara ya Kilimo ifikie malengo yake, lakini pia na *financing*, ukitaka kupata fedha weka hela. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumeona hapa mashahidi, sisi wote Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, Bajeti ya Kilimo imekuwa ikikua mwaka hadi mwaka. Mwaka wa fedha 2023/2024, tunaona Bajeti ya Kilimo ilikuwa kama shilingi bilioni 900, sasa wamekuja na shilingi trilioni moja *point something*. Kwa kweli ninaona Mheshimiwa Rais ana utashi wa kisiasa katika kuiwezesha Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, tumsaidie Mheshimiwa Rais kuiwezesha Sekta ya Kilimo ili ifanye vizuri na sisi Watanzania tunufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze hapa, nchi yetu ina ardhi, tumejaaliwa ardhi kubwa sana nchi yetu, takribani kilometa za mraba 950,000, Tanzania, lakini eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta milioni 44. Sasa, kwenye umwagiliaji sidhani kama tumefikia hata nusu. Sasa, tukiwekeza kwenye kilimo nina imani kubwa tutatoka kwenye umaskini tulionao na kwenda juu zaidi, kwa sababu kilimo na niwaambie kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo na nitoe mfano, kwa mfano zao la mchele; mchele duniani, idadi ya watu takribani shilingi

bilioni 3.5 wanakula mchele. Nchi za Asia wanakula mchele, Nchi ya India wanakula mchele na Afrika. Ninawaambia mchele ndiyo chakula pendwa duniani ukiacha ngano. Sasa, tukiwekeza kwenye mazao ya chakula tunaweza kuuza nje ya nchi na tukapata urari ulio chanya kwa Taifa letu. Kwa hiyo, ninaeleza haya ili tuisaidie Sekta ya Kilimo kwenye mipango yake ifanye vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Waziri wa Kilimo na ninamwambia kwa dhati; kama kuna jambo ambalo Mheshimiwa Waziri unakwenda kuweka alama kwa Taifa letu, ni Mradi wako wa Umwagiliaji wa Bonde la Mto Kilombero. Ninaomba uusimamie vizuri, yaache yote, tumechelewa sana watu wa Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa dhati, Mkoa wa Morogoro ndiyo mkoa ambao tuseme una miti ya kutosha. Hatufanani na wengine huko, sitaki kutaja. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, acha yote tazama Morogoro. Huu wakati wa Mama Samia, huu wakati wa Mkoa wa Morogoro kupanda kwenye Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema haya; tumeambiwa hapa takribani hekta 44,000 zinasanifiwa kwenye Bonde la Mto Kilombero na katika hekta hizo, karibu hekta 30,000 zinatoka Mlimba. Kwa hiyo, ninasema tu kwa dhati wananchi wa Mlimba wanasema Mheshimiwa Waziri wekeza hela pale. Umesema unafanya upembuzi yakinifu; ukianza mapema na sisi tutafurahi. Kwa sababu nikwambie kwa dhati, sisi Mlimba tunazalisha mchele tani laki sita, nchi nzima mnazalisha mchele tani laki tano, hivi hamwoni? Kwa jembe la mkono na kilimo cha mvua, sasa wakituwezesha mambo si yanakuwa vizuri zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee na eneo lingine, ninaenda kwenye Sekta ya Ardhi; Sekta ya Ardhi! Kama kuna jambo ambalo lazima tufanye mapinduzi kama nchi, nina mapinduzi ya fikra. Tusitazame ardhi kama migogoro, shida tuliyonayo tunaitazama ardhi kama migogoro. Kwa hiyo, hata watu wanaohusika na sekta ya ardhi ni migogoro, kazi ya ardhi

siyo migogoro, hasa wizara, Wizara ya Kisekta ilikuja na sheria muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mpaka sasa ninavyozungumza, kama Taifa hatuna *National Land Use Masterplan*. Sasa, kazi ya Wizara ya Ardhi ni kuja na *Nation Land Use Masterplan*, ambayo kimsingi niwaambie, *population growth rate* ya nchi ni asilimia tatu. Tukiendelea na matumizi mabaya tuliyonayo sasa ya ardhi, miaka 10 ijayo, miaka 20 ijayo, watu watapigana mapanga kugombania ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Wizara ya Ardhi na Wizara ya Fedha wawasaidie kuwa-*finance*. Waje na mpango kabambe wa matumizi bora ya ardhi wa Kitaifa, ambao wenyewe utaelekeza kwenye halmashauri waje na mipango miwili; *Masterplan* ya *Land Use* na *Masterplan* ya *Infrastructure*. Ninasema tu haya, yanawezekana, haitakiwi *rocket science* hapa; ni utayari na *commitment* tu, wala siyo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, najielekeza kwenye Sekta ya Miundombinu, ninamshukuru Waziri wa Ujenzi, katika mipango yetu lazima tuwe na mipango ya kati, mipango ya muda mrefu na mipango ya muda mfupi. *TANROADS* ilianzishwa mahususi kwa kuhudumia barabara za Kitaifa na barabara za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nilidhani mpango wa Wizara ya Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa nisikilize kidogo. Haya madini ninayotoa hapa ni muhimu sana, Wizara ya Ujenzi, ninaomba kidogo mkamilishe kwanza ujenzi wa *trunk roads*, kwa sababu watu wanashughulika na barabara za wilaya wakati nchi yetu bado mikoa haijaungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vipaumbele vingeanza kuunganisha mikoa, ukilinganisha mkoa na mkoa au kanda na kanda, kwa mfano, Barabara ya Morogoro – Mlimba – *Njombe Border* ni barabara muhimu kwa uchumi wetu. Ni barabara inayounganisha Mikoa ya Pwani na Nyanda za Juu Kusini. Haiingii akilini Watanzania mpaka leo *trunk road* haijajengwa, *trunk*, Barabara ya Kitaifa. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa mzungumzaji, anachozungumza ni sahihi kabisa, bado Mkoa wa Lindi na Mtwara haujaunganishwa kwa barabara ya lami.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea, ninaomba niseme haya, nihitimishe kwa sababu kengele imegonga. Ahsante, ninataka kusema nini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiijenga Barabara inayotoka Pwani – Morogoro – Mlimba – Njombe, barabara hii itainua uchumi wa Taifa letu, kwa sababu ni barabara ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho mkasome Zaburi ya 90:10.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, Mungu atubariki sote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka, ajiandae Mheshimiwa Kishimba.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye maoni haya ya Mpango wetu wa 2024/2025. Kipekee kabisa ninawapongeza Mawaziri wote wawili na timu zao kwa mapendekezo haya ambayo wameyaleta, lakini kwa sababu tunatoa maoni,

nitaenda moja kwa moja kwenye mambo hasa mawili makubwa ambayo yanabeba suala ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, ninapenda kuongelea Mradi wa *LNG* kama mradi mkubwa wa kunyanyua Taifa, lakini pia nitaongelea mradi wetu ambao nimekuwa ninauongelea siku zote wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bajeti ya mwaka 2022/2023 wakati Wizara ya Nishati inawasilisha hapa, tuliongelea habari ya *LNG*. Kwa hiyo, ninapenda tu niweke mkazo hapa kwamba, miradi hii mikubwa ambayo inaleta sura ya Kitaifa na hasa ambayo inashindana na Mataifa mengine makubwa inapokuwa inataka kutekelezwa katika Taifa, si kusema wale wanaofanya miradi hii huwa wanafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miradi ambayo tuliaminishwa na tuliona kwamba inaweza ikatusaidia kama Taifa hasa kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme, matumizi ya magari, ambapo tuta-*compress* hiyo gesi na kuwa *compressed natural gas (NG)* kwa ajili ya matumizi ya magari, lakini pia na kuuza gesi hii nje baada ya kui-*compress* tukaipakia katika meli zile kubwa na kwenda kuiuza huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tunaomba; tutakapokuwa tunapanga mpango huu, Wizara hizi mbili hasa Wizara ya Mipango, mje na *a thorough analysis*, ikiwezekana tupate *take-off* ya hili jambo. Kwa sababu wenzetu wanachofanya, kuna *players* kama watatu wanne watano ambao wao wanamiliki miradi hii mikubwa ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tunapozidi kuchelewa, uwezekano wa wao kuamua kufanya sehemu nyingine ni mkubwa na sisi tukabaki na hii gesi isitusaidie. Maana dunia inabadilika kila siku na visa vinakuwa vingi na hasa *deals* hizi kubwa zinapotokea, kila mmoja anaangalia *advantage* yake ambayo inamsaidia yeye kwenye kupata pesa, lakini pia kwenye kuzuia watu wengine wasinyanyuke. Kwa hiyo, ninaomba tulione na tuweze kulifanyia kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi pia kuongelea maendeleo ya Taifa kama hutakuwa na *stable power supply*, hasa umeme. Maana wote mnajua tunatekeleza miradi mikubwa ya Kitaifa na unapoongelea kukua, hasa ukawa na *industrial packs* kubwa, lazima uwe na *stability* ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua tunaingiza *megawatts* 2,115 kwenye Gridi ya Taifa kutoka kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini kwa mipango ambayo tunayo kama Taifa, nami bado ninaona huo umeme ni mdogo na hautoshi. Unajua leo umeme kwenye vijiji umefika maeneo mengi, ni zile *centres* tu za vijiji. Ukisema uusambaze uanze kuingia vijijini, huu umeme bado ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nina-*insist*, kama Taifa lazima tujaribu kuangalia vyanzo vingine vipya vya umeme. Kwa sababu Taifa linalokuwa katika ushindani mkubwa namna hii, hatuwezi kuwa katika *position* hii ya umeme, bado tukajivunia. Fikiria tangu uhuru tulikuwa hatujafika *megawatts* 2,000; leo ndiyo tunaenda kuingiza hizi tunafika 4,000 na kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado umeme huu ni mdogo, kwa hiyo, tuangalie jinsi ya kuzalisha umeme hasa kutoka kwenye *Project* ya Liganga na Mchuchuma, kutoka kwenye *Project* ya *LNG*, ziweze kutusaidia kuingiza umeme mwingi kwenye Gridi ya Taifa, hatimaye hao wawekezaji ambao tunasema tunawavutia waje kuwekeza hapa, waje wakiwa na uhakika wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninayasema haya; wiki kama tatu zilizopita nilikuwa Uganda na bahati nzuri nikatembelea ile *project* yetu ya Bomba la Mafuta. Kwa kweli ukijaribu kuangalia *presentations* zilizokuwa zinafanyika pale, nami kama Mtanzania nilijisikia vibaya. Maana lile bomba linalotoka Hoima kuja Tanga, kiasili yale mafuta kwa sababu ni *crude oils* lazima yaendelee kubaki katika *temperature* fulani kwa ajili ya kuyasafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaangalia kwa upande wa Uganda *pump stations* mbili zinazojengwa Uganda, wao

hawajaweka hata *issue* ya *solar*. Maana wanasema umeme uko *stable*, watatumia umeme wa maji *(hydropower)* kutoka Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *pump stations* nne zinazojengwa Tanzania, iko *package* ya ku-*include solar energy*. Kwamba, kila *pump station* ya Tanzania wameweka *solar* na jamaa yule kipindi ana-*present* pale hakujua mimi ni Mtanzania. Kweli aka-*insist* kabisa, *you know in Tanzania electricity is not stable, so, we have to include solar package here*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mtanzania iliniumiza, nikawaza nikasema; hawa jamaa sehemu kubwa ya *pump stations* ziko kwetu, lakini bado hawatuamini. Wame-*include solar package* ili waweze kwenda kufanya ule mradi uweze kuwa *stable*. Sasa, nikaona hili jambo ni lazima kama Taifa tunaposema tunakuwa, tunasonga mbele, hata kama tunaingiza kwenye *Nation Grid* leo hii umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, ni lazima tuangalie vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nina-*insist* kwenye suala la Liganga na Mchuchuma, huu mradi ndiyo mradi wa kipekee ambao unaweza ukatunyanyua kama Taifa. Maana Uganda leo wana mafuta; wako mpaka kwenye *Project* ya kujenga *refinery* ndani ya nchi yao ile, kwamba mpaka watapata *byproducts* nyingine zinazotoka kwenye mafuta, ambazo zitakuwa zinatangaza Taifa lao kama *byproducts* za kutengenezea *chemicals*, *byproducts* za kutengenezea mabomba ya plastiki na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tuombe hata sisi, huu Mradi wa Chuma, Serikali imelipa fidia, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa zaidi ya shilingi bilioni 15 ambazo ameweka pale. Sasa, kwa sababu ya *owning this project*, tunaomba tuone kwenye Mpango huu wa mwaka 2025/2026, ni nini kinafanyika kwa ajili ya *take-off* ya mradi huu. Hatuna kitu kingine cha kujivunia kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amesema habari ya *Southern Corridor* kwa ajili ya *SGR*. Sasa, kama huu mradi hauja-*take-off*, hiyo pesa tunayoenda kuwekeza huko chini itafanya nini? Ni

lazima tuhakikishe huu mradi una-*take-off*, ili hatimaye kilio hiki cha Watanzania cha kuona tunasonga mbele tuweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dola bilioni tatu ambazo zinasadikiwa kama uwekezaji, *deposit* tuliyonayo, nilikuwa naangalia hapa napitia, *deposit* tuliyonayo kwenye *iron ore* peke yake, ni zaidi ya tani milioni 126, *deposit* tuliyonayo kwenye makaa ya mawe ni zaidi ya tani milioni 428.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *price* ya leo kwenye *iron ore*, tani moja ni dola 118, ukiangalia kwenye makaa ya mawe, tani moja ni dola 141. Hii yenyewe uki-*calculate* tu ni zaidi ya dola bilioni 74, yaani unawekeza dola bilioni tatu, *deposit* uliyonayo itakuingizia zaidi ya dola bilioni 74. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, *sometimes* unakaa unaangalia, ni nini, yaani tunakwama wapi? *The think tankers of this country* wanakwama wapi kutupeleka huku? Yaani kwa nini nishindwe kuweka dola bilioni tatu nika-*recoup* zaidi ya dola bilioni 74? Bado tunasema tunahangaika na vitu vingine, wakati huu mradi uko hapo muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye andiko, majadiliano yanaendelea na mtu yule yule aliyetukwamisha kwa muda mrefu. Inafikia *stage* kwenye mawazo yangu ninawaza hii ni hujuma, ni hujuma kwa sababu, tunapoelekea makaa ya mawe yanakuwa *phased out* na tutaanza kutumia nishati safi kama mnavyoelewa. Hata haya makaa ya mawe nilikuwa ninaongea na Mchina mmoja, anasema hawawezi kuingiza makaa ya mawe kwao yakiwa na *state* ya vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote anayetaka kuingiza makaa ya mawe China, wana mtambo wametengeneza wa kuyasafisha kwanza kabla ya kuya-*export* kwenda *China*. Kwa sababu wanaamini yanasababisha kansa, wanaamini yanaleta *mercury* na vitu vingine kama hivyo. Sasa, kipindi tunapambana na dunia, makaa ya mawe tumepata bei nzuri sana kwa sababu ya vita ya *Russia* na *Ukraine*. *Energy supply* kwa sehemu kubwa ya

dunia ilisimama. Tunavyozidi kuchelewesha huu mradi tutakwama na haya makaa ya mawe tutabaki nayo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba, kwa kumalizia ninajua kengele imegonga. Waziri wa Mipango uko hapa, lichukue hili mlifanyie kazi. Bahati nzuri umekuwa Waziri wa Viwanda na unalijua vizuri. Kwa hiyo, ninaamini kwenye mpango wako wa mwaka 2025/2026, tuone *clear statement* ya Serikali ya kwenye mpango huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante!

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Fursa ya kuandika unayo, mwandikie Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Kishimba jiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Awali ya yote ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono makubwa ya kuja na Wizara ya Mipango. Ni wazi kwamba bajeti hii inayokwenda mwaka 2025/2026 itakuja na sura nyingine kabisa, sura ambayo inaonyesha kwamba kweli kuna Wizara ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaanza na utoshelevu wa umeme nchini; ni kweli na hapa ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha tunamaliza ule mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ndiyo maana sasa tunasema tuna utoshelevu wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utoshelevu wa umeme nina mambo mawili ya kushauri; kwanza tunaposema umeme unatutosheleza inatia mashaka kidogo, wakati iko mikoa kwenye

nchi hii bado haijaungwa kwenye Gridi ya Taifa. Sasa, tunaposema una utoshelevu mkubwa wa umeme, mfano mzuri, nitoe mfano kwenye Mkoa wetu wa Lindi, hasa Wilaya ya Liwale, tunachangia Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa 26%, lakini bado hatujanufaika na umeme wa Gridi ya Taifa. Kwa hiyo, ni matumaini yangu, wakati tunakwenda kujitosheleza kiumeme, basi nione mipango ya bajeti inayokuja kuhakikisha mikoa ile ambayo haijaingizwa kwenye Gridi ya Taifa inaingia kwenye Gridi ya Taifa ili tuweze kufaidi keki hii wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine, niende kwa walipakodi; je, *population* yetu ya Kitanzania inalingana na idadi ya walipakodi tulionao? Hapa ninaomba niwashauri Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba kila mwaka tunakuja na takwimu, ambazo zinaonyesha kwamba mwaka jana tulikuwa na walipakodi kiasi gani na mwaka huu tuna walipakodi kiasi gani *vis-a-vis* ongezeko la idadi ya watu hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zipo nchi zina *population* ndogo, lakini zina walipakodi wengi kuliko sisi ambao tuna *population* ya watu milioni 60, lakini tuna walipakodi wachache. Kwa hiyo, hapa ninaomba nilishauri Serikali niishauri Wizara, ihakikishe kila mwaka inazalisha walipakodi wapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itapunguza hii kimbizakimbiza ya walipakodi wachache, kwa sababu hawa walipakodi wachache tunawakamua sana ili tuweze kukidhi bajeti zetu, lakini Serikali ichukue jambo hili kwamba, kila mwaka ihakikishe inaongeza idadi ya walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine, ni kweli bajeti ya kilimo imeongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Hapa ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa maono makubwa ya kuipandisha Wizara hii ya Kilimo kuwa na bajeti kubwa kiasi hiki na matokeo yameanza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba baada ya Wizara ya Kilimo kupandishiwa bajeti tayari tuna ziada ya

chakula. Mfano, sisi kule Mikoa ya Lindi na Mtwara uzalishaji wa korosho umepanda sana. Hapa ushauri wangu tunaunganishaje kupanda huku kwa kilimo na miundombinu ya barabara, tunazalisha sana, wakulima wetu wanazalisha sana. Tunahitaji sasa mazao haya yafike kwenye masoko, mazao yanatakiwa yaende viwandani, mazao yanatakiwa yafike kwenye masoko lakini je, tumejiandaa vipi na ujenzi wa barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikosei huu ni mwaka wa tatu, mimi kwa mtazamo wangu sijaona mradi mkubwa wa barabara kwenye nchi yetu ambao umekamilika ndani ya hii miaka miwili mitatu. Kwa hiyo, ninaomba kwenye bajeti hii inayokuja...

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** ... tuone kwamba bajeti yetu hii inakuja na mpango wa ujenzi wa barabara, barabara ambazo tutakwenda kuunganisha na wakulima ili mazao yao yafike kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri Mkoa wa Lindi na Mtwara...

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** ... ni wazalishaji wakubwa sana wa mazao ya korosho na mazao ya ufuta...

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba Barabara ya Kidatu - Ifakara imekamilika na anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni jambo la muhimu sana kwamba kukamilika kwa mradi wa Barabara ya Ifakara - Kidatu ndiyo kunaunganisha barabara yake moja ya kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Lindi, Mkoa wa Morogoro Malinyi kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** ...na kwenda Njombe, kwa hiyo nataka nimsisitize ataje hizo barabara kwa sababu zinaenda kwake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga ahsante. Mheshimiwa Kuchauka, endelea. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninaipokea Taarifa yake. Nilichokuwa nazungumza kwamba ufungamanishaji wa kilimo cha kisasa na miundombinu ya barabara. Nikatoa mfano Mkoa wa Lindi pamoja na uzalishaji mkubwa wa korosho na ufuta, lakini ndiyo mkoa pekee ambao hauna mradi mkubwa wa barabara. Mkoa wetu wote hausomani kutoka wilaya moja kwenda wilaya nyingine, kutoka Mkoa wa Lindi kwenda mkoa mwingine bado barabara zetu hazisomani. Kwa hiyo, utaona kwamba kuongeza kwa bajeti ya Wizara ya Kilimo hatutaiona ile tija ya kuongezeka kwa bajeti kwa sababu ya shida iliyopo kwenye barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nitoe ushauri wangu kwenye ujenzi wa vituo vya afya, shule na kadhalika. Hapa vilevile niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa namna alivyotekeleza miradi hii kwa upande wa elimu na upande wa afya. Ninaomba nione kwenye mpango huu namna ya kupata watumishi na hapa niseme tu kwamba, kwa upande wa vifaatiba navyo vinafanya vizuri lakini bado tuna tatizo kubwa la ajira. Utakuta kituo cha afya kina ikama zaidi ya watu 25 kinahudumiwa na watu watatu. Kwa hiyo na hapa ninaomba

kwenye bajeti hii inayokuja tuone namna ya kuongeza idadi ya watumishi iendane sawasawa na uwekezaji uliowekezwa kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwenye Sekta ya Bandari, ni ukweli usiopingika Bandari yetu ya Dar es Salaam uwekezaji ni mkubwa na tumeshaanza kuona manufaa ya uwekezaji ule, ninaomba sana tuone na bandari nyingine ili Bandari ya Dar es Salaam iweze kupata msaada. Kuna Bandari ya Mtwara, kuna Bandari ya Maziwa Makuu na hapa ninaomba nisikitike sana kwenye Bandari yetu ya Mkoa wa Lindi, Bandari ya Lindi ndiyo imesahaulika kabisa; lakini kwa namna ya uzalishaji mkubwa uliopo Lindi, nilitegemea nione sasa twende na Bandari ya Lindi nayo ionekane kwenye bajeti hii na siyo tu kuonekana kwenye bajeti, ionekane ikipewa kipaumbele na iweze kutekelezwa kwenye Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kishimba, wajiandae Mheshimiwa Gulamali, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaungana na Wabunge wenzangu kuchangia Mpango wetu huu wa mwaka 2025/2026. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais, Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango na timu zao nzima kwa Mpango mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanzia kwangu Kahama, Kahama wamenipatia barabara kweli kabisa za Benki ya Dunia na barabara hizi mkandarasi ameshazitifua na mvua zinaendelea kunyesha, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ajitahidi kumlipa mkandarasi huyu maana yake hana pesa na ni za Benki ya Dunia. Kama itaendelea hivyo ina maana tunaweza kupata maafa kwa ajili ya mafuriko kwenye maeneo ya watu ambako ametibua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo Kamati ya Elimu ya Juu, juzi hapa Bodi ya Mikopo walileta hoja kwamba hawapati marejesho kutoka kwa watu waliokopa au waliokopa elimu na wanajiandaa kuanza kufanya *operation* ya zoezi la kuwakamata wadaiwa wote wanaodaiwa. Sasa hoja yangu, Bodi ya Elimu ilimpa mtu wa chuo hizo pesa, mtu wa chuo akampa elimu mwanafunzi, elimu ambayo haiajiriki. Sasa anayetakiwa kushtakiwa kabisa ni nani, ni mwanafunzi au ni chuo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haya maneno dunia inabadilika hatuwezi kuendelea na lugha ile ile ya kusema elimu ni ufunguo wa maisha, Hapana. Elimu ni bidhaa, hawa watu walichopewa ni bidhaa wameshindwa kuuza, kwa hiyo mwenye kosa ni Bodi ya Mikopo. Ndiyo maana hoja yangu kwenye Kamati yetu na Mheshimiwa Waziri alikuwepo, kwa nini tusiweke masharti kwamba chuo chochote ambacho kinataka kuingia kwenye eneo la kupewa mikopo ki-*qualify* kwamba mwaka jana walimaliza wanafunzi 300 na katika hao 70% wamepata ajira ndiyo kihusike na kupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Profesa Muhongo, alivyosema hapa kwamba kweli watu wanahitajika kule, lakini kama Bodi ya Mkopo inazitupa tu hela kwa mtu halafu anaenda kumfundisha *GPA* isiyoajirika ni sahihi si itafilisika kweli. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango, liweke suala hilo kwenye mipango yako ili hawa watu wa chuo ndio wakatafute mitaala ambayo itafanya watu waajiriwe na zile pesa zirudi kuliko utaratibu wa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi sisi Shinyanga na Kahama tulipata ugeni wa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, miongoni mwa suala ambalo tuli-*raise* pale ni suala la afya. Ninajua siongelei habari ya hela lakini hospitali wananchi wamejenga wao wenyewe, kumwona daktari kwenye hospitali ya hela unatakiwa utoe shilingi 5,000, sasa mwananchi wa kawaida Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha, hii hospitali ni ya Serikali, daktari analipwa na Serikali sababu ya mwananchi kwenda kumwona kwa hela ni nini? Labda Mheshimiwa, ulifikirie kwa makini sana, kwa sababu wananchi

hawa wana hali ngumu sana wote mnafahamu hali ya pesa ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaleta pia *issue* kwamba Serikali kwa nini haitaki kutoa bei elekezi ya dawa na matibabu? Leo hapa tunakabana na Mheshimiwa Bashe kwenye kesi ya sukari, lakini wote humu madaktari wamo, si mnatuambia wenyewe sukari ni sumu. Sasa kwenye sumu bei inapunguzwa ili watu wakanywe sumu si ndiyo, lakini tunakataa kupanga bei ya dawa, inawezekana kweli? Maana yake wote tunalazimisha kwamba sukari lazima iwe na bei ya Serikali, lakini nyinyi wenyewe hapo hapo mnasema sukari ni sumu, sasa sumu ndiyo inapunguzwa bei na inapangiwa bei kweli? Tunakataaje kumpangia mwananchi bei elekezi ya matibabu na dawa, tunang'anganiaje sumu ipewe bei elekezi? Haiwezekani! Tunajaribu sana kuliona hili suala kwa undani zaidi badala ya kuchachamaa na vitu visivyo na maana, bora tuchachamae sehemu ambayo ina uhai wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nitaongelea suala la *Kabanga Nickel*, mimi kwangu Kahama ndipo unapojengwa ule mtambo mkubwa, lakini bado tunavutana. Tumekwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha mara mbili, mara tatu. Mtu anayetaka ku-*inject* hela kwenye ule mgodi ana dola milioni 400, lakini Serikali kwa sheria iliyopo inataka 30%, lakini Serikali hiyohiyo ina hisa ya 18% kwenye ule mgodi na hali ya yale madini ni mbaya sana, kwa sababu Wachina wanatengeneza *nickel* ya bandia. Sasa tumwombe Mheshimiwa Waziri, kama kuna sheria ilete sheria hiyo ibadilishwe ili huyu aweze kuingiza pesa ili mgodi ule uanze. Kwa sababu kule kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, una *megawatt* 600 hazina mnunuzi wa umeme, huyu *Kabanga Nickel* ni mnunuzi mzuri wa umeme, sasa upande mmoja unamkatalia huyu kuweka, upande mmoja unasema huna pa kuuza umeme na huyo ndiyo mnunuzi mzuri wa umeme. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, jaribu kulifikiria sana suala hilo ili kusudi liweze kutusaidia, lakini la muhimu sana lile suala la dawa tusaidie sanasana kutupangia bei elekezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Seif Gulamali, wajiandae Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa mwisho wa mwaka 2025/2026. Ni Mpango wa mwisho baada ya kutoka katika ile Dira ya Maendeleo ya miaka 25, kwa maana 2020/2025, lakini pia nipongeze kwa maandalizi mazuri na namna ambavyo tumeweza kuona Mapendekezo mapya ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya miaka mingine 25 kwa maana ya 2025/2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu wa maendeleo ambao tunakwenda kuumaliza wa mwaka 2024/2025, tumeweza kuona mambo makubwa ambayo yanaendelea kufanyika, lakini ni Mpango wa miaka 25 ambao toka tumeuanza 2020 kufika 2025/2026 mambo makubwa tumeweza kufanikiwa. Tumeweza kuona kuna maendeleo makubwa katika upande wa umeme japo hatujafikia malengo tuliyojiwekea kwa sababu tulitakiwa tukamilishe tuwe na *megawatt* 5,000 mpaka kufikia mwakani. Ninaamini tutazifikia kwa sababu zipo mbinu mbalimbali zinaendelea kuwekezwa kuhakikisha kwamba tunafikia japo mpaka sasa tuna takribani zaidi ya *megawatt* 4,000 za umeme ambazo tumeweza kuzalisha na hasa kukamilika kwa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere lenye *megawatt* 2,115.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kubwa sana kwa Serikali inayoongozwa na Mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia na Mawaziri ambao wapo katika sekta mbalimbali ikiwa pamoja na Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati, hongereni sana kwa kukamilisha ujenzi wa Bwawa hilo na sasa kwenye umeme angalau kuna ahueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia kwa kuendelea kukamilisha miradi mikubwa kama ule Mradi wa *SGR* kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na sasa tunaendelea na ujenzi wa *SGR* kutoka Dodoma kwenda Tabora, tunaona ujenzi ukiendelea kutoka Mwanza kuja Isaka, Isaka - Tabora lakini pia tunaona harakati zingine kutoka Tabora kwenda Kigoma.

Tutakapokamilisha hii *SGR* uchumi wa nchi yetu utapanuka na utakuwa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanyika katika usambazaji wa umeme vijijini, sasa karibia 95% ya vijiji vyetu vyote vimepata umeme imebaki asilimia chache kukamilisha na kwa sababu tunaamini Mpango unaokuja unaenda kukamilisha vitongojini. Niiombe Serikali katika mipango yetu tuhakikishe kwamba wananchi wanahitaji hizi huduma kwa haraka na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia kwa kazi zote zinazofanyika za miradi ya barabara, ninapenda kushauri katika Mpango wetu huu, kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro bado tuna miundombinu ambayo siyo rafiki kwa matumizi ya magari. Niiombe Serikali iharakishe mpango wa kuongeza njia nne kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro, lakini pia njia nne kutoka Morogoro kuja Dodoma, kutoka Dodoma kwenda Tabora kupitia Igunga kwenda mpaka Nzega, mpaka Shinyanga na Mwanza. Ukuaji wa uchumi unaenda sambamba na ukuaji wa miundombinu hasa ya Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza *SGR,* lakini tusisahau kuwekeza kwenye ujenzi wa barabara hasa hii njia kubwa ambayo tunapitisha malori makubwa, lakini pia kama tunavyotambua sisi tumezungukwa na Nchi ya Rwanda, Burundi, Congo, Uganda na Zambia. Kwa hiyo lazima tuangalie hili Soko la Afrika tunawezaje kulishika kwa ukaribu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri katika mipango yako lazima tuwekeze kwenye ujenzi wa miundombinu, lakini pia tuhakikishe kwamba miundombinu hii inakuwa bora na imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuwaomba Wizara ya Fedha, wazabuni wengi wamepewa kazi mbalimbali katika maeneo mbalimbali tunaomba wawalipe fedha zao kwa wakati ili kazi hizi zisiweze kukwama. Tunaona miradi mbalimbali inatekelezwa na ni mikubwa, lakini Wizara ya Fedha na Mipango wahakikishe fedha zinapatikana kwa wakati ili tusichukue muda mrefu katika kutekeleza mradi ambao tumejiwekea kutekeleza kwa miaka mitatu au miaka miwili

tukafanya huo mradi tukautekeleza zaidi ya miaka minne ama sita ni kujirudisha nyuma kimaendeleo. Kwa hiyo niwaombe sana watu wa Wizara ya Fedha wajitahidi katika kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha na tunalipa fedha katika maeneo ambayo tumejiwekea kama sehemu ambayo tunatakiwa kuhakikisha kwamba miradi haikwami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ujenzi kwenye Sekta ya Kilimo, tunaipongeza Serikali kwa kuwa na nia ya dhati kabisa yakuwekeza fedha kwenye kilimo. Bajeti ya Kilimo imetoka shilingi bilioni 200 na sasa tunazungumza trilioni zaidi ya moja na kidogo. Tunapongeza kazi hii nzuri kwa sababu tunaona ujenzi wa mabwawa, tunaona ujenzi wa skimu za umwagiliaji, lakini tunaona namna ambavyo Wizara na Serikali zina nia ya dhati. Niombe tuwekeze zaidi kwenye kilimo, tuongeze fedha, tujenge mabwawa makubwa kwenye maeneo ambayo kuna mvua za kutosha, ambako tunaweza tukajenga mabwawa tukaweza kuyavuna haya maji, lakini pia tukajenga skimu za umwagiliaji tukawa tunalima mara mbili mpaka mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambako ninataka niishauri Wizara ni kwenye upande wa Sekta ya Michezo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Pole, pole kwa jana. Mheshimiwa Waitara, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Mabula na Mheshimiwa Juma Usonge. *(Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Waheshimiwa Mawaziri waliokaa pale, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwenye Mpango wa Serikali na mipango yetu mingi wala hatuhitaji kutumia elimu kubwa sana hapa. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inatakiwa awaambie Watanzania

na Wabunge wenzake kwamba hivi Wizara ya Fedha inakwama wapi kuchukua kodi kwa Watanzania ambao wanapaswa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha ambazo zipo walipakodi wa nchi hii hawafiki 20%, ni fedha ambazo zipo watu wanafanya biashara kiholela, mapato yanapotea ya Serikali, walipeleka zile mashine za *EFD* lakini wakaweka gharama kubwa sana, wangeweza kuzinunua wakawapa wafanyabiashara bure halafu kila fedha isilipwe *cash* ili watu ambao wanapaswa kulipa kodi walipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango katika jambo la kuanza nalo achana na vyanzo vipya, nenda kwa watu ambao wanafanya biashara, wenzetu mbona wameweza na wanafanya maeneo mbalimbali wanaweza kufanya kazi tupate fedha. La pili, kwenye matumizi ya fedha ya Serikali, ili Watanzania walipe kodi vizuri ni lazima wakilipa kodi wawe na uhakika fedha inayolipwa inaenda kufanya kazi za maendeleo kwa wananchi. Kama watakuwa wanalipa kodi halafu wanaona kwenye Ripoti ya *CAG* kila mwaka kuna madudu mengi maana yake watu wanakata tamaa. Kwa hiyo lazima tusimamie watu walipe kodi lakini pia tusimamie fedha zifanye kazi ambayo imekusudiwa kama ambavyo kila Mbunge anasema amepeleka fedha nyingi majimboni na huduma zinapatikana, wasimamie fedha ya Serikali zisipotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya Serikali kuna miradi mingi sasa hivi imekwama, maana yake lazima tushone koti kulingana na ukubwa wa kitambaa, tuwe na miradi michache ya kimkakati lakini mradi ukianzwa umalizike. Hivi kwa mfano leo barabara kama ile ya kutoka Tarime mpaka Mugumu (Serengeti) ambayo ukanda ule wote wa kwangu wanaitegemea, mkandarasi ameenda *site*, ameenda amechimba chimba ameondoka mvua zinanyesha watu wanakwama kutwa nzima, kwa hiyo unakuwa huna maelezo. Kwa hiyo katika mipango yao miradi ile ambayo imekwama ni vizuri wakatenga fedha wakaimalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kulikuwa kuna malalamiko mengi, unatoka pale Ziwa Victoria uende mpaka Rorya, uende mpaka Tarime, wanajenga tenki pale Sirari, mkandarasi amehama kaondoka na vifaa pale *site*. Kwa hiyo, miradi ile viporo, barabara mbalimbali nchi nzima, miradi ya maji, Miradi ya *REA* ya kupeleka umeme kwenye vitongoji, hii ndio mipango ya Serikali ifanyike kumalizia miradi ambayo imekamilika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukienda Musoma. Bandari ya Musoma leo haifanyi kazi, kwa hiyo, ina maana bidhaa inakuja mpaka Mwanza halafu wanapeleka kwa malori mpaka pale Musoma. Bandari ya Musoma ni sehemu ya uchumi, ikikamilika ile wataenda mpaka Kisumu, wataenda mpaka Jinja, kule Kampala, Bukoba na Kanda ya Ziwa yote ikachangamka, tupate huduma pale ni sehemu ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Musoma umesimama, hamjamalizia, tumepata misiba tunatumia gharama kubwa sana. Watu wanaumia migongo, lakini wangeweza kupanda ndege kutoka hapa, Dar es Salaam, wakaenda Musoma na ni sehemu ya Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liganga na Mchuchuma imezungumzwa miaka yote hawahitaji elimu mradi upo, chuma kipo, makaa ya mawe yapo ni Mpango wa Serikali. Iwalazimishe kazi ile iweze kukamilika tupate huduma pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ya kujenga masoko. Hivi kwa mfano, eneo la Sirari kuna eneo lipo *potential* kabisa kwa mazao yote ya Tarime na Rorya. Siku hizi Wakenya wanachukulia mazao mashambani hata yakiwa mabichi ambayo hayajaiva. Ukijenga pale soko la kimataifa maana yake mazao yote ya Kanda ya Ziwa utayauza pale Sirari, watu watachangamkie masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kule Tarakea, nenda Horohoro, Tanga, nenda Tunduma, mkiwekeza maeneo hayo mtapa fedha nyingi sana na uchumi wetu utakuwa na maeneo haya wananchi watapata huduma nzuri zaidi, ndiyo maana

nasema katika mipango ya Serikali wala huhitaji kutumia nguvu kubwa, ni elimu ya kawaida kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninataka nisema ni watumishi wa umma; kweli tumejenga shule, sekondari, lakini walimu kwenye shule hawapo. Katika sekondari zetu mnazungumza habari ya sayansi, kuna watoto wetu wanafanya mitihani ya *form four,* hawajasoma *practical,* wanasoma kwa kuangalia vitu kwa macho, sasa sayansi anaelewa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima mkaweke mpango kwamba, shule zote za sekondari mpeleke vifaa vya maabara, watoto wasome sayansi tupate madaktari, tupate ma-*engineer,* tupate manesi na ni jambo ambalo linawezekana, kama ambavyo tumejenga madarasa. Sasa tuelekeze kuajiri walimu wenye sifa, lakini pia na vifaa ambavyo vitasaidia katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ni, mipango ya Serikali. Ukifuatilia miradi mingi ya Serikali kwanza inabidi utafute fedha ya kupeleka mradi halafu unakwenda kulipa fidia kwa sababu, maeneo hayajapangwa. Mpaka leo tunapanga hapa mipango, lakini kuna ugomvi mkubwa kati ya wakulima na wafugaji, hayajatengwa maeneo ya kulima hatukutenga maeneo ya wafugaji, hatukutenga maeneo ya viwanda na maeneo ya miji. Kwa hiyo, ukipeleka fedha ya mradi fulani ni lazima utenge fedha ya kwenda kulipa fidia na wananchi wetu hawajalipwa, wanalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ni lazima tupange, kwamba, tuondoe ugomvi wa wakulima na wafugaji, tuondoe ugomvi wa wananchi waliokaa karibu na Hifadhi ya Serengeti na maeneo mengine kwa mipango. Tujadili kwamba, wanyama wapo kweli, lakini watu wameongezeka sasa, kipi kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua, haya yakifanyika maana yake ni nchi yetu itaenda kasi. Mipango hii ambayo inapangwa hapa tumeshaijadili mara kadhaa, tunamwelekeza Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila na

mwenzako wa Fedha. Miradi yetu ile viporo na ujue huko tunakoenda mwakani, unajua kuna nini mwakani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii viporo naomba mkaikamilishe, ili Wabunge, mimi nina mpango wa kurudi Bungeni sina mpango wa kuachia Jimbo. Sasa siwezi kurudi Bungeni kama Barabara yangu ya Tarime – Serengeti haijakamilika, maji ya Ziwa Victoria hayajaenda kule kwangu, kama vifaa vya maabara haujapeleka, kama hujaondoa ugomvi kati ya wakulima na wafugaji, kama hujaondoa mgogoro uliopo kati ya watu wa Hifadhi ya Serengeti, wananchi wangu na kule Serengeti kwenyewe. Haya mambo yanawezekana, huhitaji kuwa Profesa wala Daktari, ni *willingness.* Profesa jambo la ushauri la mwisho ni, wewe ni mtaalam, nendeni mkaangalie shida ipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *placement;* kama wanaweka mtu mahali, waweke mwenye uwezo. Tumewashauri mara kadhaa, angalieni Makatibu Tawala wa Mikoa ambao wanasimamia watumishi wote katika mikoa yetu. Waangalie Wakurugenzi wetu, wawachuje wale ambao wanaweza kufanya vizuri kazi ya mipango, kusimamia fedha na mapato yetu wabaki, wale ambao hawana sifa waondoeni, kuna shida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa ni kweli kwamba tuna shida ya *placement* katika nchi hii. Kuna watu hawana uwezo, lakini ni Mkurugenzi pale, kwa hiyo, mapato yanapotea. Leo watu wanakula fedha mbichi, hata kwenye masoko fedha zinapotea, kwenye minada fedha zinapotea, watu wetu hawalipi kodi, ukichunguza wale watumishi wenyewe ndio wanazipitisha katika mlango wa nyuma. Kwa hiyo, kupata fedha, nchi hii zimejaa tele ni mipango na *commitment,* inawezekana huhitaji kuwa msomi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, atafuata Mheshimiwa Juma Usonge na jiandae Mheshimiwa Abeid Ighondo.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa kuchangia katika mada hizi mbili ambazo zimeletwa na Waheshimiwa Mawaziri hapa. Nitaongelea zaidi kwenye suala zima la Mpango wa Maendeleo pamoja na vipaumbele vyake ambavyo wameweka. Naomba kuvinukuu, wameongelea suala la kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji na utoaji wa huduma, kukuza uwekezaji na biashara kuchochea maendeleo ya watu na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi katika suala zima la kukuza uwekezaji na biashara. Nilikuwa naangalia katika taarifa ya Mheshimiwa Profesa, pale ukurasa wa tisa, anazungumzia suala la uchangiaji katika ukuaji wa uchumi na sekta ambazo zinaongoza amezitaja pale; ametaja kilimo kina 15.9%, ujenzi 15.5%, madini 11%, viwanda na mtiririko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nitarudia kulisema na nimekuwa nikilirudia mara kwa mara. Kuna sekta moja ambayo tunaisahau sana katika suala zima la kuchangia ukuaji uchumi, lingeweza kuchukua nafasi kubwa sana kwa sababu, masuala ya viwanda pamoja na kwamba, viwanda ina asilimia tisa hapa, pengine ingekuwa na asilimia nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nazungumzia suala la uendelezaji miliki. Sekta ya miliki tunaisahau, lakini tujue kabisa sensa ya watu na makazi iliyopita imezungumza suala zima la ongezeko la watu, tumetoka milioni 48 sasa tupo milioni 61. Ukiangalia *population density* ambayo tulikuwa nayo mwaka 2012 mtu mmoja alikuwa anaweza ku-*occupy* hekta 2.5. Sasa hivi tuna hekta 1.4 kwa sensa ya mwaka 2022 tujue wazi kwamba, ardhi inazidi kwisha, watu wanaongezeka. Kwisha kwake kunatokana pia na mpangilio mbaya ambao pengine hatujaweza kuusimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukienda kwenye sekta ya miliki, uwekezaji wake ni rahisi na ni mzuri na unachangia katika sekta nyingi, watu wa viwanda watauza, watu wa chakula watauza, watu wengi wa kutosha watapa ajira. Ukiangalia hitaji la

makazi kwa watu na tunahitaji makazi, si yale tu ya kusambaa ya kwenda *horizontal,* tunataka yale ya *vertical. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mahitaji, nilisema hata juzi, ni nyumba 390,981 zijengwe kwa mwaka, lakini taasisi zetu zote ukiangalia *National Housing,* nenda sijui *Watumishi Housing* na nenda hizi *Real Estate* zilizopo za *private,* uwezo wao wa kujenga nyumba kwa mwaka ni nyumba 1,153. Sasa ni lini watafikisha hizo nyumba 300,000 kwa mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tukasema suala zima la kufungua wigo kwa wawekezaji. Tukazungumzia suala la *Diasporas* ambao wanapata hadhi maalum, waweze kuwekeza kwenye nyumba. Tukazungumzia suala la mtu wa nje, ambaye atakuja ajenge nyumba na kuuza, ataondoka, akijenga hapa anaiacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia masuala ya Mheshimiwa Mtemvu, kule kwake Magomeni Kota ambako tunasema unafanya *land pulling.* Unakusanya vijumba vyote vile ambavyo havina ile hadhi pengine, halafu wale watu wote wanapata nyumba katika yale maeneo, lakini unajenga kwa kwenda juu; uta-*save* ardhi yako, lakini *accommodation* ya watu wengi itakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili hatulioni kama ni suala linalochangia kwenye ukuaji. Hizi sekta zilizowekwa nadhani sekta ya miliki ingeweza kushika hata nafasi ya tatu au ya nne katika uchangiaji wa uchumi. Ningeomba sana Serikali, tumelisema sana hili, tuone namna bora ya kuona ni jinsi gani tutakwenda kushirikisha sekta hii ili iweze kuingia kwenye ukuaji wa uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie madini, wanafanya vizuri sana, hasa hawa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, tungeomba sasa ule umiliki wa ardhi kwa hawa wachimbaji, waweze kumilikishwa maeneo yao yale, lakini pia, watatumia ardhi ile katika kujiongezea mitaji. Wanapoongeza mitaji tayari pia, kunakuwa na wigo wa kuongeza uchumi katika suala zima la

ongezeko la fedha. Bila kuwawezesha kwa kuwa na miliki ya ardhi bado itakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala zima la wafugaji, sasa hivi ni wachungaji, wanaofuga ni wachache sana. Nako pia, tukaangalia wale wenye maeneo wakapewa elimu ya kuweza kufuga wa ufugaji wa kisasa, wakazalisha nyasi wao wenyewe kwa chakula, itakuwa imesaidia sana hata ile migogoro iliyopo. Tukaacha yale maeneo ya vijiji ambayo wametenga, kwa ajili ya wafugaji, kuna wale ambao ni ma-*settler* wana maeneo yao, lakini bado wanataka kuingia kwenye maeneo mengine. Wale wawezeshwe namna ya kuweza kulima nyasi, waweze kuzalisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Sekta ya Uvuvi inakwenda vizuri na inafanya vizuri, lakini tuone namna bora sasa ya kuwa na utunzaji wa mazalia ya samaki, ili yaweze kutunzwa pale tunapotaka kuvua samaki, maana yake ni yaende kwa msimu. Maeneo mengine yaachwe yaendelee kama yalivyo, lakini tuwe na maeneo *specific* ambayo tunajua kwamba, tunaenda kuvuna samaki pale na ongezeko lake limekuwa ni kubwa. Kwa hiyo, ni vizuri pia, tukaangalia sekta hizi katika suala zima la kuwawezesha wanaosimamia na kuweza kuona ni jinsi gani watakwenda katika kutunza mazingira, lakini pia na kuweza kufanya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Serikali kwenye Sekta ya Uchukuzi na usafirishaji wamefanya vizuri kabisa katika miundombinu yote *SGR*, bandari na mambo mengine. Kuna miradi tunayoianza haiishi kwa wakati, viwanja vya ndege, Uwanja wa Ndege wa Mwanza uko pale kila leo na hata kwenye maandiko hapa sikuona wapi upo? Labda mtu atanisaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekaa pale, kuna changamoto ya watu wanadai fidia na uwanja umesimama hauwezi kuendelezwa. Ningeomba sana miradi ikianza ikamilike ili tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji. Jana wamempongeza Mheshimiwa Aweso na mimi nampongeza sana

kwa miundombinu ya kawaida ameweka. Changamoto iliyopo ni usambazaji wa maji yale, miundombinu iliyopo ni chakavu, mingine toka watu wapo 100,000 na sasa watu wapo 500,000 haiwezekani miundombinu ileile iweze kusambaza maji. Utaweka matenki makubwa, utaongeza vyanzo vya maji, lakini kama hatufumui mfumo mzima wa usambazaji bado changamoto itakuwepo. Kwa mfano, watu wa Mwanza hawaelewi maji yanatoka Mwanza, Shinyanga, sasa yanakuja Dodoma halafu Mwanza wana changamoto ya maji na maji yapo Ziwa Victoria, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, miundombinu yetu ya usambazaji maji ndio inayotakiwa kuboreshwa kwa sababu, matenki ya *reserve* yapo mengi, chanzo kipo kimewekwa, changamoto tu ni namna ya kuweka miundombinu itakayofuatilia usambazaji katika maeneo haya. Tukilifanya hili itakuwa imetusaidia sana katika suala zima la kuondoa changamoto iliyopo na kuweza kuendelea kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo amepongezwa na kuweza kupewa *degree* kutoka kwenye kile Chuo Kikuu kule India, wametambua mchango wake. Kwa hiyo, sisi kama Tanzania hatuna budi kuendelea kumuunga mkono pale ambapo yeye kasimamia zile *R4,* zipo vizuri. Kwa hiyo na sisi tuendelee kuhakikisha kwamba, Mheshimiwa Rais…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kengele ya pili.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Hawa ni walimu ambao ni

mabalozi wa kupinga ukatili kutoka Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa *Innocent* Bashungwa, Waziri wa Ujenzi. Hawa ni wapiga kura wake kutoka Karagwe, Mkoa wa Kagera. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, ambao ni Chama cha Mabroka wa Madini Nchini (CHAMMATA) kutoka Longido, Mkoa wa Arusha. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Keneth Nollo, mpiga kura wake kutoka Wilaya ya Bahi, Mkoa wa Dodoma. Karibu. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ambao ni Wafamasia kutoka Hospitali ya Mkoa wa Dodoma *(General Hospital)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ambao ni marafiki zake kutoka Kyerwa, Mkoa wa Kagera. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Mwandabila, Viongozi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa kutoka Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Janeth Mahawangwa, Wajasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mwenyekiti wa Machifu kutoka Usukumani, ambaye ameambatana na wapiga kura wake kutoka Kisesa, Mkoa wa Simiyu. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 38 wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ambao ni Watumishi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T), Jimbo la Kusini Magharibi, Mkoa wa Iringa. Karibuni. *(Makofi)*

Vilevile wapo wageni 110 wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, wanafunzi 100 na Walimu 10 wa Chuo cha Ualimu Bustani kutoka Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 110 wa Mheshimiwa Josephat Gwajima. Hawa ni Maaskofu na Wachungaji kutoka Madhehebu Mbalimbali Nchini Tanzania. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Usonge, jiandae Mheshimiwa Abeid Ighondo na jiandae Mheshimiwa Riziki Said Lulida.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipatia fursa hii ya kuweza kusimama kutoa mchango wangu pamoja na maoni, kufuatia taarifa tatu zilizowasilishwa hapa Bungeni. Taarifa ya Kamati ambayo inashughulika na Masuala ya Bajeti, taarifa ambayo imewasilishwa na Waziri wa Nchi, Mipango na Uwekezaji pamoja Taarifa ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nikupongeze sana. Niwapongeze sana Mawaziri na pia, nimpongeze sana Rais, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuweza kuisogeza mbele nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nijikite zaidi kwenye maeneo makuu matatu; eneo la kwanza, nitajikita kwenye masuala ya mazingira ambayo yapo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Eneo la pili, nitajikita zaidi kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii na eneo la tatu, nitajikita zaidi kwenye eneo la Wizara ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, nikiri kwamba, kweli Mheshimiwa Waziri amezungumzia wazi kabisa miradi yote ya mazingira, hususani ile ya tabia ya nchi, mbali na changamoto ambayo tunaipata kwa sababu, mifuko hii tunategemea fedha nyingi kutoka kwa wadau wetu wahisani kutoka nje. Wizara imetamka wazi kabisa, kwenye mpango wetu huu ambao tayari tunaenda nao itajikita zaidi kukusanya fedha ndani ya nchi kwa ajili ya kutekeleza ile miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati, tumekuwa tukilalamika sana kwenye Kamati yetu kuhusiana na miradi yetu mikubwa, ni mizuri, lakini mwisho wa siku inakosa fedha, kwa ajili kuiendeleza. Sasa, Mheshimiwa Waziri, ameyazungumza hapa leo kwamba, miradi hiyo sasa hivi itatengewa fedha kupitia Wizara zetu. Kwa hiyo, ni jambo kubwa na ni la kupongezwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukiangalia kwenye miradi kama hii ya mazingira ni miradi ambayo inakuwa sura ya kimuungano na fedha ambazo zinapatikana zinakuwa zinagawiwa, nusu zinabakia huku Tanzania bara na nusu zinaenda Zanzibar. Ukweli usiopingika ni mabadiliko ya tabianchi, hususani kwa upande wa Zanzibar, ndiyo inayaumiza zaidi. Kwa hiyo, niombe sana Wizara, kwenye mgawanyo wa fedha ambazo tayari tutakuwa tunazipata tuhakikishe kwamba, upande wa Zanzibar nao tunaelekezea fedha nyingi, kwa ajili ya kunusuru Kisiwa chetu cha Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengi yamelalamikiwa hapa na Wabunge mbalimbali. Kwa mfano, kuna maeneo ya kule Pemba, nayo sasahivi yanaathirika na ujio mkubwa wa maji, pia, maeneo ya Nungwi, maeneo ya Mjini pale *Stone Town,* yote hayo kutokana na mabadiliko ya tabianchi maji sasa hivi yanaingia kwenye mitaa ya watu. Fedha tunazozitegemea tayari ni za Muungano kwa hiyo, niiombe sana Wizara kwenye hili ni lazima tuliangalie, lakini pia, tuiangalie Zanzibar kiupekee zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni, Maliasili na Utalii. Kwenye eneo hili Mheshimiwa Rais ni lazima tumpongeze sana kwa asilimia mia moja. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais amejivua Urais akasema lazima niingie mtaani, niingie msituni, niingie baharini, kuhakikisha Tanzania naitangaza. Kwa hiyo, lazima Mheshimiwa Rais kwenye eneo hili tumpongeze sana kusema ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameutangaza utalii na sasa hivi ukiingia maeneo yote duniani kote *Royal Tour* ndiyo inazungumzwa zaidi. Kwenye eneo hili Mheshimiwa, kama Wizara, lazima tujipange pia, tumhakikishie Mheshimiwa Rais ile

*target* ya kusema kwamba, tunataka tuingize watalii wasiopungua 5,000,000 basi tuifikie. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Mipango amezungumzia kwamba, mpaka sasa hivi tumeshaingiza watalii wasiopungua 3,000,000 na *points*, lakini *target* hii tutaifikiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Wizara iweke mipango mikakati ili kuhakikisha kwamba, utalii utaongezeka zaidi na *target* yetu ya 5,000,000 inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni utalii wa fukwe tumeuacha na tumejikita zaidi kwenye utalii wa wanyama pori, milima pamoja na misitu, lakini kwenye utalii wa fukwe bado hatujaweka mikakati. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, angalia zaidi kwenye eneo la fukwe, tunayo maeneo mengi bado hatujawekeza. Tukiwekeza zaidi kwenye fukwe naamini kwa 100% ile *target* ya Mheshimiwa Rais kufikia watalii 5,000,000 tutaifikia na tunaweza tukaongeza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri tuangalie nchi ya *Morocco,* wao hawana wanyama na milima, lakini wana fukwe za Sahara na wanaingiza watalii zaidi ya milioni 10 kwa mwaka. Kwa nini Tanzania ambao tumebarikiwa na vivutio vingi vya kiutalii tusifikie kwenye *target* hiyo ya milioni tano? Ninaamini kabisa kwenye eneo hili tunaenda kuongeza watalii mara dufu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hilohilo la utaalii pia tuangalie zaidi utalii wa vyakula, bado huko hatujawekeza zaidi kwenye eneo la vyakula. Sasa hivi ukiangalia ukienda kwenye hoteli nyingi za kitalii, vyakula vingi vinavyoagizwa utasikia south Afrika au Nchini Kenya, lakini nchini kwetu vyakula vingi ambavyo tunazalisha ni vyakula vilevile *traditional crops*, ni vyakula vya kikawaida tu ambavyo vyote tumevizoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watalii wenzetu hawa wanapotoka duniani kuna vyakula vyao wamevizoea na wanapokuja kwenye nchi zetu hizi mara nyingi sana wanapendelea vyakula ambavyo wametoka navyo nyumbani kwao huku pia wavikute. Kwa hiyo, tuangalie namna gani

tunaweka mkakati kutafuta mbegu kabisa za Ulaya, zikaja hapa nchini kwetu tukapata fursa na wakulima wetu wakaweza kulima mazao hayo baadaye wakapata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwenye Wizara ya Uvuvi, bado nitaendelea kuzungumza zaidi na Mheshimiwa Ulega kwenye zao la mwani. Niipongeze sana Wizara yako, imejitahidi sana kutoa elimu kwenye zao la mwani. Kwa sasa hivi elimu imewafikia Watanzania kwa 100% kwa hiyo niwapongeze sana kwenye hilo, nimeona mikakati yako mizuri kabisa ya kuisaidia nchi hii hususan kwenye *blue economy* lakini zaidi kwenye zao hili la mwani, bado hatujaweka mikakati zaidi ya mwani kuwa na thamani zaidi. Wakulima wengi wanalalamika, mwani unanunuliwa, lakini thamani ya mwani ni ndogo sana kwa wakulima wetu. Kwa hiyo niiombe sana Wizara kwa sasa hivi tuweke mikakati zao letu la mwani liweze kuwa na thamani ili mkulima aweze kufurahia kama mazao mengine ya korosho, ufuta na mazao mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, niwashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abeid Ighondo, wajiandae Mheshimiwa Lulinda na Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa niseme maneno yangu machache kuhusu ajenda hii iliyopo mezani kwetu hapa. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan, ambaye kusema kweli kwa kipindi kifupi hiki cha uongozi wake tumeona akiboresha maeneo mengi sana ya huduma, kuboresha miundombinu, kuboresha kila eneo ambalo tunawapata wananchi wetu wakimhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeona hata michango ya Wabunge humu ndani kila Mbunge anayesimama anasema jambo fulani limefanyika kwenye eneo lake, haya ni maono ya Mheshimiwa Rais wetu na tunahitaji kuendelea kumpa moyo na

kumwombea ili aendelee kututumikia wananchi wenzake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sijawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Profesa Kitila kwa taarifa zao nzuri ambazo wameziwasilisha na hivyo na mimi niweke mchango wangu mahususi kwenye hotuba zao hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo manne kwa haraka haraka kwa ufupi. Nataka nizungumzie kilimo, mifugo, viwanda pamoja na miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Ninapokwenda kuzungumza maeneo haya hasa kwenye maeneo haya ya sekta za uzalishaji ambayo ni kilimo, mifugo iweze ku-*link* na viwanda kwa maana ya kwenda kusindika, tuzalishe kwa wingi ili tuweze kwenda kusindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kilimo ninampongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Bashe kwa kuweka kipaumbele na kuongeza bajeti kwenye eneo hili la kilimo. Kule kwangu ameniletea mradi mkubwa sana wa umwagiliaji pale Msange na ninataka kusisitiza hapa kwamba kipindi hiki ili tuweze kuukomboa uchumi wetu, tuondokane na uchumi huu tunaosema unaochechemea tuweze kuusogeza uende huko kwenye uchumi ambao ni endelevu, lazima tuwekeze kwenye hizi sekta za uzalishaji hasa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tunaenda kuwekeza kwenye kilimo lazima tuondoke kwenye kile kilimo cha kizamani, kilimo cha kutumia jembe la mkono. Kwa mazingira hayo lazima tuwekeze sana kwenye zana za kilimo zile zinazotusaidia kulima kwa maana ya matrekta, teknolojia lakini pia na miundombinu yenyewe kwa maana ya umwagiliaji pia lazima tuwekeze kwenye tafiti, hatuwezi kujikomboa hapa kama hatujawekeza kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye utafiti tuna taasisi zetu zinazofanya utafiti. Kuna hii taasisi ya *CAMARTEC* na kuna *TEMDO* mbazo ni mahsusi kwa ajili ya utafiti, lakini hizi taasisi hazijawezeshwa, zenyewe zipo kwa ajili ya utafiti kwenye zana za

kilimo, lakini hazina nyezo, hazina fedha. Zitengewe bajeti ya kutosha ili sasa ziweze kufanya kazi ya kutuletea mbinu bora za namna gani tunaenda kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mbegu, hatuwezi kulima. Msingi hasa wa kilimo ni mbegu, unapokwenda shambani msingi namba moja ni mbegu. Ukikosea tu kwenye mbegu ina maana mwaka mzima umepotea na *resource* zote unaweza kwenda kuziwekeza kwenye kilimo zimepotea. Sasa ni muhimu sana, tunapoongeza kwa kiwango fulani kuna juhudi fulani zimefanyika lakini bado tupo nyuma mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitolea mfano Singida tunalima sana alizeti na hapo mwanzo kulikuwa kuna juhudi za kuhakikisha kilimo cha alizeti kinakuwa ni zao la kimkakati la kitaifa kwa ajili ya kuzalisha mafuta, lakini mbegu tulizozipata hazijatusaidia. Wakulima wetu wanahitaji *hybrid seeds* ambazo zinatoa mafuta mengi angalau gunia moja lenye kilo 60/70 litoe dumu moja na ziada. Sasa hivi hata hilo gunia moja haliwezi kutoa hata galoni tatu. Pia hapo hekta moja haiwezi kutoa hata gunia kumi. Kwa hiyo, tunampotezea mkulima muda, anaenda anafanya kazi kubwa lakini hakuna anachovuna. Kwa hiyo, ninasisitiza hapa ni lazima tuhakikishe tunatazama eneo la mbegu bora za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la teknolojia pia nimesema tafiti lakini lazima tu-*link* na teknolojia yetu. Teknolojia yetu tunatumia bado duni mno, tuondoke huko. Ni lazima tuweke kipaumbele kwenye teknolojia yetu, tuondoke kwenye kile kilimo cha kutumia zana za zamani za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia pia eneo la ugani. Ni kweli tumewekeza sana hapa na ninampongeza Mheshimiwa Rais. Maafisa Ugani tumewapa vitendea kazi kwa maana ya pikipiki, vile vifaa vya kupima udongo vya kutosha lakini hapa bado tunahitaji kuwasimamia na kulisimamia eneo hili ipasavyo. Mheshimiwa Waziri Bashe kama yupo hapa ndani ninamwomba awekeze sana kwenye usimamizi. Hizi rasilimali zilizopelekwa huko zitumike ipasavyo ili zimfae mkulima, kwa sababu zile zimepelekwa kwa ajili ya kumsaidia mkulima. Kwa hiyo,

zisimamiwe ili ziweze kuleta tija ambayo ilikuwa inakusudiwa na iliyokuwa inatarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo pia kuna eneo la masoko, tutazalisha, lakini bila kuwa na masoko imara ili mkulima wetu aweze kuona tija ya kilimo, alime auze bei nzuri, alime alizeti aone bei yake nzuri anayoenda kuuza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele nyingi hapo! Nikienda kwenye eneo la mifugo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah! Basi kwenye eneo la miundombinu nisisitize hizi Barabara, *trunk roads,* pia na zile zinazounganisha Mikoa na Wilaya. Sisi kule tuna barabara ile ya kutoka Singida - Ilongero kwenda Haydom hii barabara inakwenda inaunganisha Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Simiyu na Mara, mtu hatahitaji kwenda Mwanza, atakatiza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, kaa chini.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lulida na ajiandae Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja ya mpango iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Kitila Mkumbo, Waziri wa Uwekezaji, lakini bila kuwa na umuhimu sana ninampongeza Mheshimiwa Waziri William Wanging'ombe Lukuvi, kwa kweli nasema Mwenyezi Mungu azidi kuwalinda na azidi

kuwabariki na niliku-*miss* sana Mheshimiwa Lukuvi, lakini leo kwa uwepo wako hapo nimefarijika sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu nitazungumzia maeneo matatu. Eneo la kwanza ni maendeleo katika mikoa kimkakati lakini nitauzungumzia kwanza Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi katika Majimbo Nane ya ukoloni ilikuwa ni Jimbo mojawapo, walilolitambua kama ni Jimbo la maendeleo. Hivyo katika Majimbo Nane - Lindi ilikuwa ni Makao Makuu ya *Southern Province* ikiwemo Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Mtwara. Leo tunapoizungumzia Lindi ni Mkoa maskini kwa vile haikutengenezewa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa 13 ambayo tulikuwa tunasema ni Mikoa maskini Tanzania ikiwemo Dodoma, miundombinu iliyopelekwa Dodoma imeifanya Dodoma kuonekana ni mkoa tajiri, sasa niulize kwa nini Lindi wameiacha? Imeachwa kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi tulikuwa na *airport*, ile *airport* ilikuwa ni ya pili katika Afrika. Ilikuwa ndege *British Airways*, ikitoka London inatua Alexandria, ikitoka Alexandria inatua Lindi chini ya *KAR* halafu inakwenda South Afrika, Johannesburg. Jiulize je, *airport* ya Lindi unaiongeleaje katika mfumo wa dunia, haimo. Mkoa wa Lindi katika bandari ambazo zilikuwa zinafanyakazi mojawapo ni Bandari ya Lindi, lakini jiulize leo unaiona wapi Bandari ya Lindi? Haipo, haionekani! Viwanda vyote havionekani, vimeingia katika uwekezaji wamevifunga. Lakini inasikitisha kuona ni Manispaa maskini, lakini ina uwezo mkubwa wa kuzalisha. Hivyo, naomba Waziri wa Fedha ambaye ni balozi wa watu wenye ulemavu iangalie Lindi kwa umakini, isiwe mikoa mingine inakimbia mingine inakuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 Septemba, Mheshimiwa Rais alikuwa Lindi, kwa kweli alihuzunika. Alifarijika kwa sababu mbili. Moja, alikutana na watu wa Lindi ambao walimpokea kwa umahiri sana. Katika mikoa ambayo Mheshimiwa Rais katika utembezi wake na kuzunguka kwake, Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi ulivunja rekodi kwa watu kumkubali. Alitoa kauli moja,

nina deni na Mkoa wa Lindi. Katika msafara ule Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitembea na Mawaziri, niliwaona Mheshimiwa Waziri Bashungwa, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Uchukuzi na hizi hoja wakati zinaletwa pale walikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze Waziri Bashungwa. Baada ya kuingia mafuriko alikaa *site* na alihakikisha barabara zile zinapitika, Mwenyezi Mungu akulinde zaidi, hii ni mara ya pili nampongeza Mheshimiwa Bashungwa. Alitoa ahadi kwa wanawake wale waliowalisha chakula pale Somanga kwamba utawaletea majiko ya gesi, mimi nipo tayari kuyapokea majiko ya gesi nikawagawie Liwale na Somanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa nendeni mkaiangalie Bandari ya Lindi, naomba Kamati kama Mungu atawajalia waende Lindi katika kikao kinachofuatia. Waone bandari ile, haina miundombinu ya aina yoyote. Leo Nchi ya Comoro imeamua kuja kuwekeza katika Bandari ya Lindi kwa kutumia *wharfage,* majahazi na kila kitu, wanaweka wapi mizigo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tulikuwa tunasikia hela zinatengwa, zinaenda wapi? Nikitoka katika Bunge hili, kwa kumuunga Mheshimiwa Rais, mimi nipo tayari kwenda Lindi, lakini naomba niende Lindi na Waziri wa Uchukuzi na timu yake yote kuanzia Katibu Mkuu, Meneja wa Bandari, Mkurugenzi Mkuu wa Bandari tukakae Lindi tuhakikishe Lindi ile yenye maendeleo inawezekana. Inafikia mahali unajiuliza kwa nini Lindi imesimama, lakini imesimamishwa mikoa mingine imepelekwa mbele na imepewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Bashungwa, umepambana na kwa kweli Serikali imepeleka bilioni 140 kwa ajili ya kuhakikisha zile barabara ambazo zilikufa zinafufuka, lakini leo mvua ikinyesha kuanzia mwezi ujao Liwale haipitiki, Nachingwea haipitiki, inasikitisha sana. Haiwezekani mikoa ambayo inazalisha mazao ya fedha za kigeni ikiwemo korosho na ufuta inaongoza ufuta katika Afrika lakini leo kajiulize, mtu kutoka Liwale anautoaje ufuta wake kuuleta Lindi, inakuwa ni

tatizo. Hivyo tukae kwa pamoja, hii nchi ni ya sungura wa wote, tuweze kuisimamia Lindi na iweze kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia aibu kuiona Lindi ambayo ina uchumi katika upande wa madini leo imekuwa ya pili kwa madini Tanzania, nenda kajiulize madini yale yanafanya nini? Hakuna barabara, hakuna miundombinu, kitu ambacho ni aibu. Leo ukimwambia Waziri aende Liwale atakwambia kwa mwaka mmoja naenda mara moja kwa vile hakupitiki, lakini jiulize Liwale ambayo inadhalilishwa leo alitoka Waziri Mkuu wa kwanza Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, hajaenziwa mpaka leo! Sitakubali, kama mwezi huu hawatakwenda watu hawa kwenda kuisimamia.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri sana. Hongera sana na Lindi itafanikiwa usiwe na hofu.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja, lakini nikiondoka na Mawaziri wa Uchukuzi na timu yake ya Bandari tuhakikishe Bandari ya Lindi na *airport* ya Lindi inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Pia ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2025/2026. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, vilevile ninampongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Mpango. Vilevile niungane na wote waliopongeza kwa kuanzisha Wizara hii ya Mipango na kuwaweka watu makini ambao kwa kweli tumeona mipango yetu mingi imeanza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na sekta ya maji. Maji ni uhai, kila mtu anahitaji maji, viumbe vinahitaji maji, kilimo

kinahitaji maji. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sera yake ya kumtua mwanamke ndoo kichwani, kwa kweli tunampongeza sana, tunajua kwamba toka akiwa Makamu wa Rais hii ilikuwa ni ndoto yake kwamba wanawake sasa tutuliwe ndoo kichwani na hii ni heshima kwa sisi wanawake wote nchi nzima kwamba, Mama amekwenda kugusa vitu ambavyo vinamjengea heshima mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yamefanya hata ndoa zetu zimeanza kuimarika kwa kiasi kikubwa, pia maji yamefanya mwanamke sasa hata kuweza kufanya kazi za uzalishaji kwa sababu muda mwingi sana alikuwa akitumia kutafuta maji. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, wetu na apewe maua yake mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze sana Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ametimiza ndoto ya mama yetu na tumeona kwa kweli akifanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba mwanamke anatuliwa ndoo kichwani kwa miradi mingi ambayo ipo katika Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mpango maalum kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa maji safi na salama na lengo la dira ya miaka mitano inasema kwamba upatikanaji wa maji unatakiwa 85% vijijini na 90% mijini lakini taarifa ya mwaka 2023/2024 inaonesha kwamba mpaka sasa hivi upatikanaji wa maji umefikia 70% vijijini na 90% mijini. Lengo hili nafikiri inatakiwa sasa miaka mitano ni mwakani mwaka 2025 tunatakiwa tufikie hilo lengo lakini zipo changamoto nyingi sana ambazo zinasababisha lengo hili pengine ikawa shida lakini tunaomba kwa sababu uhalisia ukiangalia hizi asilimia unakuta bado akinamama wanahangaika na maji hasa huko vijijini, kwa hiyo ninaomba sasa, hizi changamoto angalau zifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ni fedha za Mfuko wa Maji, kutowasilishwa katika Mfuko huo kwa sheria inayofuata. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, nakumbuka kwamba tulimwita kwenye Kamati yetu na ninaipongeza Kamati yetu ya Maji na Mazingira.

Kwa kweli mara nyingi sana imekuwa ikihakikisha kwamba suala hili linafanyika vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, alikuja na tukaweka mkakati kuhakikisha sasa huu mfuko unafanya vizuri zaidi ili pesa zipatikane nyingi katika hii Wizara ili miradi iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kumekuwepo na changamoto kubwa ya madeni ya wazabuni na wakandarasi kutolipwa kwa wakati na kusababisha hiyo miradi kucheleweshwa. Sasa gharama inaongezeka kwa sababu miradi inakuwa inachelewa kukamilika kwa wakati. Pia, kunakuwa na riba kubwa sana ya madeni. Kwa hiyo, naomba hili pia lichukuliwe kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumekuwa na mitambo. Tunaishukuru sana Serikali yetu, wametuletea mitambo karibu kila mkoa. Hii mitambo ya maji ipo, lakini tatizo kubwa sasa ni ukosefu wa fedha, ili hii mitambo iweze kusaidia uchimbaji wa visima sehemu ambapo hakuna miradi ya maji. Kwa hiyo, naomba sana hizi changamoto ziangaliwe kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna changamoto kubwa ambapo kumekuwa na madeni ya huduma za taasisi za Serikali. Tumeona ripoti ya 2023/2024, wanadaiwa karibu shilingi bilioni 45. Hili jambo kwa kweli tumelizungumzia sana kama Kamati na kama Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa nini taasisi za Serikali zinadaiwa wakati zinatakiwa ziilipe Wizara ya Maji? Sasa mpango mkakati ni nini? Je, sasa wanazilipaje ili hizi pesa ziende kusaidia miradi ya maji ili sasa mwanamke kweli atuliwe ndoo ya maji kichwani na Mheshimiwa Rais wetu aweze kuifikia ndoto yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona pia kuna gharama kubwa sana ya umeme kwa ajili ya kuendesha huduma ya mamlaka zetu nchini. Sasa tulikuwa tunaomba, kwa sababu tulivyozitembelea mamlaka nyingine zinalipa umeme karibu shilingi bilioni mbili kwa mwezi. Inasababisha *unit* ya maji inapanda

sana kiasi kwamba gharama ya maji inakuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu. Huu Mpango wa Taifa wa Maendeleo ushughulikie changamoto zifuatazo: kwanza, kulipa madeni kwa wakandarasi na kuwasilisha fedha za Mfuko wa Maji zinazokusanywa kwenye chanzo. Pia, matumizi ya mitambo basi yatengewe fedha maalum ili visima vingi viweze kuchimbwa na mabwawa mengi yaweze kuchimbwa. Kuwe na mpango mkakati ili taasisi za Serikali zilipe madeni yake. Pia, Serikali ione uwezekano wa kupunguza gharama za umeme ili kuwezesha uendeshaji kuwa rahisi zaidi. Kwa sababu tulienda kwenye vijiji, tumekuta *units* za vijijini ni kubwa kuliko mijini. Kwa hiyo watu wanashindwa kuunganisha maji vijijini kwa sababu bei ya gharama ya uendeshaji wa miradi ni kubwa sana. Kwa hiyo, ninaomba hili liangaliwe ili watu wengi huko vijijini waweze kuunganisha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifanyike pia tathmini ya upatikanaji wa maji nchini kuanzia ngazi ya vijiji, kata, tarafa, wilaya na mkoa ili kupata hali halisi, kwa sababu tumeona uhalisia hauoneshi jinsi ambavyo tunapata hizo tathmini, lakini ukienda huko chini unakuta kwamba, bado kuna changamoto kubwa sana ya maji pamoja na tunapata asilimia inakuwa kubwa. Ili tathmini itoe majibu sahihi itakayosema, kuandaa mpango ili miundombinu ya maji iwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa naangalia *REA,* unaona kwamba sasa hivi tuko kwenye vijiji halafu baadaye tunaenda sasa kwenye vitongoji. Sasa hata kwenye maji iwepo tathmini kama hiyo, kwamba, je, vijiji vingapi vimeshapata maji? Sasa bado vitongoji vingapi kila eneo? Hii itatusaidia na sisi kuwa na tathmini kwamba sehemu ambapo hakuna maji sasa ni kitongoji fulani ambacho tunapambana miundombinu iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hivi visima vinachimbwa, lakini hamna usambazaji lakini miundombinu haiwekwi miundombinu ili watu wapate maji. Pia, tumeona vile vituo vya maji vinakuwa mbali sana kiasi kwamba wanawake bado

wanabeba ndoo kichwani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Maji, tunaomba sana hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusiana na Liganga na Mchuchuma... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mafuwe, wajiandae Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Mama Sitta na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla sijachangia Mpango, ninaomba niweze kuomba mambo matano. Moja ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, walipe wakandarasi. Watu ambao wamehudumia Serikali wengi wanapata taabu na wanafilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba sana waanze kufikiria sasa kuanza kujenga treni ya mwendokasi kuelekea Kilimanjaro. Itoke Dar es Salaam kwenda Moshi – Arusha. Pia, naomba sasa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wanafahamu kwamba tumetengewa shilingi bilioni 11.6 kwa ajili ya Ujenzi wa Soko la Kwa Sadala. Tafadhalini sana, tunaomba hii fedha ili soko lianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia hili suala la Liganga na Mchuchuma, tangu nasoma shule ya msingi ninalisikia linazungumzwa. Ifike mahali liishe na sisi watu wa Hai tuliomba na wakasema wataweka kwenye mpango kwamba kile kiwanda cha mashine *tools* kiwe kinapata *material* kutoka huko. Kwa hiyo, jambo hili lifike mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwenye maombi yangu, wapokee utaratibu ambao tumewashauri hapa kwenda kwenye *cashless.* Haya mambo ya kutumia pesa kwa maana ya makaratasi, yanatuchelewesha. Tukubali na tupokee ushauri huo. Baada ya kusema hayo, sasa nichangie mpango ulioko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele ambavyo wameviweka ni kwamba wamesema, ukurasa ule wa 13, "kuimarika kwa upatikanaji wa usalama wa chakula." Ndiyo ninataka nichangie hapa. Wenzangu wengi wamezungumza, tunaposema upatikanaji wa usalama wa chakula ni nini? Tumeona mipango ambayo Serikali wameweka mbele yetu na tumeona maoni ya Watanzania wengi wakati wanachangia mawazo yao kwenye Maono ya Mpango ya Miaka 50 ijayo. Wengi, takribani watu 1,170,000 walioshiriki wamesema kipaumbele cha nchi hii kiwe ni kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ifike mahali tutoke kwenye maneno, twende kwenye vitendo. Tunaposema kilimo, tuone *output* ya kilimo, tuone tunazalisha na tunauza. Tusiongee sana, tumeshaongea na muda umefika sasa wa kulima kilimo ambacho kitakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri, tungeweza kuigawa nchi yetu katika kanda mbalimbali kulingana na aina ya ardhi na upatikanaji wa maji. Kwa mfano, tukasema Kanda ya Ziwa tulime zao hili, kwenye mkoa huu tulime aina ya zao moja lakini kwenye kilimo hicho, tuongezee thamani mazao. Kama tunasema tunalima nanasi, basi tuweke mashamba ya nanasi, tuweke umwagiliaji wa kutosha na tuweke viwanda vya kutengeneza juisi ya nanasi ili mtu alime afikishe bidhaa mwisho. Tuhangaike kutafuta masoko huko duniani. Kuliko hivi tunavyolima kidogo kidogo halafu hatuna umahiri kwenye zao fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukisema Ukanda huu wa Kaskazini walime mahindi na maharage. Ni vizuri ifike mahali viongozi wetu walioko kwenye mikoa na wilaya ukimwambia Mkoa wa Kilimanjaro, wewe tunakupa *target* ya tani bilioni kadhaa za mahindi. Usipofikia hicho ndiyo kipimo chako.

Ukifanya vizuri maana yake umefanikiwa na ukishindwa umeshindwa, ndiyo kipimo kiwe hivyo. Kwa hiyo, kwa kufanya hivi tutajikuta nchi yetu ina chakula cha kujitosheleza na tutaweza kuuza nje ya nchi kwa kuongezea thamani mazao tuliyonayo na ni sambamba na kujenga viwanda na hili linawezekana. Tukubaliane kwamba, kama tunaweka zao hili, kila zao ambalo tutapanga kulilima liwe na kiwanda chake cha kuongeza thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wamezungumza kwenye mpango kama kipaumbele cha tatu, wamesema kuongezeka kwa ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli za uwekezaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema Sekta Binafsi iingie, tunaiandalia mazingira gani hii Sekta Binafsi? Leo ukiangalia sheria zetu za kodi, siyo rafiki hata kidogo. Ninasema bado zina *hangover* ya kikoloni, kwa sababu wale walioko *TRA* wanamwona mfanyabiashara ni adui. Sasa hili siyo sawa. Tufike mahali tu-*regulate* sheria zetu za kodi, ziwe rafiki. Yule anayeenda ku-*charge* kodi pale aone kwamba kuna mtu kawekeza fedha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunapofanya *auditing*, mtu anapeleka ripoti yake *TRA* inawekwa mezani, mtu anazikusanya zaidi ya miaka minne hazijafanyiwa kazi, lakini angeenda mwaka huo akapewa ripoti yake akaambiwa ulikosea hapa, inamsaidia mwakani kubadilika. Pia wale watumishi walioko *TRA* wakumbushwe kwamba wana wajibu wa kulea wafanyabiashara. Siyo hivyo wanavyoishi, wanataka kukamua ng'ombe, lakini kumlisha ng'ombe hawataki, siyo shughuli yao na inafika mahali wanaona ni fahari kufunga biashara za wafanyabiashara. Ni fahari kwao kufilisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali hiyo *attitude* ibadilike, kwamba ikifika meneja wa mkoa kuna mfanyabiashara amefilisika, wewe meneja tuku-*charge* kwamba kwa nini huyu amefilisika? Hukumshauri vizuri. Kwa hiyo, hilo na lenyewe lionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema uwekezaji, pia naomba nizungumze jambo moja. Tulinde wawekezaji na wafanyabiashara wetu wa ndani. Pamoja na kwamba mimi ni muumini sana wa diplomasia; hivi jamani kinachoendelea pale Kariakoo mnakiona? Wale wageni waliojaa pale, anazalisha kule kwao China, anakuja na kontena, anaenda analiweka ndani halafu anachukua yeye mwenyewe anaenda kupanga pale anauza. Mnategemea ushindani wa biashara sisi Watanzania tutaweza kushindana nao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, tunatakiwa kuendelea na mahusiano mazuri na wenzetu, lakini ni lazima tulinde watu wetu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wafanye *research* kinachoendelea pale Kariakoo. Vinginevyo wale watu watakimbia pale; watashindwa kufanya biashara na wafanyabiashara wetu watafilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kusema na niliuliza swali juzi hapa kuhusiana na *CSR* kwenye Mlima Kilimanjaro. Sikatai Mlima Kilimanjaro ni wa kwetu wote, lakini maeneo mengine kwa mfano wanaofanya biashara ya dhahabu utakuta wako ndani ya maeneo yetu lakini wanapata *CSR*. Pia, sisi Mkoa wa Kilimanjaro siyo mbaya wakafikiria namna ya kutengeneza sheria ili na sisi tupate *CSR* kutokana na maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa Mkoa kama Kilimanjaro na wilaya ambazo maeneo yao ni madogo sana, sisi Wilaya ya Hai ardhi ni kama imekwisha. Maeneo mengi yako kwenye vyama vya ushirika. Hebu niombe, tunafahamu kipaumbele kwenye vyama vya ushirika ni kulima zao la kahawa, lakini bado mashamba yale ni rafiki kwenye utalii. Naomba sana Mheshimiwa wa Mipango atembelee Wilaya ya Hai, aone yale mashamba; yanafaa sana kwenye uwekezaji wa hoteli za kitalii ili tubadilishe mfumo wa uchumi wetu kwa sababu hatuna sehemu nyingine ya kwenda kulima. Lazima tutafute *alternative* ya kufanya biashara ambayo itaongeza pato la watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wameliweka hapa zuri kabisa ni kwamba, kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa

mipango. Nimefurahia sana jambo hili. Nidhamu ni nini? Ni pamoja na ile taarifa ya mashirika mlisikia kilichotokea pale, wakuu wa taasisi wale. Ninaomba, ifike mahali hizi kazi tupeane kulingana na uwezo mtu anavyoweza kufanya kazi. Kama wamekiweka hapa kipaumbele hiki, maana yake ndiyo kinaenda kusimamia mipango mingine, tupate watu wenye uwezo mzuri, washindanishwe wasipewe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai ziko nafasi za uteuzi, lakini zile za utendaji mtu aombe, washindanishwe, tupime uwezo wake na awe anafanyiwa *review* kila mwaka kulingana na uwezo wa kazi yake, ndipo mipango hii itaweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya katika nchi yetu na wananchi wa Hai wameniambia niseme ahsante sana kwa Mheshimiwa Rais kwa miradi kedekede aliyoleta ndani ya Jimbo la Hai. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa, wageni waliopo Bungeni mchana huu; mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, mpiga kura wake kutoka Mkoa wa Singida. Karibu. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wageni watano wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Biharamulo na Lweru, kutoka Mkoa wa Kagera. Karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi na walimu 100 wa Shule ya *American and British English Centre* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haji Amour Haji, wajiandae Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kuniona. Awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anavyoiendesha nchi yetu na namna anavyojenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa namna ambavyo nao wanavyofanya kazi zao vizuri sana za kuweza kujenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika upande wa mchakato wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa na kuangalia malengo yake. Nitajikita kuhusiana na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026 na hasa kuangalia dhima yake inayozungumzia suala la kujenga uchumi shindani na viwanda pamoja na maendeleo ya watu. Katika dhima hii ya uchumi, hasa kwenye uchumi wa maendeleo ya watu pamoja na mchakato wake, nitaangalia mambo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, nitaangalia suala la elimu. Maendeleo ya watu ni lazima kwanza kitu cha kwanza tuangalie suala la elimu. Bila ya elimu maana yake hayo maendeleo juu ya watu maana yake itakuwa bado, hatutaweza kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala la elimu ya watu, maana yake ni kuwaondosha katika *mindset* zao na kuzileta katika *mindset* za kimaendeleo. Suala la pili, nitaangalia suala la matarajio ya namna ya watu kuweza kuishi ambalo nalo limo katika mpango ambao upo na jambo la tatu ni pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija na mpango uliowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, ni mpango ambao nitasema kwamba umeakisi haja kubwa sana na nitasema kwamba ni mpango ambao umejitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nije katika ile Falsafa ya Mwalimu Nyerere ambayo alizungumza maneno hasa katika masuala ya maendeleo ya watu. Alizungumza hivi, "Maendeleo ni watu lakini siyo kitu." Maendeleo ni watu siyo vitu. Ili watu waweze kupata maendeleo, lazima watu waweze kujitegemea. Ili watu waweze kupata maendeleo ni lazima watu kupambana na

umaskini. Ili watu waweze kupata maendeleo ni lazima kuondosha ujinga pamoja na maradhi.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo Falsafa ya Mwalimu Nyerere ambayo alizungumza na alikuwa na mantiki kubwa sana alivyokuwa anazungumza maneno hayo, kwamba, maendeleo ni watu, hasa katika kupunguza umaskini, kuondosha ujinga, maradhi na masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, katika huu mpango tulionao, maana yake ni dhahiri kwamba tunajadili suala la kujitegemea. Tunajadili suala la kupambana na umasikini na tunajadili suala la kuondoa ujinga pamoja na maradhi. Hayo ndiyo mambo tunayojadili katika huu mpango. Pamoja na dhima tuliyokuwa nayo ya uchumi shindani pamoja na viwanda, hayo yote yanaakisi maneno ya Mheshimiwa Marehemu Mzee wetu, Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la kujitegemea. Suala la kujitegemea, ukiliangalia hasa ni suala ambalo ni mtambuka sana na ni suala pana, ambapo tukiangalia katika suala la kujitegemea, maana yake tuangalie suala la rasilimali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kama Tanzania, kama ni nchi maana yake tunazo rasilimali za kutosha katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Ukiangalia ardhi tunayo na ndani ya ardhi huko kunapatikana maji, madini na ndani ya ardhi humo tunafanya shughuli zetu zote ambazo hizo kama ni utajiri kama ni nchi maana yake tunayo rasilimali ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika suala la rasilimali watu, maana yake watu ndiyo sisi. Maana yake ni kujaribu tu kuwapa elimu watu wote kuondokana na ujinga na kupata elimu yenye tija kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufika katika hatua ya malengo tunayoyakusudia na maendeleo yenye kuleta tija, kuna mambo ambayo ni lazima tuyaangalie katika hali ya upana mkubwa sana. Suala kubwa la kuweza kuliangalia ni suala la

elimu. Bila kuangalia elimu, maana yake mipango yetu yote tutakuwa hatuwezi tukafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa sana katika maisha yetu na katika mazingira yetu, bila kuwajengea watu mazingira ya elimu na elimu yenyewe, maana yake iwe ni elimu yenye tija, ya ujuzi na ya kujenga maarifa. Tukiwa na elimu ya kujenga ujuzi, tukiwa na elimu yenye kujenga maarifa maana yake hapo tunaweza tukatengeneza mfumo wetu mzuri wa maendeleo yetu ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo limezungumzwa na watu wengi sana, ili mpango wetu uweze kukamilika tuangalie suala la kilimo, kilimo maana yake ukitizama katika hali ya nchi yetu asilimia kubwa ya watu ambao wanaishi katika nchi ya Tanzania maana yake wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mipango yetu maana yake tuangalie sana suala la kilimo, lakini kilimo chenyewe maana yake kilimo kilichokuwa bora, kilimo ambacho chenye kuleta tija. Ili kuweza kuwa na kilimo kilichokuwa bora na kilimo chenye kuleta tija maana yake ni lazima kwamba tuwe na miundombinu ambayo ni mizuri, tuwe na wataalam ambao watakaoweza kuimarisha kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee walikuwa wanatuambia kwamba kilimo ni uti wa mgongo tukiangalia kweli kwamba kilimo ni uti wa mgongo bila kuangalia suala la kilimo kama nchi yetu maana yake watu tutaweza kuwaacha na njaa. Ila tukiweza kulima maana yake tutakuwa tuna uwezo wa kuweza kuondosha njaa, tutaweza kuondosha, tutakuwa tuna uwezo wa kuweza kupata kipato cha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala lingine katika kuondosha maradhi, maana yake ni lazima kwamba tujenge hospitali ambazo zimeshajengwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kila mahali, lakini tatizo letu ni moja. Maana yake tatizo letu ni kwamba tunahitaji kuwa na wataalam ambao watakuwa ni wataalam bobezi, ambao wataweza kutibu

maradhi ambayo yataweza kuwaondosha maradhi watu wetu kama kuondosha umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nije katika suala la tatu hasa lililopo katika mpango wa maendeleo; nije kwenye suala la ufuatiliaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mama Sitta ana dharura, kwa hiyo tunakwenda moja kwa moja kwa Mheshimiwa Luhaga Mpina, jiandae Mheshimiwa Mgalu na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wetu wa mwaka 2025/2026. Kabla sijaanza mchango wangu niruhusu niwapongeze watu wawili; moja ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuunda Tume ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi na hasa baada ya sisi hapa Bungeni kubishana muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini matokeo ya hii tume yataleta mageuzi makubwa sana katika ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili nami kwa kuchukulia umuhimu wa jambo hilo pamoja na kwamba nilikuwa mapumzikoni kule tayari nimeshaandaa kurasa 50 ambazo nitazipeleka kwenye tume ambazo zimezungumzia maeneo mbalimbali ya namna ambavyo nchi yetu inapoteza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa pili, ninataka nimpongeze ni Mheshimiwa Donald Trump, Rais wa Marekani, ninampongeza

kwa ushindi mkubwa na kwa kuaminiwa tena na wananchi wa Marekani hongera zake aendelee kuongoza nchi hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Kisesa kwa kuendelea kunivumilia hata wakati wa juakali lakini wameendelea kuwa pamoja nami, hongereni sana wananchi wangu. Nitahakikisha kwamba kwa nguvu zote na kipaji chote nilichopewa na Mwenyezi Mungu tunatekeleza ile azma yetu ya kwamba hakuna kupumzika mpaka maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa nichangie mpango na nianze kwenye utekelezaji, nipitie kidogo eneo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Taarifa ya Mpango hapa inaonyesha kwamba mradi wetu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao utazalisha *megawatt* 2,115 tayari sasa hivi uzalishaji umefikia *megawatt* 740 na tumefikia 99.21%, lakini hatuambiwi sasa mpango wetu huu unakamilika lini ili kuzipata zile *megawatt* zote 2,115. Tuliwaahidi wananchi kwamba umeme huu ni umeme wa bei nafuu, hatujaambiwa katika mpango huu unafuu wa umeme kwa wananchi kutokana mradi wetu huu mkubwa tuliowaahidi kwamba tutashusha bei za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, umeme wetu tutawauzia majirani zetu, leo hii katika mpango huu nchi ngapi ambazo tayari tumeshaingia nazo mkataba wa kuziuzia umeme na umeme wetu unaenda kushuka bei kwa kiasi gani? Ili wananchi wetu wapate umeme kwa bei nafuu, wawekezaji wetu waweze kufaidi uzalishaji ndani ya eneo ambalo lina uzalishaji wa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la utekelezaji wa Mradi ni *LNG*, mradi huu tunaambiwa tu kwamba mazungumzo yanaendelea sasa miaka imeenda sana mazungumzo yanaendelea na utaratibu wa kawaida kwa mujibu wa Sheria ya *Natural Resource* pamoja na *alterity* zinataka hii mikataba iingie hapa Bungeni. Sasa huko wanapoendelea na mazungumzo wanaendelea kwa muda gani? Kwa sababu miradi hii, kama walivyosema wenzangu inahitajika kutekelezwa kwa haraka ili tuweze kunufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mkataba wa usafirishaji mizigo wa kuchangia makasha kwa wasafirishaji wa mizigo tofauti tofauti yaani *imported loose cab*. Hapa katikati Sheria ya Usafirishaji wa Mizigo hiyo ilibadilika kanuni za usafirishaji wa mizigo hii ilibadilika ikafika mahali kwamba msafirishaji wa mizigo yaani *consolidator* anasafirisha mizigo majina ya nyaraka zote yanaandikwa kwa jina lake yaani *bill of landing, commercial invoices, parking list, declaration form, TPA documents, payment list* zote hizi ziliandikwa kwa majina yao kwenye usafirishaji kule anaposafirisha mzigo, lakini tukapata matatizo makubwa sana ya wafanyabishara wengi kukosa nyaraka za ulipaji wa kodi. Kwa sababu majina kule yameandikwa kwa jina la msafirishaji na hapa anakuja kuuza anasafirisha kwa majina yake na anakuja kulipa kodi yeye na ana-*declare VAT input tax* yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku wananchi wetu wanashindwa kuuza bidhaa kwa kutoa risiti, wananchi wetu wanakuwa hawana nyaraka zozote za kufanya malipo ya kodi na wananchi wetu na wafanyabiashara wetu wakashindwa hata kutumia *EFD* na wananchi wetu wakawa na matatizo makubwa sana, migomo ilitokea mingi sana kule Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumanne, tarehe 5 Novemba, 2024 hapa Serikali imekuja kusema sasa wafanyabiashara, nyaraka zao zitaandikwa kwa majina yao, lakini hapa tumepotezewa fedha nyingi sana; sasa kwa sababu tumepoteza fedha nyingi hizi fedha zetu tunazi-*recover* vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nami nashauri kwa sababu ili kampuni la *OPPO Agency Company Limited* kwa muda wa miaka mitano limefanya hii *business* na kuna wafanyabiashara wengi ambao wamei-*load* mizigo, lakini inapofika huku kwenye ku-*clear* mizigo nyaraka zao za usafirishaji wa mizigo hazionekani, kwa maana ya kwamba mizigo hiyo haikuingizwa ili kukwepa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufanyike ukaguzi wa kiuchunguzi yaani *forensic auditing* ya muda wa miaka mitano kulichunguza kampuni la *Oppo Agencies Limited* katika kipindi hicho cha miaka mitano na kubaini kodi iliyopotea na kama

tutabaini kodi iliyopotea, kampuni iilipe Serikali hiyo hasara itakayokuwa imetengenezwa ndani ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine hapa ni suala la Mkataba wa *DP World*, suala la mkataba wa *DP World* tumeambiwa vizuri hapa, lakini nataka kusema tulikubaliana kwamba Mikataba ya *HGAs* iletwe hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri hapa anaeleza mwekezaji wa *DP World* atawekeza dola za Marekani milioni 250 sawasawa na bilioni 687 kama sikosei bilioni kwa miaka mitano.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mwekezaji huyo ameshaenda anakusanya kodi sasa na huo uwekezaji wake atawekeza kwa muda wa miaka mitano*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana hapa Bungeni kwamba mikataba hii ya *HGAs* yote mitatu italetwa kwenye hili Bunge ili tuweze kujua nini kilichokubalika ndani ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi Sheria yetu ya *Natural Resources* inasema kifungu 12 kwamba mikataba yote ya rasilimali lazima iletwe hapa Bungeni. Ninaendelea kuuliza hivi imeshindikana nini kuletwa mikataba ya Bandari ya Dar es Salaam tuliyoingia mkataba na *DP World* hapa Bungeni. Nani aliyeenda kukubali kwamba sisi tunakubali uwekezaji wa bilioni 687, nani aliyekubali kwamba sisi tumekubali *ratio* ya kugawana mapato na *DP World* kwa *ratio* ya 40 kwa 60 nani aliyekubali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mkataba....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina kengele ya pili.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo dakika moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, kengele ya pili. Mheshimiwa Mgalu, Mheshimiwa Ng'enda na Mheshimiwa Ally Jumbe jiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kutoa mchango wangu kwenye majadiliano yanayoendelea. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Pili kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ninaunga mkono maoni yetu yote ambayo yaliwasilishwa na kwa umahiri na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Oran Njeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mipango Profesa Mkumbo, kwa kazi nzuri pamoja na watendaji wao wote na namna ambavyo alitupa ushirikiano wa karibu sana kwenye Kamati yetu ya Bajeti wakati tunafanya majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Profesa Mkumbo katika Taarifa yake amewasilisha Mpango wa Maendeleo 2025/2026, lakini ninataka niungane naye kwa namna ambavyo ameelezea kwa ufasaha mafanikio yaliyopatikana ndani ya miezi sita baada ya Serikali kukabidhi shughuli za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa Kampuni ya *DP World* Dar es Salaam. Kwa nini ninaungana naye ni kwa namna ambavyo kama yeye mwenyewe anavyosema, ni namna Mheshimiwa Rais wetu alivyokuwa shupavu, jasiri, mstaamilivu na sote ni mashuhuda wa namna hata Bunge hili lilidharauliwa baada ya kupitisha ule mkataba hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeze Mheshimiwa Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia, ninakupongeza na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ambavyo mmetuongoza katika mjadala ule lakini nadhani katika yale maneno yanayosemwa kwamba wanaokutukana siku moja watakusalimia kwa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaamini wale ambao walikuwa wamempinga tena kwa lugha ya kebehi watamsalimia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan wa heshima kubwa, baada ya kuona mafanikio haya tu ya muda mfupi na tuna imani yale ambayo faida zote zilizoelezwa za mkataba huu wa *DP World* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya uendeshaji wa Bandari Dar es Salaam na siyo bandari zote, siyo mkataba wa milele yote hayo yamejidhihirisha, ni kweli kwenye ukweli uongo hujitenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda kuipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya namna ambavyo imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati, lakini kwenye mradi huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa kuwa natoka kwenye Mkoa wa Pwani ambapo mradi huu unajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze kwa dhati Serikali kwa kuingiza *megawatt* 750, lakini nina shukrani za maeneo ya visiwa ambayo hatukuwahi kudhani kama utapelekwa umeme wa gridi ya Taifa, nina shukrani za kutoka visiwa vya Wilaya ya Kibiti, Mbuchi, Maparoni, Kiongoroni na Visiwa vya Wilaya ya Mafia umefika umeme wa *Grid* ya Taifa kwa mara ya kwanza jambo ambalo limekuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umepitishwa kwenye majaruba ya maji, kwenye bahari, kwenye maingiliano ya *delta* na Bahari ya Hindi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa historia hii, lakini pia na kwa miundombinu. Sasa hivi visiwa hivyo vinafikika na miundombinu ya barabara yamejengwa madaraja ambayo hayakuwahi kufikiriwa ndani ya miaka 60 ya uhuru. Ni wazi kwamba kazi nzuri imefanywa, lakini kwa kuwa kazi hizo zinafanyika kutokana na makusanyo ya mapato, tunajadili mapendekezo hapa ambayo natarajiwa kukusanya trilioni 55. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati pia tumefanya tathmini ya utekelezaji wa robo ya kwanza ya bajeti ya mwaka huu 2024/2025. Hapa ninataka niipongeze kwa dhati *TRA* kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa, nimpongeze Kamishna mpya wa

Mamlaka ya Mapato Tanzania Yusuph Mwenda, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo tumeona kasi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha robo ya kwanza wamekusanya zaidi ya trilioni 7.7 na 105%, lakini hatua zinazochukuliwa na Mamlaka ya Mapato sasa hivi tumemwona Kamishna akifanya ziara mikoa mbalimbali, akikutana na wafanyabiashara, wafanyakazi na wadau mbalimbali. Amefanya ziara kwenye maeneo ya mipaka yetu, amefanya ziara kwenye maeneo ya bandari zetu, amefanya kikao na *TIC* pamoja na wawekezaji wa nje waliokuwepo hapa nchini. Hatua zote zinaonekana lengo lake ni kuongeza ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika hili ni kuomba Serikali kwenye bajeti inayokuja 2025/2026 kuona namna ya kuwezesha Mamlaka ya Mapato. Wanajenga mifumo ya ukusanyaji mapato mfano mfumo wa *IGAS*, mfumo wa *TANSIS* na mifumo mbalimbali, lakini changamoto kubwa ni namna ya uwezeshaji ili kukamilisha mifumo hii. Niombe Serikali ile bajeti ya bilioni 400 ambayo wamekuwa wakitoa kidogo kidogo kwa ajili ya mamlaka hii ya mapato ikamilishe ile mifumo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia iwezeshe vitendea kazi magari ya kupambana na wakwepa kodi zile *scanner* katika maeneo ya mipaka yetu kwa mfano Kamati ya Bajeti tulitembelea Namanga, tumewahi kutembelea sisi mabalozi wa kwetu tumetembelea Holili, tumetembelea Tarakea, lakini pia kupitia ziara ya Kamati ya Bajeti imetembelea Buhigwe tumeona Mkoa wa Kigoma kule mipakani. Kwa hiyo, Serikali ina uwezo kukusanya mapato mengi zaidi kama itaiwezesha *TRA*. Ombi langu katika hili kwa kuwa kila kitu trilioni 55 tunatarajia, trilioni 38 zitokane na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya trilioni 38 hizo ambazo ni zaidi ya 70% zaidi ya trilioni 31 zitakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameonyesha ushujaa na

ushupavu na matarajio ya kuwezesha *TRA*, ameongeza wafanyakazi kwa mara ya kwanza zaidi ya 1,200 mwaka wa fedha 2023/2024 uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuwa akiwezesha hatua ya kuunda kikosi kazi cha kupitia mifumo ya kodi, ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha wanakusanya kodi kwa haki bila upendeleo na wote tunalipa kodi, lakini na wale ambao wana vitendo vya kukwepa kodi wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia uimarishaji wa Taasisi za *TRAB* na *TRAT* ili kuwezesha wanasikiliza masuala mbalimbali ya kodi lakini pia hata Ofisi ya Msuluhishi wa Kodi iwezeshwe ili kwa pamoja jitihada zote zichangie upatikanaji wa trilioni 55 zinazotarajiwa, lakini hata sasa trilioni hizi 49. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii lakini kiukweli Awamu hii ya Sita, ameupiga mwingi kwenye kukusanya mapato.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana kengele ya pili, Mheshimiwa Kengele ya pili ahsante.

Mheshimiwa Kilumbe, jiandae Mheshimiwa Ally Jumbe, tuanze na hawa wawili kwanza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kunipa nafasi nami ya kutoa mchango wangu katika kujadili suala la mpango. Kabla ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa afya na uhai na zaidi ya yote nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa kutuonyesha njia ya sisi kutoa michango yetu mizuri kutokana na wasilisho zuri walilofanya pamoja na Wenyeviti wa Kamati walioweka michango mzuri katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuanza na maneno yanayosema kujitawala ni kujitegemea. Taifa lolote ambalo ni tegemezi Taifa hilo linapunguza hadhi na heshima ya uhuru wake. Kwa hiyo, nataka pamoja na yote tunayozungumza tumerudisha Tume ya Mipango kwa sababu tumeona ipo haja ya kufanya hivyo. Kwanza kwa ajili ya kuweka mipango kwa maslahi ya Taifa, lakini pili kuweka vipaumbele vya utekelezaji wa mipango hiyo. Pamoja na kuyafanya yote hayo lazima tuwekee *ringfence* hili jambo lenyewe la Tume ya Mipango kwamba mipango yetu tukishaipanga tuiheshimu tusiwe na tabia ya kwenda mbele rudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mwingine ukiulizwa unasema hapa tunahitaji *political will,* mpango ndiyo *political will* yenyewe tulishaweka mpango tuuheshimu tuufuate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi nyingine mipango mikubwa inakuwa ni sehemu ya Dira ya Taifa na inakaa kwenye Katiba ya Nchi ili mtu yeyote anayekuja, kiongozi yeyote wa nchi anayekuja anaiheshimu, anaifuata kwa sababu haya ni masuala ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo la kusema mipango yetu iheshimiwe, jambo lingine ambalo ninataka niliseme ni kwamba, katika kujitawala ni kujitegemea. Mipango yetu ijielekeze katika kupunguza utegemezi wa Taifa letu na ili kufikia dhamira hiyo ya kupunguza utegemezi, yapo mambo ya msingi ya kuyasukuma na kuyapa kipaumbele katika mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, nimepata bahati ya kujifunza sana mambo mengi kwenye Sekta ya Nishati, lakini leo hii tunapozungumza mipango yetu ningezungumza kwa

nchi yetu, Mpango wa kwanza ambao ungekuwa kipaumbele kwa Taifa letu, ni kuzalisha gesi asilia kwa wingi na kuisambaza katika nchi yetu yote, ili gesi hii itusaidie kupunguza gharama za kuhitaji mafuta ya nishati kutoka nje ambayo yana msalaba wa kutafuta kitu kinaitwa dola kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo yapo magari yanatumia gesi, yanapanga foleni kutwa nzima kutafuta gesi ambayo inazalishwa nchini haihitaji dola. Kwa hiyo, tukiongeza uzalishaji, na tena sasa hivi nimetembelea kule Madimba wala siyo suala la kuongeza uzalishaji maana wamepunguza uzalishaji kwa 60% kwa sababu mteja wao mkubwa alikuwa ni *TANESCO* na *TANESCO* wamepunguza kuchukua gesi baada ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kuanza kufanya kazi. Kwa hiyo, kuna gesi nyingi ambayo bado haijatumika imezuiliwa kuzalishwa kwa sababu haina mtumiaji. Tuongeze matumizi ya gesi haya yatatutoa kwenye utegemezi, utumwa wa kutafuta dola, utumwa wa kupatana na wenye kampuni za mafuta kuwanyenyekea utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni chuma, tuvune chuma ili miradi yote ambayo inahitaji chuma tupate chuma kutoka nchini. Hadithi ya Liganga imekuwa ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; lakini siyo tu kuongeza maana hata viwanda ambavyo tulitaka vitusaidie katika kukuza uchumi, tumechukua viwanda vingi ambavyo sivyo vinavyo-*add value* ya mazao ya wakulima, wavuvi na wafugaji, yaani viwanda tulivyovihitaji ni viwanda ambavyo vinaongeza thamani ya mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo hii kuna mzalendo mmoja pale *SIDO* Kigoma ameweka Kiwanda cha Kukamua Mafuta ya Mawese na kuya-*refine* kutoa hiyo *Korie*. Kiwanda kiko pale lakini uzalishaji wa michikichi umekuwa ni mdogo mpaka analazimika kuchukua mafuta kutoka Malaysia ili aje hapo ayasafishe ndiyo auze, kwa hiyo, lazima tuongeze kasi. Mpango wetu lazima useme, tunataka kuondokana na suala la kuagiza mafuta kutoka nje ni nguvu gani tutaiweka kwenye kilimo cha michikichi ili kuondokana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanya kazi kubwa kweli ya kusukuma michikichi lakini siioni nguvu kubwa ya Serikali kuweka pesa kwenye kilimo cha michikichi, kuwawezesha wananchi walime vizuri, walime ya kutosha ili tuweze kuzalisha mafuta kwa wingi. Kwa hiyo, niwaombe sana lazima tujielekeze katika jambo hili kwa nguvu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninasema Serikali yetu inafanya kazi kubwa na nzuri na hakuna habari ya kurudi nyuma katika mambo tuliyofanikiwa. Mambo tuliyofanikiwa ni pamoja na kuboresha bandari zetu, tumeshawapa kazi *DP World* waendelee kufanya kazi na sisi tunategemea mavuno makubwa kuliko hata huko nyuma tulikokua. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Jumbe, Mheshimiwa Maganga jiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba nami nitumie fursa hii kwa leo kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na hasa kwa mambo mawili. Jambo la kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na jinsi anavyojitoa kwa ajili ya Watanzania na anavyotumia utashi wake kuhakikisha anatufikia wananchi wote na hata wale walioko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Serikali hasa Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao ni wasikivu, wanatusikiliza na ni wanyenyekevu. Hii ni silaha kubwa ya maendeleo na ninafikiri hata Mheshimiwa Rais alijua kwamba akitumia silaha hii ataweza kufanikiwa na ni kweli amefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie juu ya huu Mpango, lakini nitajikita kidogo kwenye ukuaji wa pato la Taifa na katika hili ninaomba nisisitize kwamba, ninaomba twende kwa tahadhari na tahadhari hiyo ikae hasa kwenye deni letu la Taifa. Ninaomba sana Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha hebu

twende tupunguze *GDP to Debit Ratio* angalau tufike 3%0, itatusaidia sana, lakini ninaomba nishauri tutafikaje hapo, ili tufike hapo ninaomba kwa unyenyekevu hebu suala la kuongeza *National Mineral Reserve* litiliwe mkazo. Tukiitunza dhahabu yetu ikawa kwenye benki yetu, Benki Kuu tutakuwa tunaongeza pato na tutaweza kuhakikisha kwamba thamani yetu inakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mfumo wa *EFD* umetushinda, hatutaweza kukusanya pesa kwa mfumo wa *EFD* kupata *VAT*, ili tuondokane na hilo, ningeomba tutumie mifumo ya kisasa hasa kwa kutumia mfumo wa kwenda kwenye Bohari zetu kule ambako wanatunza mizigo. Tutumie hata kodi zetu kuhakikisha tunapohesabu mzigo, mtu wetu ambaye ni mfanyabiashara anapoleta mzigo kule ndiko tutumie kuhesabu badala ya kuhesabu kwa watu wanaonunua, ninafikiri Mheshimiwa Tarimba alilielezea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumeendeleza sana maziwa yetu, lakini ninataka nitoe tahadhari, inawezekana hata maendelezo yaliyopo kwenye Ziwa Nyasa tunayapigia hesabu kwamba yataleta manufaa. Ninaomba nitoe tahadhari ifuatayo; Mheshimiwa Rais ametujengea meli tatu Ziwa Nyasa, meli kubwa ya abiria inaitwa *MV-Mbeya Two*. *MV-Mbeya Two* mkiipigia hesabu ninaomba niwahakikishie tutakuwa tunafanya makosa kwa sababu ile meli haifanyi kazi ipasavyo na haina uwezo wa kufanya kazi kwa sababu haijajengwa kukidhi mazingira ya Ziwa Nyasa. Sasa ningeomba tufanye uchunguzi wa kutosha ili tujenge meli ambayo inafanana na mazingira ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunajenga bandari kubwa sana pale *Mbamba Bay*. Ninaomba nitoe tahadhari, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 81 hii ni *investment* kubwa sana na katika *investment* ambayo tumepata Ziwa Nyasa hii ni ya kwanza. Sasa tunapopiga hesabu za mzigo, tunapiga hesabu za kutoa mzigo moja kwa moja *Mbamba Bay* kwenda Malawi na Zambia kwa kupitia *Mbamba Bay* kwenda Nkhotakota kwenda *Nkata Bay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe tahadhari, ninaomba utafiti ufanyike na tuangalie njia mbadala. Tayari tuna matatizo ya mpaka wa Malawi na Tanzania kwenye Ziwa Nyasa, bado hatuja-*solve* hili tatizo. Ni lazima tuwe na tahadhari na hili halijafika popote. Tunapopiga hesabu za kwenda wakati huku tuna matatizo, ningeomba tujihadhari sana, Mpaka wa Malawi na Tanzania bado ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Bandari za Malawi zinaendeshwa na Wareno. Wareno wanaendesha Beira, Beira ni mshindani wetu kwa Bandari ya Mtwara, hawatatuhusu tupeleke mzigo wetu moja kwa moja kwenye bandari zao na bandari zile wanaweza wakatu-*charge* fedha nyingi na mfano umetokea. Tukitaka kupeleka meli yetu ya abiria tu fedha wanazo-*charge* ni kubwa. Kwa hiyo, ningeomba tuangalie *alternative*. Tuimarishe Bandari ya Itungi, tuimarishe Bandari ya Kiwira na sambamba na barabara inayotoka Katumba Songwe kwenda Ileje ili tuweze kupeleka mzigo Malawi na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni ushauri tu, kwamba kwa sasa hivi Zambia wana *crisis* ya umeme na nina uhakika na Malawi watapata *crisis* ya umeme, Je sisi tumejiandaaje kupeleka umeme Zambia? Pale *Kiwira Coral Mine* kuna makaa ya mawe, naomba sana hebu twende tukafanye *investment* pale, umeme ule tuwauzie Wazambia Kariba inakauka. Kwa hiyo, ningeomba sana wanapofanya mipango, hebu tufanye hii ni mipango ya Serikali kuimarisha *Kiwira Coral Mine* ili tuuze umeme Zambia na Malawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Songwe; tumezungumza muda mrefu sana kuna Bonde la Mto Songwe na kamisheni iko pale sasa hivi ina umri zaidi wa miaka 20. Ninaomba sana hebu tuimarishe italeta manufaa kwa wananchi wa Kyela na Wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa sababu kutakuwa na skimu za umwagiliaji ambazo ni zaidi ya hekta 3500, ninaomba sana tulifanyie kazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kinachotufanya mpaka sasa hivi tuhangaike na kinachokula fedha ya Taifa ni matumizi ya

*diesel* au mafuta. Ninashangaa mpaka leo tunapozungumza mipango, nilidhani kitu cha kwanza sasa hivi tuelekee kwenye umeme na gesi na ambapo tungeanzia, tuanzie kwenye *BRT* pale Dar es Salaam. Miundombinu yetu, basi zetu na vifaa vyetu vya usafiri viende kwenye gesi na umeme. Tusisubiri kutumia *diesel* tena, lakini miundombinu yetu hebu tuiangalie. Kwa nini bado tunaendelea kujenga miundombinu ambayo itaisha thamani sasa hivi? Kwa mfano, pale *BRT…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi mchana wa leo ili niweze kuchangia hoja iliyoko mezani, Mpango wa Mwaka 2025/2026. Awali ya yote nipende kumshukuru Mungu muumba wa mbingu na nchi kwa kuweza kupata fursa na nafasi hii ya kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa huu Mpango uliouleta hapa Bungeni tuujadili, lakini yapo maeneo tunapenda tuishauri Serikali. Kwa kuwa sisi Wabunge tunaishi na watu na tunajua maisha ya watu jinsi wanavyopata taabu na ninaomba unisikilize sana hapa Mheshimiwa Waziri. Unaweza ukatupeleka sana kwenye mipango ya juu sana ukaacha yale maisha yetu ya kiuhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lipo suala la maboma hapa nchini. Nikizungumzia maboma tunaweza tukasema kila Mbunge ana kilio huko kijijini. Kwa hiyo, kwenye huu mpango ninaomba hili suala lipewe kipaumbele ili nguvu za wananchi walizozifanya zikaweze kuokoka au wanufaike na rasilimali zao ambazo wao wenyewe walichanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu; Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninakumbuka mwaka 2022/2023 tulizungumza hapa Bungeni na wewe ukanikubalia kwamba nilete mpango wangu na nikaleta. Niliandika barua kwa kuomba kwamba kila halmashauri tuweze kununua vifaa vya ujenzi. Hii shida mpaka sasa hivi inatusumbua sana majimboni. Tunajua tumepitisha trilioni kwa ajili ya ujenzi wa Barabara, lakini haviji kwa wakati muafaka. Tukiangalia sasa hivi huu ni mwezi Novemba, tunaelekea mwezi Desemba kwenye masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa na vifaa kila halmashauri au kila mkoa kama tulivyoshauri kwenye Sekta ya Maji tusingekuwa tunasubiriana. Sasa hivi mifumo ni mingi ya kisomi na kitapeli wala *NeST* haitoki, pesa hazitoki wakandarasi hawalipwi. Kwa hiyo tunakwama tunakuwa na mambo mengi lakini utekelezaji ni hewa. Kwa hiyo, ninaomba kwa mpango huu mwaka 2025/2026, Mheshimiwa Waziri unikubalie, nitaleta tena mpango wangu wa kutaka kununua vifaa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hasa kwenye jimbo langu kwa sababu tukiwa na vifaa halafu sisi wenyewe ni mafundi wa kutengeneza hivyo vifaa hakuna shida ya kuweza kutengeneza miundombinu yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, wakandarasi wanaofanya kazi hasa wa ndani simu na meseji ni nyingi sana kwa kila Mbunge. Wamefanya kazi na bado wanaidai Serikali, ili sasa Serikali iweze kusifiwa na kupewa sifa za kweli ni vyema wakandarasi wa ndani waweze kulipwa kazi walizozifanya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la ajira, nchi yetu imebahatika kuwa na wasomi wengi sana. Mheshimiwa Waziri, nimeangalia kwenye mpango wako sijaona dhamira kubwa ya kuweza kuwasaidia wasomi ambao wamesoma wana vyeti, wameshaweka vyeti vyao ndani na kila ajira mkitangaza, kila nafasi zikitoka wana-*apply* lakini mwisho wa siku wanafanya *interview* hawaajiriwi. Kwa hiyo, kwenye huu Mpango ninaomba mjaribu kulipa kipaumbele hili suala ili kusudi watu waweze kuajiriwa kwa sababu walitumia pesa nyingi kuweza kusomesha watoto wao pamoja na mambo mengine na wengine walifilisika

kabisa wakiwa wanasomesha shule za *international* na mpaka sasa watoto wao hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la watu waliyoitumikia Serikali, mafao. Tunao wanajeshi, tunao wazazi wetu ambao wameitumikia Serikali ila hawalipwi mafao yao kwa wakati. Ninaomba kupitia mpango huu hao watu wakaweze kupewa kipaumbele. Wengine wapo wamemaliza wana miaka miwili, mitatu, mitano, wengine miaka kumi lakini hawajalipwa. Kila siku wanaambiwa nenda ukalete vielelezo hivi, uliajiriwa lini? Ulizaliwa wapi? Maswali yanakuwa mengi mwishowe wanaona Serikali kama vile imewatelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ushauri wangu mwingine hapa, ninapenda niishauri sana Serikali yangu ya Awamu ya Sita. Kwa kuwa sisi ni washauri wakuu wa Serikali, hasa tunapopata nafasi kusimama hapa Bungeni, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na wataalam wote ambao wanahusika kutusikiliza kama Wabunge, watusikilize, ipo shida ambayo hata mwaka jana ilinipata kwenye jimbo langu. Mvua zilinyesha nyumba zikaanguka, wapo walioporomokewa na nyumba, hata juzi hali hii imetokea Jimboni kwangu kule Masumbwe, watu wameumizwa na majumba, lakini kwenye bajeti zetu huwa tunapitisha bajeti ya maafa na huo Mfuko huwa unakaa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, lakini ukweli ni kwamba hao watu huwa hawapati huduma kwa wakati muafaka. Ninaiomba Serikali iweze kuangalia fungu hilo ili waathirika wa mafuriko wanapopata mafuriko, pale mafuriko tu yanapotokea Serikali iweze kuwasaidia watu hawa ili waweze kunufaika na Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda nishauri hapa kwa siku ya leo, ni suala la askari wetu ambao wanatulinda kila mji hawana nyumba za kuishi kabisa, lakini hata ofisi sisi kama wananchi tunajitahidi kuwawekea makao ili waweze kuendelea kufanya kazi zao za kipolisi. Kwenye Mpango huu wa 2025/2026 ninaomba hili suala na lenyewe liweze kupewa kipaumbele ili askari hawa nao waweze kufanya kazi kwa morali na mambo mengine ili yaweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo sula lingine la hii mitandao ya mawasiliano. Kwenye Jimbo langu nina uhitaji wa mitandao mitano. Zipo kata ambazo hazina mawasiliano kabisa, wananchi wangu wanateseka sana. Ninaomba Serikali iweze kuliangalia, Waziri wa Mawasiliano uweze kulipa kipaumbele na uweze kuboresha kwenye eneo hilo kwa upande wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu ulimwengu huu wa kidigiti, tunapoteza pesa nyingi kwenye hizi *electronic machine*, hata juzi tumeona hapa wakati tunapitia Ripoti za CAG, vitu vingi vinapotelea kwenye *POS* na hili suala ni vyema tukawa tunaenda upande upande huku tunatumia *manual* huku tunatumia *electronic* ili kuhakikisha fedha zinazokusanywa na Serikali kuanzia kwa yule mwananchi wa kawaida awe anafahamu kwamba amekusanya shilingi ngapi na zimeenda kufanya nini. Ni vyema kila mwananchi akawa na uelewa na mambo haya kuliko kuambizana tu mifumo ya kifedha imebadilika halafu fedha haziji. Wakati mwingine wananchi wanachangia michango yao kwa ajili ya ku-*support* Serikali, lakini pale zinapoingia kwenye akaunti hapo ndiyo mifumo inaanza ku-*scratch* na kuleta matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala linatunyima heshima na sisi kama wawakilishi wa wananchi kwa kweli linatupa taabu sana na hatupendi yaje yatutokee yale yaliyotokea Kenya kwa sababu ilifika sehemu Wakenya wakaona Bunge lao haliwasaidii wakaamua kabisa kufanya fujo na kuwafanyia vurugu Wabunge wao. Sasa sisi hatupendi hili suala liweze kuja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ninapenda niwashukuru tena wananchi wangu wote kwa kuendelea kuniamini na ninasema nitakuwa ninasimama kama Balozi wao ama kama Mwanasheria wao mkubwa na niwatoe wasiwasi hakuna jambo litaharibika. Kulingana na hali hii ni mwaka wa nne nipo hapa nitazidi kufanya kazi kwa hali na mali kwa sababu nimeshayazoea sasa maisha ya hapa, suti zinanienea vizuri na kazi tunafanya na Serikali wananielewa pale ninapowaomba wananisaidia. Kwa hiyo, wazidi kunipa ushirikiano na tuweze kulisongesha Taifa letu kuhakikisha tunatoka hapa tulipo tunaenda sehemu nyingine nchi ya ahadi ambayo tuliahidiwa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunalotaka tuliombe hapa kwenye upande wa maendeleo ya Taifa letu kwenye huu Mpango, nimwombe Mheshimiwa Waziri, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, mengine nitaleta kwa maandishi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninasimama kwa Kanuni ya 70(3) ambayo inasema Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka kuhusu utaratibu baada ya kuruhusiwa na Spika kudai kwamba Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uwongo kuhusu jambo ama suala alilokuwa analisema Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kusimama, pamoja na kuheshimu michango ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mpina, Mbunge wa Kisesa, lakini ninalazimika kusimama kuweka kumbukumbu sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mbunge wa Kisesa anaongea pamoja na mambo mengine aliyoyaongea alisema *DP World* imeshaanza kukusanya kodi. Mimi ndiye Waziri wa

Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania inayohusika na kukusanya kodi iko chini ya Wizari yangu. Ninalithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna kodi yoyote inaruhusiwa kukusanywa na taasisi yoyote isiyo ya Serikali na ambayo haijapewa dhamana hiyo, na kwa mantiki ya alilokuwa analiongelea la *DP World*, hakuna kodi yoyote wanakusanya. Kodi zote ambazo zote zinakusanywa bandarini zikiwepo *Import Duty, Exercise Duty, VAT,* Kodi ya Reli na *Custom Processing Free* zote zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi baada ya *DP World* kuanza shughuli zile ambazo zimeongeza ufanisi bandarini, kodi inayokusanywa na *TRA* imeongezeka na kufikia shilingi trilioni 1.23, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tangu *TRA* ianzishwe, hata *wharfage* zinakusanywa na *TPA*. Kwa maana hiyo, kauli aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge wa Kisesa kwamba *DP World* imeanza kukusanya kodi ni ya uwongo na imelenga kulipotosha Bunge na Watanzania na kama hajafanya kwa makusudi, ninaomba afute hiyo kauli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Fedha amesimama kwa Kanuni ya 70(3) na maelezo aliyosema ni sahihi yapo kwenye Kanuni zetu na ametumia tena Kanuni ya 5 kudai mhusika ambaye ni Mheshimiwa Mpina afute kauli yake au alete vielelezo.

Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninachangia kama nilitumia neno kodi nikimaanisha tozo zinazokusanywa na *DP World* sasa baada ya kuwa imekabidhiwa tangu Aprili, 2024. Kwa hiyo, kama nimetumia neno kodi au kukusanya, ninalifuta kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, nilimaanisha tozo ambazo sasa hivi wanakusanya *DP World*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, kaa chini.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwanza hongera kwa kuweza kuchambua vitu kama hivyo ambavyo vinapeleka taswira na

taarifa mbaya na taarifa za uwongo kwa wananchi kubeba taarifa ambazo kwa kweli wala siyo za kweli. Mheshimiwa Mpina, umefuta kauli yako na sasa namwomba Katibu Mezani na maelekezo kwa *Hansard*, taarifa ya Mheshimiwa Mpina ya kuwa *DP World* inakusanya kodi iondolewe katika Kumbukumbu Rasmi zetu za Bunge. Tunataka Mawaziri wa namna hii, kukiwa na jambo linaleta ukakasi, unasimama na unalisemea ukweli. Hilo limekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Ole-Sendeka, baada ya hapo, Naibu Mawaziri na Mawaziri mjiandae kujibu na kupokea ushauri wa Bunge.

Ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumerudi kipindi cha jioni. Tunaanza na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri Judith Kapinga, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi na Mheshimiwa Mollel, jiandaeni.

Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mchana wa leo taarifa zote mbili. Pia, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai hadi siku ya leo. Pia, kwa namna ya kipekee niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili Profesa Kitila Mkumbo na Daktari Mwigulu Lameck, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wasaidizi wao kwa taarifa nzuri ambayo imewasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia, kutoa pole zangu za dhati na za wananchi wa Simanjiro kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa Tatu wa nchi yetu, Afande Jenerali David Musuguri. Pia, kwa namna ya kipekee nieleze bayana kwamba, Taifa letu limempoteza kiongozi maarufu, mashuhuri, aliyejitoa, kwa ajili ya uhai wa Taifa lake na kusaidia kuliunda Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, lakini pia, aliyetoa mchango mkubwa katika vita vya kumwondoa *fascist* Iddi Amin Dadaa katika ardhi ya Tanzania. Kwa hiyo, kwa minajili hiyo nitumie nafasi hii kuendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema na ampe pumziko lililo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, baada ya ripoti na taarifa iliyotolewa na Waziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, amebainisha bayana juu ya sifa za aina ya miradi itakayopewa kipaumbele katika Mpango wetu wa Maendeleo wa 2025/2026. Pia, niseme dhahiri kabisa naungana naye kwamba, sifa za miradi hiyo ambayo ameitaja bayana kuwa, ni

miradi ambayo itachochea ukuaji endelevu wa uchumi, miradi itakayozalisha ajira kwa ajili ya wananchi wetu, miradi itakayochochea kupunguza umaskini wa watu, miradi itakayoongeza uwezo wetu wa kiushindani na mwisho miradi itakayoimarisha utawala bora na utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia suala hili la utawala bora na utawala wa Sheria, ziko sifa ambazo hazibishaniwi miongoni mwa sifa nyingi alizonazo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kiongozi aliyeonesha uungwana wa hali ya juu na aliyeonesha kuwa ni kiongozi wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ushahidi wake pamoja na mengi ni maamuzi aliyoyaonesha hivi karibuni, ambayo amesikia kilio cha wafugaji wa nchi hii na kuweza kuwaagiza Mawaziri wake wote wawili, Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Profesa Paramagamba Kabudi, kwenda kumaliza suala la tatizo lililokuwepo Ngorongoro. Vilevile, kumtuma Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alipokuja katika ziara ya Mikoa ya Kaskazini kutoa tamko juu ya usalama wa ardhi ya wafugaji kwamba, haitabadilishwa matumizi kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, kwa niaba ya wafugaji wa nchi hii na kwa niaba ya wafugaji na wananchi wa Simanjiro, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uungwana wake na vitendo vyake vya haki. Liko jambo moja ambalo ningetaka tena kushajihisha maneno haya niliyoyasema kwa kueleza uzoefu uliojidhihirisha katika siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashahidi kwamba, Mwaka 2023 Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Rais, Haki Jinai, katika kuendeleza misingi ya utawala bora katika nchi yetu na taarifa hiyo ya Tume ya Haki Jinai ilikuja kupokelewa na yeye mwenyewe. Pia, baadaye akaiunda tena na kuiboresha tume hiyo kwa kuwapa magwiji wawili, Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba na Mheshimiwa Mkuchika, kuungana na timu hiyo, ili kuja na mapendekezo ya utekelezaji wa Taarifa ya Tume ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri katika kufanya hivyo, Mheshimiwa Rais, alisema yeye mwenyewe kwa kauli yake kwamba, amesukumwa na mambo mawili makubwa katika suala zima la kusimamia misingi ya utawala bora, kwamba, amesukumwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 na pia, amesukumwa na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Hata hivyo, ninaongeza la tatu na hili liko bayana kwamba, sababu nyingine ya tatu ni kwa sababu, unaweza kuwa na ilani nzuri ya uchaguzi, unaweza kuwa na katiba nzuri ya nchi, lakini kama hakuna utashi wa kisiasa, hakuna litakaloweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, sababu ya tatu ni Mheshimiwa Rais mwenyewe amesukumwa na utashi wake wa kisiasa wa kuwatendea haki Watanzania na ndio maana akaamua kuunda Tume hiyo ya Hakijinai. Vilevile akaamua kuunda Kamati ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Hakijinai, wakati huo huo akafanya semina kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Bunge lako Tukufu pia, lilikuwa ni miongoni mwa watu waliopata semina ya taarifa hiyo ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ibara ya 5(1) ya Katiba yetu, inasema, "Shughuli zote za utendaji wa shughuli za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais", hakuna mashaka kwamba, mtumishi yeyote wa umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapofanya shughuli za utendaji, anafanya kazi hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Rais. Hata hivyo, kitendo kilichotokea hivi karibuni katika Mkoa wangu wa Manyara ni kitendo ambacho kinaonesha kwamba, baadhi ya viongozi wetu hawawezi kutii na kuheshimu maelezo ambayo wanapewa na uongozi wa juu wa nchi yetu. Sikutarajia baada ya kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tu wananchi wapatao saba, ambao ni viongozi katika Wilaya ya Simanjiro waliwekwa ndani kwa siku saba bila dhamana. Watu hawa ni viongozi wanne kutoka Kata ya Kitwai, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata hiyo, pamoja na viongozi wengine wa mila na madiwani

wawili wastaafu. Vilevile, viongozi wa Kata ya Langai wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Langai Mheshimiwa Jackson Sipitieck, pamoja na viongozi wawili wa mila na kiongozi mmoja wa chama, waliwekwa ndani mahabusu kwa siku saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya mawasiliano na Waziri wa Mambo ya Ndani, namshukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Masauni na nikafanya mawasiliano na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa na wote walipokea simu, hadi usiku wa manane. Hata hivyo, mwishoni waliniambia kwamba, wanafungwa mikono kulielekeza Jeshi la polisi kutoa dhamana kwa wananchi hawa kwa sababu, wamewekwa ndani kwa amri ya Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Mkuu wa Mkoa, kwa masikitiko makubwa nazungumzia vitendo vilivyofanywa na nafasi kama niliyowahi kuwa nayo. Saa za Mkuu wa Mkoa mwisho ni 48 na kwa tukio lililotokea lenye sura ya jinai mbele yake na baada ya kutoa amri hiyo ya kumweka mtu ndani, anawajibika kwenda kwenye kituo cha polisi au mahakamani kuandika maelezo ya sababu zilizosababisha kumweka huyo raia ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha ni kwamba, wananchi hawa wamekaa mahabusu siku saba. Wakiwa ndani siku ya tano, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wa Mkoa na Katibu wa Mkoa walikwenda kuwajulia hali na walipoomba wakutane nao, walimpigia simu Mkuu wa Mkoa na kuweka sauti na kumwambia, "Mkuu tumekuweka kwenye sauti, watu hawa tumewakuta, ni viongozi saba, viongozi wa jamii, viongozi wa chama na waheshimiwa madiwani." Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa bila aibu, mbele ya wale ambao wametuhumiwa na wamekaa ndani siku tano, akatamka yeye mwenyewe kwa kinywa chake, "nimewaweka ndani, najua hawana makosa, lakini wataendelea kuozea hapo mpaka Mbunge wao atakapokuja kupiga magoti kwangu." Kitendo hiki nisingepiga simu kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, wala nisingepiga simu kwa Waziri wa TAMISEMI, kama ningekuwa na mahusiano mazuri na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi mmoja uliopita, baadhi ya Wabunge wa Mkoa wa Manyara tulikwenda kwenye mkutano

mmoja pale Manyara, aliwasalimia Wabunge na akakataa mkono wangu na kukataa salamu zangu. Baada ya hapo nikasema si neno, siwezi kuendelea kulazimisha salamu. Hata hivyo, katika hili ambalo linahusu raia wangu, wananchi walioniweka madarakani na Rais Samia madarakani, nitaendelea kuwasilisha kilio hiki kwa wale ambao wanamwakilisha Mheshimiwa Rais, ambao ni Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokitamka na ambacho kilionekana kwenye mitandao ya simu na wale wananchi wakisikitika baada ya kutolewa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni kwamba, kitendo hicho hakiingii kwenye akili ya kiongozi yeyote. Hata hivyo, anasema mpaka nimpigie magoti. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, nitapiga magoti Kanisani kwa Mungu wangu aliye hai, nitapiga magoti kwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu na Mkuu wa Nchi yangu, akiniamuru fanya hiki. Hata hivyo, nataka nimpe taarifa, sitakaa nipige magoti kwa Queen Sendiga wala kwa Mkuu yeyote wa Mkoa katika Jamhuri ya Muungano kwa sababu, siyo nafasi yangu kujitweza kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, tunapozungumzia misingi ya utawala bora, utawala wa Sheria, hakuna aliyepo juu ya Sheria. Hata kama Mkuu wa Mkoa ana maslahi yake na kumwandaa mgombea wa Simanjiro ambaye wala hana madhara kwangu, mimi siyo mtoto wa kufikia kwa chama hiki. Mimi siyo mtoto wa kufikia kwenye uraia wa nchi yangu, wala siyo mtoto wa kambo kwa mamlaka ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, ifike mahali wanaopewa dhamana na Rais, wajiweke kwa namna ambayo wananchi wakiwaona, waone wamemwona Rais. Nilikuwa Mkuu wa Mkoa, miongoni mwa ma-*DC* wangu ni pamoja na Komredi Kassinge, huyu hapa, hatujawahi kumweka mtu ndani kwa masaa yoyote yale kwa miaka yangu minne, sijawahi kumweka mtu ndani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olesendeka, pole sana kwa kadhia uliyoipata. Nikuombe sasa uchangie maoni na ushauri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, safi kabisa nakushukuru. Maoni yangu katika eneo la utawala bora ndio hayo. Naomba sasa niende katika eneo lingine ambalo ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mashaka kwamba, Wilaya yangu ya Simanjiro inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinapaswa kupata msaada wa Serikali katika kipindi hiki na hasa baada ya mvua kubwa za mwaka 2023. Hivi leo nimepokea taarifa kwamba, Bwawa la Sukura limekauka, bwawa ambalo lilichimbwa tangu wakati wa Marehemu Sokoine na karibu kata mbili zinazotegemea bwawa hilo sasa mifugo itatawanyika. Ninamwomba Waziri Mwigulu na Waziri mwenye dhamana katika masuala ya mabwawa ya mifugo watenge fedha, kwa ajili ya dharura hiyo iliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo pia korongo lililowaathiri sana wananchi wa Kata ya Shambarai, Mirerani, Endeamutu na Kata ya Naisinyai, ambalo jana watu wa Bonde pamoja na Mkuu wa Wilaya, Kopro Lulandala walikwenda kule, kwa ajili ya changamoto ambayo wananchi wanayo katika lile eneo. Ni rai yangu kwa wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tusaidieni kupata fedha, kwa ajili ya kunusuru kadhia hiyo ambayo imewakabili wananchi katika mvua zilizopita. Hii ni pamoja na barabara za Kata za Msitu wa Tembo na Kata ya Ngorika ambazo hivisasa hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho, ni muhimu sana tunapozungumzia habari ya maendeleo na ustawi wa wananchi, ipo miundombinu ambayo inatakiwa iangaliwe, na hasa katika Sekta ya Ufugaji. Tunapozungumzia ufugaji wa kisasa, ufugaji wenye tija, ng'ombe wenye nyama ya kutosha, ng'ombe wenye maziwa mengi ni lazima kuboresha miundombinu. Huwezi ukadai kuwa na *fresian, jerse*y na *Ayrshire* katika mazingira ya nyanda kame, bila kuwa na mabwawa ya kumwagilia majani na kuotesha majani yatakayotumika na ile mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi pia, kutarajia kuwa na *boran, simmental, Brahman,* ng'ombe wa maziwa na nyama halafu ukategemea waweze kustawi katika ukanda ambao

nyumbu, swala, pundamilia, nyati na tembo wanatoka katika hifadhi na kuleta aina ya kupe ambao wanaambukiza magonjwa ya *anaplasmosis, East Coast fever, MC* na *malignant catarrhal fever and foot-and-mouth disease*. Wakati umefika sasa mipango yetu ijielekeze kwenye uwekezaji wa kusaidia wafugaji kuwa na mbegu bora. Pia, ranchi zetu za *NARCO* zifanye kazi waliyopangiwa, ya kuwa na mifugo bora ambayo wananchi wataweza kuiga kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Kongwa leo, wale ng'ombe wote wa Wagogo ni wafupi. Ni wafupi kwa sababu, Kongwa haijatimiza wajibu wake wa kuwasaidia majirani kuwa na mifugo bora yenye nyama nyingi na maziwa mengi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDSIHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze Mawaziri, Mheshimiwa Profesa. Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuwasilisha vyema hotuba zao za Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/2026. Katika mpango huo, Serikali imeainisha nia na mikakati ya kuboresha sekta mbalimbali za uchumi nchini ikilenga kuimarisha Sekta za Uzalishaji; Uchimbaji Madini, Nishati, Elimu, Biashara, Viwanda na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye kuishauri Serikali itekeleze kwa ufasaha mikakati yote iliyopangwa katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Nishati, Elimu, Viwanda na Biashara ili kuboresha uchumi wa Watanzania na Taifa kwa ujumla. Sekta za Uzalishaji za Kilimo, Mifugo na Uvuvi Nchini

Tanzania zinahusisha zaidi ya nusu ya nguvu kazi ya Watanzania. Hivyo basi, ni vyema Mpango wa Maendeleo ulenge kwenye kutekeleza yale yote yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali Mpango uzingatie yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao kwa kutumia mbinu bora za kilimo ufugaji na uvuvi.

(ii) Kuendelea kuboresha mifumo ya umwagiliaji na kuchimba mabwawa ya kunywesha mifugo na ya kufuga samaki.

(iii) Kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuanzisha viwanda vidogovidogo na kutengeneza vifungashio bora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

(iv) Kuzalisha mazao mengi ambayo yatakidhi uhitaji wa viwanda vya ndani na mengine kuingia katika soko la kimataifa.

(v) Kutafuta soko la uhakika kwa mazao yote ya kilimo na mifugo yanayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yakitekelezwa kwa nidhamu, bila wasiwasi tutaboresha mapato ya wakulima, wafugaji, wavuvi na yale ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze sana Serikali kwa juhudi na uwekezaji mkubwa kwenye Sekta ya Nishati. Mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni wa kielelezo na umetatua changamoto ya upungufu wa umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwamba, kwenye mpango huu wa maendeleo, Serikali iwekeze kikamilifu kwenye maendeleo ya nishati mbadala yanayohusisha matumizi ya gesi asilia. Ni vyema mpango utekeleze miradi inayojikita kwenye matumizi ya gesi asilia kuzalisha umeme na matumizi ya

nyumbani kwa kupikia na kuendesha mitambo kama magari, kwani nchi yetu ina akiba ya gesi ya futi za ujazo trilioni 57.54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usalama wa nchi yetu na kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, ni vyema kujiandaa na kutekeleza uwekezaji katika miradi ya nishati mbadala na endelevu itakayotumia nishati ya jua na joto ardhi kuzalisha umeme. Nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 2,000 za umeme wa jua na joto ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wetu, naishauri Serikali ijikite kuisaidia Sekta ya Elimu kwenye kutekeleza mitaala mipya ambayo inajikita kwenye kutoa elimu yenye ujuzi ambao utawawezesha vijana wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari waweze kujitegemea na kuwa na manufaa kwa Taifa baada ya kuhitimu. Kwa upande wa sekondari, ni muhimu Taifa lifanye mageuzi ya haraka kwenye utekelezaji, ili tusiwe na matabaka ya wasomi. Hivyo basi, Mpango wa Maendeleo ujikite kwenye uwekezaji katika miundombinu ya shule kwa kujenga madarasa, maabara na kutoa vitabu. Vilevile Serikali itoe ajira kwa walimu ili kukabiliana na upungufu mkubwa uliopo katika shule za msingi na sekondari zilizomo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Biashara na Viwanda ni vyema mpango ukalenga kwenye kuisaidia nchi iwe na viwanda vingi ambavyo vitatusaidia kuzalisha bidhaa zinazokidhi mahitaji ya Watanzania na ziada kuuzwa nje. Kwa mfano, ni vyema kuweka mazingira rafiki ya kikodi kwenye viwanda vya ndani ili waweze kuzalisha kwa tija na baadaye kuuza kwa wingi na kutusaidia kuboresha pato la Taifa. Kwenye ziara za Kibunge tulizofanya kwa kuvitembelea viwanda mbalimbali hapa nchini, kumekuwepo na kilio kinachofanana cha kodi ambazo siyo rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *contribution to Tanzania National Development Plan 2025/2026; The Importance of Mental Health in National Development.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *as Tanzania works towards its National Development Plan for 2025/2026, it is crucial to consider mental health as an integral component of national development. Mental health is not only a personal matter but a societal issue that affects social, economic, and physical well-being. According to the World Health Organization (WHO), mental health is defined as a state of well-being where an individual realizes their own abilities, can cope with the normal stresses of life, work productively, and contribute to their community. Therefore, mental health is essential to fostering a productive, healthy and stable society, all of which are central to Tanzania's development goals.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *mental health and its impact on development; mental health affects all aspects of society. Individuals with mental health challenges often experience poor economic outcomes, lower educational achievements, reduced productivity and increased rates of disability. Mental health issues can also lead to strained healthcare systems and significant social costs. This is particularly concerning in a developing country like Tanzania, where the population faces numerous socio-economic challenges, including poverty, unemployment, and limited access to quality healthcare services.*

*Furthermore, untreated mental health conditions can exacerbate social inequalities and hinder the realization of Tanzania's sustainable development goals (SDGs), particularly in health (SDG 3), quality education (SDG 4), and decent work (SDG 8). To achieve a prosperous and equitable society, addressing mental health must become a priority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Performance Audit of Mental Health Services in Tanzania (2024 Report); in March 2024, the Controller and Auditor General (CAG) of Tanzania conducted a Performance Audit Report on the availability of mental health care services in the country. The audit revealed significant gaps in mental health care services, including limited access to mental health professionals, inadequate infrastructure, and a lack of public awareness about mental health issues. Key findings include:-*

*(i) Inadequate Mental Health Professionals: There is a severe shortage of trained mental health workers, including psychiatrists, psychologists, and social workers, with many regions in Tanzania lacking such professionals entirely.*

*(ii) Limited Mental Health Infrastructure: Public health facilities often lack the necessary resources and infrastructure to provide adequate mental health care, such as specialized psychiatric wards or necessary medical equipment.*

*(iii) Stigma and Public Awareness: Mental health is often stigmatized in Tanzanian society, which leads to underreporting and untreated cases. There is a critical need for public awareness campaigns to reduce stigma and promote early intervention.*

*(iv) Funding and Budgetary Allocation: Mental health services are underfunded and the current national budget allocation for mental health is insufficient to address the growing demand for services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *recommendations from the 2024 Performance Audit Report; the CAG's report outlined several key recommendations to improve mental health services in Tanzania:-*

*(i) Increased Investment in Mental Health Care: The government should allocate more funds to mental health services, including the expansion of psychiatric care infrastructure, hiring more mental health professionals and providing necessary training.*

*(ii) Public Awareness Campaigns: Launch national campaigns to raise awareness about mental health, reduce stigma and encourage early treatment.*

*(iii) Integration of Mental Health into Primary Health Care: Mental health services should be integrated into*

*primary health care systems to make them more accessible in rural and underserved areas.*

*(iv) Strengthening Mental Health Policies: Review and update existing mental health policies to ensure they align with international best practices and address the evolving mental health needs of Tanzanians.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *recommendations for Inclusion in the National Development Plan and Budget 2025/2026; to ensure mental health is adequately addressed in Tanzania's National Development Plan and Budget for 2025/2026, the following actions are recommended:-*

*(i) Allocate Adequate Budget for Mental Health: The government should allocate a specific percentage of the national health budget to mental health services. This would ensure that resources are dedicated to improving mental health infrastructure, hiring professionals and creating awareness campaigns.*

*(ii) Policy Implementation and Monitoring: Include mental health in national policies and establish a monitoring framework to track progress on the availability of mental health services. This should be linked to Tanzania's overall development goals, ensuring that mental health is not sidelined.*

*(iii) Integration into Education and Workplace Programs: Mental health services should be integrated into schools, universities and workplaces to promote early detection and prevention. The national plan should also consider providing mental health education as part of the curriculum at various levels.*

*(iv) Public-Private Partnerships: Encourage collaboration between the public and private sectors to build and sustain mental health infrastructure. Private sector investment can help meet the growing demand for mental health services, especially in urban areas.*

(v) *Public Awareness Campaigns: Launch national campaigns to raise awareness about mental health, reduce stigma, and encourage early treatment. Let us make this a stepping Stone.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *conclusion; addressing mental health is vital for Tanzania's social and economic development. By incorporating the recommendations from the 2024 Performance Audit Report into the National Development Plan for 2025/2026, Tanzania can improve the mental health of its population, reduce the social stigma associated with mental illness and create a more productive, healthy and prosperous society. Mental health is not merely a healthcare issue but a development issue and its prioritization in national planning will be essential for the success of Tanzania's growth and prosperity in the coming decades.*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayotufanyia Watanzania kupitia Serikali yake ya Awamu ya Sita. Nampongeza kwa maamuzi yake ya kuunda hii Wizara ya Mipango na Uwekezaji, hii inaonesha upendo na maono makubwa ya Mheshmiwa Rais kwa Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii chini ya Waziri wake, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii. Nitazungumzia kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na hapa ninazungumzia utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, yaani 2023/2024 na pia, robo ya 2024/2025 na hapa nitazungumzia utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye suala la utawala bora na utawala wa sheria. Kwenye mipango ya nyuma imeendelea kuimarisha mifumo ya utawala bora na utawala wa sheria kwani sio ubishi, mifumo hii inatakiwa kuendelea kuimarishwa. Nimejaribu kupitia mpango huu wa 2025/2026 sijaona kabisa sekta hii ya utawala bora ikijadiliwa, imenishtua. Hakuna ubishi kabisa kwamba rasilimali watu ndiyo rasilimali

inayotegemewa na rasilimali zote kwa kuwa, rasilimali hizo haziwezi kujiendesha bila ya usimamizi bora wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mpango uweze kufanikiwa lazima kuwepo na rasilimali watu, hivyo basi mpango huu wa Mwaka wa Fedha 2025/2026, lazima useme bayana kwamba, awamu hii imepanga kufanya nini katika kuimarisha mfumo wa utawala bora, mwisho wa siku rasilimali watu iweze kusimamia vyema miradi na programu za kimkakati na kisekta na, ili iweze kusababisha Serikali iweze kufikia dhamira ya maisha bora kwa wote, kama iliyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Ninaendelea kuipongeza Serikali, pamoja na kuimarisha mifumo ya utawala bora pia, imeshughulikia kwa kiwango kikubwa suala la maslahi ya watumishi, hususani wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwakilishi wa wafanyakazi nimeweza kuzifikia halmashauri 184 za Tanzania Bara na kuzungumza na watumishi wa halmashauri hizo. Wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uboreshaji wa maslahi mbalimbali ya kiutumishi, lakini wana changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nizungumzie changamoto kubwa ya makazi kwa watumishi. Makazi bora kwa watumishi imeendelea kuwa tatizo kubwa hasa kwa halmashauri zilizopo pembezoni ambazo pia, zimehamisha makazi ya awali kwenda kwenye makazi mapya ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile makazi kwa mtumishi yeyote ni usalama na ni heshima, ninashauri badala ya kujenga nyumba kubwa na chache za Wakuu wa Idara, Taasisi na Halmashauri, zijengwe nyumba hata za vyumba viwili za kutosha, ili ikiwezekana watumishi wengi wapate makazi na ikiwezekana watumishi watakaoishi kwenye nyumba hizo wachangie kiasi kidogo cha pesa, kwa ajili ya ukarabati mdogo mdogo utakaojitokeza. Ninashauri mpango uje na mkakati wa muda mfupi, wa kati na mrefu wa kutatua tatizo hili kubwa na sugu la kukosekana kwa makazi ya watumishi. Ninashauri Serikali

ishirikiane na wadau mbalimbali pamoja na taasisi na mashirika mbalimbali, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kutafuta fedha za kuendeleza maendeleo katika nchi yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza maisha bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya hali ya uchumi kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2024 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.2 na asilimia 3.3 kwa mwaka 2024 na 2025 mtawalia. Kwa hiyo, uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2022 na unatarajia kukua kwa asilimia 1.7 na asilimia 1.8 Mwaka 2024 na 2025 mtawalia na ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* ulikua wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na asilimia 6.1 mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi wa Taifa, Serikali inaonesha kwamba, mwaka 2023 pato halisi la Taifa Mwaka 2015 lilikuwa shilingi trilioni 148.39 kutoka shilingi trilioni 141.25 mwaka 2022. Sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2022 na shughuli za uchumi zilizochangia ukuaji huu ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa madaraja ya juu na miundombinu ni mchango mkubwa katika kuchochea uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa. Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi ambalo utekelezaji wake umefikia 93% na linatarajiwa kumalizika mwaka 2025 pamoja na madaraja ya juu ya Dar es Salaam.

kukamilika kwake kutaongeza ufanisi katika shughuli za kiuchumi, kukuza biashara na kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha Kimataifa. Serikali itumie mpango wa kufadhili ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* kwa kutumia *ECGA,* ili kukamilisha vipande vyote vilivyobaki kwa haraka, hususan vipande vya Uvinza, Malagarasi, Msagati na Kaliuwa, Mpanda na Karema. Pia, Serikali itumie fursa ya uwepo wa sheria ya mfumo wa kukaribisha sekta binafsi kutumia miundombinu ya reli kwa makubaliano ya malipo ili kuvutia wawekezaji katika reli ya *SGR*.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa na ridhaa yako niwasilishe mchango wangu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi alivyosimamia kidete miradi mikubwa ya kimkakati;

(a) Ujenzi wa *SGR* ambapo sasa *lot II* za Dar es Salaam – Morogoro na Morogoro – Dodoma zimekamilika na kubadilisha kabisa taratibu za usafiri kati ya Dar es Salaam na Dodoma na kufanya uchumi wa Dodoma kupaa ghafla.

(b) Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao sasa umefikia 96% na sasa mgao wa umeme haupo tena nchini.

(c) Kufufua na kulijenga upya Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* na sasa *ATCL* ina ndege 16, ikiwepo ndege moja kubwa ya mizigo.

(d) Kupeleka fedha nyingi, kwa ajili ya miradi ya maendeleo sekta zote majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, naomba nitoe ushauri juu ya mambo muhimu machache ya kuzingatiwa katika mpango unaopendekezwa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kilimo. Hii ndiyo sekta inayoajiri Watanzania wengi (70%), lakini mchango wake katika pato la Taifa uko chini 30% licha ya mipango na kauli mbiu nyingi; uti wa mgongo, siasa ni kilimo, kilimo kwanza na kadhalika. Nchi yetu bado ina eneo kubwa la ardhi ambayo inaweza kuzalisha chakula na mazao mengine ya kibiashara, lakini bado tunashindwa kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mpango unaopendekezwa nashauri uelekeze nguvu kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea hali ya hewa. Pili, mpango unaopendekezwa nashauri uelekeze nguvu kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua yatumike kufanya kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine ya kibinadamu na tatu, mpango unaopendekezwa nashauri uelekeze nguvu katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao yanayolimwa, ili hatimaye kilimo chetu kiwe ni kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati. Mpango unaopendekezwa nashauri uelekeze nguvu nyingi katika kuhakikisha gesi asilia tuliyonayo inavunwa, ili azma ya Mheshimiwa Rais ya matumizi ya nishati safi, salama na rafiki kwa mazingira kwa kiwango cha 80% ifikapo Mwaka 2034 inatimia, ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme ambao utahitajika kwa wingi kukidhi mahitaji yatokanayo na umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya barabara. Mpango unaopendezwa nashauri uhakikishe ahadi zote zilizotolewa na viongozi wakuu wa nchi, za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, zinatekelezwa. Mpango pia, uzingatie hali ya majimbo kijiografia, ukubwa na *terrain* katika ujenzi ama kwa lami au zege kwa maeneo ya milimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameshasema mengi ya muhimu kwa hiyo, kwa haya machache ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mungu kunijalia afya na nguvu za kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Kyerwa na kuwepo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi. Ninampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa jinsi alivyomwaga pesa nyingi kwa wananchi na kwa msimamo wake wa kutowasikiliza wasiotutakia mema; walipiga kelele za kuzuia *DP World*, ujasiri na uimara wake umeanza kuleta neema kupitia uwekezaji kwa Bandari ya Dar es Salaam. Mungu aendelee kumlinda na kumpa maono zaidi mama yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mwigulu na wasaidizi wake kwa kazi kubwa na nzuri ya ukusanyaji na usimamizi wa fedha. Ndiyo maana tunaona kila kona ya nchi yetu miradi inaendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Mipango, Profesa Kitila Mkumbo, kwa mpango mzuri wa kuisogeza Tanzania mbele. Ushauri wangu ni, pamoja na miradi mingi iliyopelekwa kwa wananchi bado haijakamilika. Ninaishauri Serikali, pamoja na mipango mizuri Serikali iweke nguvu kubwa kwenye miradi ambayo haijakamilika ili ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara nyingi, miradi mingi ya maji haijakamilika, miradi hii ikikamilika italeta unafuu wa maisha kwa wananchi kwa kupunguza gharama za maisha, lakini pia, kwa kuchukua muda mrefu inaiingiza Serikali kwenye gharama za kupigwa faini za kuwacheleweshea wakandarasi malipo. Miradi hii ikikamilika kwa wakati itawapatia huduma wananchi na unafuu wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, mifugo na uvuvi. Naipongeza Serikali kwa hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa kuboresha kilimo, mifugo na uvuvi, ninaamini tukiamua kuongeza

nguvu kwenye sekta hizi tunaweza kuongeza fedha nyingi za kigeni maana mazao haya yanayotokana na kilimo, mifugo na uvuvi yanahitajika sana nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunayo mazao ya kimkakati na zao la kahawa likiwa mojawapo ya mazao hayo, ambapo tayari tumeshapata soko la uhakika katika nchi ya China. Hili ni soko kubwa na la uhakika, tukilitumia vizuri tutainua Pato la Taifa na la mwananchi mmoja mmoja, lakini kilimo hiki, ili kiwe na tija ni lazima Serikali iongeze utafiti kwenye mazao haya ya kimkakati, tupate mbegu bora na kupata uzalishaji mkubwa. Mfano, pamoja na zao la kahawa kuanza kupata bei nzuri na soko la uhakika, zao hili limeanza kushambuliwa na ugonjwa wa mnyauko na wadudu wanaokula majani ya kahawa mpaka inakauka na hapa Serikali ituambie imejipangaje kukabiliana na ugonjwa huu unaoshambulia kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya kuinua uchumi. Ninaishauri Wizara ya Mipango kuweka nguvu kwenye matumizi ya gesi majumbani na kwenye magari. Wataalam wengi wanasema matumizi ya gesi ni nafuu kuliko umeme na mafuta. Mungu ametujalia neema hii, sasa ni wakati wa kuitumia, ili kuongeza pato la Taifa na itapunguza gharama za maisha kwa wananchi na uharibifu wa mazingira ambao unaendelea kuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchuchuma na Liganga. Miradi hii imekuwa ikiongelewa. Naishauri Serikali ifike sehemu ya kufanya maamuzi magumu, kama uamuzi uliofanyika kwenye Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na Mradi wa *SGR,* ili tuweze kufikia hitimisho la miradi hii ambayo imekuwa Wimbo wa Taifa. Ninashindwa kuelewa shida iko wapi na nini kinakwamisha. Waziri atueleze kama kuna kizuizi katika ulimwengu wa roho tuiteni watumishi wa Mungu ili tumkemee yeye azuiaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulinzi wa miradi yetu. Naishauri Serikali, haya mafanikio tunayoyapata kwa miradi yetu ya kimkakati, kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR* na Bomba la Gesi hapa tunatangaza vita ya kiuchumi. Lazima kwenye mipango yetu tuweke mkakati wa kuilinda dhidi ya hujuma

yoyote inayoweza kutokea kwa maadui wa ndani na maadui wa nje maana hii ni vita ya kiuchumi. Maendeleo ni vita, wako maadui zetu wasingependa waone tunafanikiwa kwa hiyo, katika hili Serikali ni lazima ijipange kukabiliana kuhakikisha miradi yetu iko salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja zote na ninaomba kuwasilisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Judith Kapinga, jiandae Mheshimiwa Mahundi na Mheshimiwa Mollel, jiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa ufanisi mkubwa sana ambao unalenga kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Kwa rai hiyo hiyo, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, wote kwa kazi nzuri wanazozifanya za kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati tunaongozwa na kiongozi mchapakazi, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Tunaendelea kumpongeza kwa kuhakikisha Sekta ya Nishati inaendelea kuchangia katika uchumi wa Taifa letu na kutupatia utulivu ambao tunao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze watoa hoja, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara zao za Fedha na Mipango. Mtakubaliana na mimi kwamba, wanafanya kazi nzuri sana katika kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sekta wezeshi, lengo la mpango ni kuhakikisha Sekta ya Nishati inachangia katika ukuaji wa biashara, viwanda pamoja na ukuaji wa uchumi na shughuli nyingine za jamii. Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mpango,

Sekta ya Nishati imejikita kuhakikisha tunaboresha miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Tunaboresha misingi ya kiuchumi katika Sekta ya Mafuta na Gesi, vilevile tunaendelea kuboresha mazingira wezeshi ya kuhusisha sekta binafsi katika sekta hii muhimu ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge juu ya michango yao kwenye vyanzo vya uzalishaji wa umeme. Nimewasikia wakitoa mawazo kwamba, inabidi tuboreshe vyanzo zaidi, ili kuboresha upatikanaji wa umeme katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaanza utekelezaji wa mpango huu 2021, tulikuwa tuna *megawatt* 1,571 ambazo zilikuwa zinachangia katika gridi yetu ya Taifa. Leo ambapo tunakwenda kumaliza Bwawa la Mwalimu Nyerere tunakwenda kuwa na uwezo wa takribani *megawatt* 3,914. Ni kazi kubwa sana imefanyika kuweza kufikia *megawatt* hizi ambazo tunazo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaelewa Waheshimiwa Wabunge katika azma yao ya kuhakikisha tunaendelea kuwa na vyanzo vingine vya uzalishaji. Pia, Serikali tayari tuna mipango hiyo ambayo inatekelezeka na tunayo mipango ya mbeleni. Pamoja na Mradi mkubwa wa Julius Nyerere ambao Waheshimiwa Wabunge wametoa pongezi juu ya utekelezaji wake, kwa sasa hivi tuna mitambo minne inayozalisha *megawatt* 940.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mingine ya uzalishaji ambayo pia, inaendelea. Tunao Mradi wa Malagarasi kule Kigoma, ambao ukikamilika utakwenda kuzalisha takribani *megawatt* 49.5. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, alitupatia fedha dola za Kimarekani milioni 144, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mradi wa Malagarasi, tunao Mradi wa Kakono kule Kagera ambao ukikamilika utakwenda kuzalisha takribani *megawatt* 87.8. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais alitupatia fedha takribani Dola za Kimarekani milioni 161.47, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hii mitatu tunao mradi wa uzalishaji wa umeme kwa jua Kishapu ambao unaenda kuzalisha *megawatt* 150, na tumeanza awamu ya kwanza ya *megawatt* 50 na tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais alitupatia fedha takribani *Euro* milioni 130.7 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Waheshimiwa Wabunge nataka kuwahakikishia kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayo azma na nia ya kuhakikisha tunaendelea kuwa na miradi ya uzalishaji na ninyi wote mmeona miradi ambayo yote wakandarasi wako *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo tunayo azma ya kuendeleza miradi mingine hapo mbele, tunao mradi wa Ruhuji ambao kama utatekelezwa utaenda kuzalisha takribani *megawatt* 358, Rumakali *megawatt* 222, pia tunao mradi wa Somanga - Fungu ambao utaenda kuzalisha takribani *megawatt* 300, vilevile tuna mraadi wa Mtwara gas *fire* ambao utaenda kuzalisha takribani *megawatt* 330. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo nimewasikia Waheshimiwa Wabunge wakionesha umuhimu wa Serikali kuanza uzalishaji wa umeme kupitia rasilimali yetu ya jotoardhi, nami nakubaliana na ninyi Waheshimiwa Wabunge. Rasilimali hii ya jotoardhi ipo katika ukanda wa nchi ambazo zinapitiwa na Bonde la Ufa, katika nchi hizi zote kama rasilimali hizi zitatumika katika kuzalisha umeme zitaweza kuzalisha umeme wa takribani *megawatt* 40,000. Tanzania pekee yake tunakadiria uwezo wa kuzalisha takribani *megawatt* 5000, kwa hiyo, ninakubaliana na ninyi ipo azma ya Serikali kuanza kuzalisha umeme kwa jotoardhi. Kinachotupa nia na faraja na moyo ni kwamba katika miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita tumepiga hatua kuelekea uzalishaji wa umeme kwa kutumia jotoardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, tumewawezesha kwa uwezo - *training* mbalimbali wataalam wetu ili waweze kubobea katika jambo hili ambalo ni jipya kwetu. Pili, tulifanya tafiti za awali za kubaini maeneo ambayo yana rasilimali yetu hii, tulibaini maeneo matano ikiwemo Lutoi, Natron, Mbozi, Songwe pamoja na Kyegombaka. Kwa hiyo, baada ya kubaini

maeneo yale ilitakiwa sasa twende ku-*confirm resource* kuhakikisha tuna rasilimali kiasi gani kwenye kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametupatia fedha na tumeshamweka mshauri mwelekezi *(KenGen)* ambaye sasa yuko *site* kwa ajili ya kufanya zoezi la *confirmation of resource*. Pamoja na hiyo tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais ametupatia fedha bilioni 15.7 kwa ajili ya kununua mtambo wa uchorongaji kwa ajili ya zoezi hilo. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuelekea uzalishaji wa umeme kwa jotoardhi hakika tumepiga hatua, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kusimamia kazi hii kwa weledi mkubwa sana chini ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ili kuonyesha kwamba tunaenda kule ambako ni matamanio ya ninyi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendeleza zaidi vyanzo vya nishati jadidifu ili kupunguza utegemezi wa kiuchumi, lakini kuongeza usalama wa nishati, vilevile kuleta uendelevu wa kinishati ambao unachangia kiasi kikubwa sana katika kulinda mazingira na kwa kweli tupo kwenye njia salama sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ya uzalishaji, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge wakichangia kuhusiana na umuhimu wa Serikali kuwekeza zaidi katika miradi ya usafirishaji pamoja na usambazaji. Serikali inawekeza katika miradi mbalimbali ya *power transmission*, miradi ya msongo mkubwa wa umeme ambao utaweza kusaidia kuimarisha umeme katika maeneo mbalimbali, vilevile na miradi ya msongo mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi mingi na miradi ambayo ni ya ndani ya nchi na miradi ambayo itasababisha pia sisi kwenda katika mkondo wa umeme wa nchi jirani vilevile. Baadhi ya Wabunge wamechangia hapa, tunao mradi ambao utatu-*connect* kwenye *south African power pool* na nchi zaidi ya nchi nane, huo ni mradi ambao umeanza na mkandarasi yuko *site* na

utajenga pia vituo vya kupooza umeme kuanzia Iringa, Mufindi, Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga. Kwa kweli ni mradi mkubwa sana ambao utaimarisha umeme hapa nchini, lakini utatufanya tu-*connect* na nchi nane za Ukanda wa Jangwa la Sahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalojivunia ni mafanikio makubwa ambayo tumeweza ku-*connect* na *East African Power Pool,* kupitia mradi wetu wa njia ya kusafirisha umeme lakini tumejenga kituo pale Remuguru, Arusha ambacho kina-*connect* na kituo upande wa pili wa Kenya na sasa hivi tuna uwezo wa kutoa umeme na kuingiza umeme kutoka katika nchi 14 za ukanda wa Afrika Mashariki. Kwa kweli, pamoja na changamoto ambazo tunazo tumepiga hatua kubwa sana katika zoezi la usafirishaji wa umeme ndani ya nchi na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la usambazaji wa umeme nimewasikia Waheshimiwa Wabunge juu ya matamanio yenu kuhakikisha tunaendelea kuboresha miradi kwenye vitongoji. Katika Bunge hili mwaka 2021, Wabunge waliishauri Serikali kuweka mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji vyote, mwezi Machi, 2021 tulianza mradi huu. Mheshimiwa Rais alitoa fedha shilingi trilioni 1.573 kuhakikisha tunapeleka umeme vijiji vyote na hadi leo tumebakisha vijiji 78 tu. Kwa hiyo, azma ambayo tulikubaliana hapa katika mpango huu wa kupeleka umeme kwenye vijiji 4,071 Waheshimiwa Wabunge imetekelezeka na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutenga fedha kwa ajili ya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunaanza zoezi la vitongoji na kwa kweli Serikali haijapoa, tumeanza na mradi wa vitongoji 3,070 na saa hivi tunaweka mradi wa vitongoji 4,000, ni azma yetu kati ya miaka mitano mpaka saba tuweze kukamilisha vitongoji 32,000 ambavyo vimebakia. Kwa hiyo, ndugu zangu maendeleo ni hatua ni lazima yafanyike kwa awamu ili tuweze kufika huko, lakini tulikotoka siko ambako tuko sasa hivi, tumepiga hatua kubwa na Serikali imejizatiti kuendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji ili wananchi wetu waweze kuboresha shughuli zao za kiuchumi na kijamii kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika Sekta ya Mafuta na Gesi, kwa kweli nimewasikia juu ya matamanio yao ya kuona mradi wetu wa *LNG* unaendelea na ndiyo matamanio ya Serikali. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kusubiri nia ya Serikali ni kuona mradi huu unatekelezeka. Huu ni mradi ambao utazalisha takribani futi za ujazo trilioni 45. Kwa hiyo, tuendelee kusubiriana, tunaendelea kufanya kazi nzuri nataka niwahakikishie tuko sehemu sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamechangia juu ya miradi ya mafuta na gesi katika mkondo wa juu, mkondo wa kati na mkondo wa chini, lakini nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema pamoja na ugunduzi wa gesi takribani *TCF* 57 tunazalisha katika vitalu viwili tu vya Songosongo pamoja na Mnazi *Bay*. Nataka niwaambie, baada ya miaka 16 leo Serikali imetoa *development license* katika kitalu cha Ruvuma Ntorya na kitalu hiki kina jumla ya futi za ujazo trilioni 1.4. Kwa hiyo, baada ya miaka 16 Serikali ya Awamu ya Sita imepiga hatua kwa kutoa *development license* kwa ajili ya kitalu cha Ntorya, kwa hiyo kwa kweli tumepiga hatua, lakini baada ya miaka takribani 12 tunaenda kwenye duru la tano la kunadi vitalu ifikapo mwezi Machi mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yetu ni kuhakikisha vitalu ambavyo tunavyo takribani 24, ambavyo 21 vipo katika Bahari Kuu na tatu vipo *Lake* Tanganyika, tunafanya matumizi mazuri ya rasilimali ambazo tunazo. Kwa hiyo, ninataka niwaondoe hofu Serikali ya Awamu ya Sita iko katika mchakato sahihi sana kuhakikisha tunatumia rasilimali zetu za mafuta na gesi kwa mstakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine Wabunge wengine wamesema hapa ni pamoja na Mradi wa *EACOP*, vilevile tunaendeleza utafiti katika kitalu chetu cha Eyasi, Wembere kwa hiyo kwa kweli mambo yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamechangia juu ya umuhimu wa kutumia gesi asilia kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea. Nataka niwaeleze Waheshimiwa Wabunge

kwamba mkakati huu tunao. Tunao mpango kabambe wa matumizi ya gesi ambao ni wa 2017 hadi 2046 na mpango huu umejikita katika kuwezesha viwanda hivi vya *Petro-chemicals* kwa ajili ya kutumia gesi asilia katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vina matumizi makubwa kwa hiyo suluhisho lake ni hii gesi ambayo tunategemea kuwa na mradi wa *LNG* na *TPDC* wamejipanga kutoa eneo pale kwa ajili ya kongani la viwanda ikiwemo viwanda hivi vya kuzalisha mbolea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malizia.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naamini Wizara ya Viwanda pamoja na Wizara ya Kilimo tutashirikiana kwa karibu kuhakikisha katika Mradi huu wa *LNG, TPDC* wanatenga eneo kwa ajili ya kongani la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mafanikio haya ambayo tunayaona katika Sekta ya Nishati ni jitihada za Mheshimiwa Rais. Miradi hii inatekelezeka kwa sababu Mheshimiwa Rais anatafuta fedha za kutekeleza miradi hii, lakini inatekelezeka vizuri sana kwa sababu Mheshimiwa Waziri, Dkt. Dotto Mashaka Biteko anahakikisha miradi yote inatekelezeka kwa ufanisi na weledi mkubwa sana, tunaendelea kumwombea Mheshimiwa Rais afya njema ili tuweze kunufaika na matunda yake kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI;** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu inaelekea sekta yako unaifahamu vizuri sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mahundi, wajiandae Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Mkenda na Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote

ninapenda kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye anaendelea kutuwezesha kutimiza majukumu yetu ya kibinadamu. Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa Mama msikivu, Mama ambaye anashaurika na kutufanyia mambo mengi sana na mpango thabiti wa maendeleo ya nchi yetu tunaweza kuona namna wasaidizi wake tunavyoendelea kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nasi tuko pamoja na wenzetu kuhakikisha Mpango wa Maendeleo ya Taifa tunausimamia kwa thabiti, kwa sababu bila mawasiliano thabiti mambo yote haya tunayoyapanga huenda yasiende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuongelea uhuru wa Vyombo vya Habari kwa sababu haya yote tunayoyafanya, tumekuwa tukijifunza kutoka kwa wenzetu walioendelea zaidi yetu, lakini na sisi pale tunapofanya kwa lengo la kuwafikishia wananchi wetu lazima Vyombo vya Habari vihusike. Vyombo vya Habari vimeendelea kuimarika nchini Tanzania na kwa namna ambavyo Dkt. Samia ameendelea kuongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyombo vya Habari vimeweza kupata Bodi ya Ithibati ambayo lengo lake kubwa ni kuhakikisha taarifa zote zinazowafikia wananchi ziwe zenye maudhui rafiki na siyo za kubomoa maadili ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha Vyombo vya Habari tunaendelea kulinda uhuru wake tumepiga hatua kubwa sana, tumeweza kuvuka hatua 46 tokea mwaka 2023, Chombo chetu cha Habari kilikuwa cha 143 lakini mwaka 2024 tumeshika nafasi ya 97 kwa maana hiyo tumeweza kuvuka kwa asilimia kwa hatua 46 zaidi, maana yake tumepita nchi nyingi sana katika kuona kwamba tunatetea na kuishi Uhuru wa Vyombo vya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa kidigitali sisi kama Wizara ya Habari, Mawasiliano, Teknolojia ya Habari

tumeweza kuhakikisha tunajenga miundombinu ya kutosha ili tunavyoingia sasa kwenye uchumi wa kidigitali tuweze kufanya kazi vizuri. Tuna mradi wa minara 758, Waheshimiwa Wabunge wote watakuwa mashahidi katika kila Jimbo tumeweza kufikisha minara mitatu na zaidi kwa lengo la kuona kwamba tunaboresha usikivu maeneo yote na tunaendelea kuiboresha huduma hii ya minara kadri ambavyo tunawezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika minara hii iko idadi ya minara ambayo inajengwa kwa ajili ya kuboresha kutoka teknolojia ya *2G* na inakwenda kwenye teknolojia ya *3G* hadi *4G*, maana yake nini? *2G* ni zile simu ndogo maarufu kama viswaswadu zamani tumekuwa tukivitumia kwa ajili tu ya kuongea *voice,* lakini tumeboresha minara mingi sasa iweze kutumia teknolojia ya *3G* na *4G* kwa maana ya kuruhusu *data* na hii ndiyo inayoendelea kutusogeza katika dunia ya ulimwengu wa kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nitoe taarifa katika hii minara 758 tayari minara zaidi ya 302 imewashwa. Tuko zaidi ya 40% minara imewashwa na tumeweza kuongeza usikivu maeneo mbalimbali. Kwa maeneo yale ambayo bado hatujayafikia ni ile minara zaidi ya 400 Waheshimiwa Wabunge niwaombe tuendelee kuwasiliana na ndiyo maana juzi tumeweza kugawa hicho kitabu ambacho kinatoa taarifa ya utekelezaji wa minara hii na kila Mbunge hapa inaonesha Jimboni kwake wapi mnara unajengwa. Kwa hiyo, kama kuna makosa ya kibinadamu yaliyofanywa na wataalam wetu tunawakaribisha ninyi mko hapa kwa niaba ya mamilioni ya Watanzania huko nje, basi tuweze kuwasiliana tuweze kurekebishana kuona tunaujenga mnara eneo halisi lenye changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya hiyo minara 758 tuna minara mingine ambayo ipo kwenye mradi inajulikana kama *rural connectivity,* hii kazi yake ni kusogeza huduma kule pembezoni mwa miji kabisa nayo ni minara 636. Kati ya minara hii minara 621 ni maalum kwa ajili ya usikivu wa simu na minara 15 ni kwa ajili ya redio. Haya yote tumeyafanya kwa kuzingatia jiografia ya Tanzania maeneo ya mipakani tumeyazingatia kule mipakani kwa mfano kwa Mkoa wa Mbeya ukifika Kyela ama ukifika Tunduma

kwa Mkoa wa Songwe unaona kuna mwingiliano wa mawasiliano, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema huu ni wakati sasa Watanzania wanatakiwa kupata mawasiliano thabiti kutoka ndani ya nchi na siyo mwingiliano wa mawasiliano kutoka nchi jirani kwa sababu ya minara iliyopo kwenye mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tunayafanya lengo ni kuhakikisha mpango huu wa Taifa ambao Waheshimiwa Wabunge wameujadili hapa na kutoa maoni yao ya kina na kuona Serikali tunaweza kuwajibika vizuri kuleta maendeleo kwa wananchi, mawasiliano haya ndiyo yatakayowezesha haya yote tunayoyafanya kwa sababu pia katika maagizo ya Mheshimiwa Rais tunakumbuka ametusisitiza wasaidizi wake wakati ananiapisha mimi, wakati anamwapisha Mheshimiwa Jerry Silaa lakini katika mikutano mbalimbali tuhakikishe mifumo inasomana, nasi tumeshafanya kazi sasa ni zaidi ya 99% na kufika Disemba tutazindua rasmi kuonesha kwamba mifumo ya makampuni mengi sasa yanaweza kusomana na kila kitu kinakwenda kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhakikisha tunaimarisha namba jamii kwa maana ya kila Mtanzania sasa badala ya kumiliki ile namba ya *NIDA* ambayo inam-*favo*r mtu kuanzia miaka 18 na kuendelea, sasa namba ya kijamii ni namba hiyo hiyo na *NIDA*, lakini sasa inaboreshwa kwa kuongezewa taarifa itaanzia mtoto anayezaliwa leo. Kwa hiyo, wananchi wote Watanzania wataweza kutambulika, kuanzia yule mwenye siku moja mpaka yule ambaye atakwenda siku yake ya kufariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye suala la *Artificial Intelligence (AI)*. Tuna kila sababu ya kujipongeza sana kuwa na kiongozi imara kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza kusimamia suala hili na kwa uongozi mahiri wa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya *TEHAMA,* kaka yangu Dkt. Nkundwe ameweza kufanya kazi nzuri sana. Ninakumbuka nilisafiri naye kwenda nchini Estonia tulikwenda kujifunza kule kuhusiana na akili umbwe na akaahidi kuja kuandaa kongamano kubwa ambalo litaibua vipaji na kuvitambua vipaji vingi vilivyopo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwamba mwezi Oktoba, tarehe 13 mpaka 17 tulikuwa na kongamano kubwa sana pale Mwalimu Nyerere *Convection Center* na iliweza kuonyesha namna vijana wa kitanzania wako vizuri kwenye suala la *artificial intelligence* kwa maana ya akili umbwe. Tulianza kuwahusisha jamii ya wanawake ambao wanafanya biashara kidigitali na waliweza kuja pale na kuelezea manufaa makubwa sana wanayoyapata kupitia kufanya biashara kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuko hatua kubwa katika matumizi ya akili umbwe. Siku ya pili tuliweza kuwashirikisha vijana mbalimbali wa kike na wa kiume. Wao pia waliweza kuja kuonesha kazi mbalimbali wanazozifanya. Ni furaha iliyoje? Watoto kwenye *level* ya shule ya sekondari waliweza kuja na vifaa walivyovitengeneza na kuonesha namna ambavyo akili umbwe inaweza kufanya kazi. Hata nchi mbalimbali zilizokuja kushiriki kongamano lile hazikutarajia kama Tanzania tuna vijana wadogo *level* ya sekondari wanaweza kufanya mambo makubwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni ubunifu ambao unaendelea kusimamiwa na Dkt. Mkundwe na kuhakikisha kwamba Tanzania nasi hatubaki nyuma. Tunaendelea kuiweka sawa mifumo ya akili umbwe ili iendelee kuleta chachu katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niseme kwamba katika kuona tunaendelea kuboresha mawasiliano nchini, tumeweza sasa kuwa na *satellite* kubwa ambayo kama nchi itakwenda kutuongezea heshima na kutusogeza zaidi katika dunia ya kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanafanyika kwa kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameweza kuruhusu fedha nyingi zinaweza kutumika na miradi mingi inaendelea kufanyika. Haya yote yanawezekana, lakini kubwa na kwa sababu pia tuna Waziri anayesimamia vizuri, kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, anasimamia vizuri kila kitu kinakwenda kama ambavyo kimepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea haya yote sasa naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge. Ninaendelea kuomba ushirikiano baina yenu na sisi Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tunawategemea kwa sababu ninyi ndiyo taswira ya Taifa letu. Wanapoweza kuleta mrejesho wa mawasiliano katika maeneo yenu tunaendelea kuona wapi tuongeze nguvu na wapi tupeleke teknolojia ya juu zaidi, kwa sababu kwenye maeneo ambayo bado tunatumia *2G*, lakini wananchi wake bado hawana simu hizi za kufuta na wao pia tunaamini siku moja wataweza kusogea na kutumia teknolojia ya *3G* na *4G*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wageni waliopo Bungeni jioni hii; kuna Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Mgeni wa Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Bingwa wa Saratani na Vinasaba, kutoka Hospitali ya Taifa – Muhimbili. Karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mhandisi Isack Kamwelwe, wapiga kura wake kutoka Mkoa wa Katavi. Karibuni. *(Makofi)*

Namwita Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Profesa Mkenda na Mheshimiwa Bashe jiandaeni.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili mpango hapa Bungeni. Sisi watu wa afya kwa kweli tunaujadili kwa kujiamini kwa sababu tunaye jemedari wetu ambaye ni Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mtafutaji. Pia, tusisahau ndiye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambaye kwa uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye kila sekta inatufanya Wabunge wa Chama

Cha Mapinduzi tukirudi Bunge la Januari tunakuja tukiwa tumeshinda vijiji kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi afya kama unakumbuka Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alipohutubia Bunge kwa mara ya kwanza hapa, alipofika eneo la afya hasa kwenye eneo la mama na mtoto aliongea kwa kurudia na kusisitiza. Alipoongea hakuishia hapo aliweka shilingi trilioni 6.7 kwenye Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi makubwa yalitokea kwenye eneo hili la afya kutokana na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kutumbukiza shilingi trilioni 6.7; aliipokea hii nchi tukiwa na *CT scan* mbili tu kwenye hospitali za mikoa, lakini leo tunavyozungumza kila hospitali ya mkoa kwenye nchi hii imefungwa *CT scan*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makadirio na maelekezo ya Shirika la Afya Duniani inatakiwa katika kila watu milioni moja pawepo na *CT scan* moja, lakini alichokifanya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya Tanzania badala ya kuwa na *CT scan* moja katika watu milioni moja, leo Tanzania hii kila *CT scan* moja inahudumia watu laki nane. Maana yake Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amevunja ile rekodi ambayo ingetegemewa na Shirika la Afya Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hospitali zetu za kanda zote zina *MRI machine;* hakuna hata hospitali moja ambayo haina. Rais wetu kutokana na uwekezaji mkubwa ambao ameuwekeza kwenye teknolojia, miundombinu, madawa na mambo mengine pamoja na elimu, leo kushuka kule chini, tuliposimama hapa tulitegemewa mwaka kesho tushushe vifo kutoka 556 mpaka 225 na ilitegemewa mwaka kesho, lakini kwa sababu ya uwekezaji huu mkubwa ambao Rais wetu amefanya kwenye Sekta ya Afya tumeshusha vifo mpaka 104. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, kwa muda mfupi ambao Rais wetu amekaa hapa amepunguza vifo vya akina mama kwa 81.2%. Tumebakisha

18% ili kuweza kumaliza vifo vya akina mama moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan siyo hivyo tu, pia wakati anapokea nchi ilikuwa ukienda *Ocean Road* 90% ya Watanzania wanafika *Ocean Road* wakiwa tayari kansa ni zile za kungojea kufa. Maana yake kansa iko kwenye *terminal stage,* lakini kwa sababu ya uwekezaji huu mkubwa wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan wa shilingi trilioni 6.7, leo ukienda *Ocean Road* 78% ya watu wanaokuja wanakuja na kansa katika *stage* za mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye eneo la kansa kwa kuweka *resources* kwenye *infrastructure,* teknolojia na mambo mengine amepunguza vifo kwenye eneo la kansa kwa 78%. Maana yake tulikuwa na 78% ya watu waliokuwa wafe kwa kansa, lakini kwa sababu ya kazi ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan leo watu hao wako na familia zao wanaishi na wanaendelea na maisha ya kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan akiingia madarakani kulikuwa na tiba dawa ambayo ukiwekewa inasaidia kinga zako wewe mwenyewe ziweze kwenda kuua zile seli za kansa, yaani mwili wako unatengeneza chembechembe zinazokwenda kuondoa kansa mwilini. Ilikuwa tukitaka kupata tiba hiyo ni lazima uende Ulaya au India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunavyozungumza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaleta Tanzania hiyo teknolojia. Leo Watanzania hawaendi India na walikuwa wakienda India wanatumia shilingi milioni 100 kutibiwa; leo tunatumia shilingi milioni 10 na Watanzania wanapona hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa pia ukipata kansa labda iko pembeni ya ini kwenye *organ* iliyoko karibu na ini; ukipigwa mionzi unapiga mpaka na ini ambalo halihusiki. Ndani ya nchi hatukuwa na teknolojia ambayo ingesaidia kupiga mionzi tu eneo lile lenye

tatizo na mtu akaondoka maeneo mengine hayajapata madhara. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaleta teknolojia hiyo na sasa Watanzania wanapigwa hapa nchini Tanzania. Ilikuwa wanafuata hiyo teknolojia nje kwa zaidi ya shilingi milioni 90. Leo hapa Tanzania wanatibiwa kwa shilingi milioni 10 na wanabaki hapa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais wetu anapokea nchi hatukuwa na *PET/CT scan.* Kuna mashine ambayo imeunganishwa *PET scan* na *CT scan* kwa pamoja; mashine hiyo ina uwezo wa kugundua kansa ambayo itatokea miaka 10 ijayo. Maana yake ina uwezo wa kuangalia uvimbe na kwenda kwenye seli yako inaangalia kama kuna dalili za kuanza kansa unatibiwa mapema kabla ya kansa kuwa kansa kamili. Hatukuwa na teknolojia hiyo, ukitaka teknolojia hiyo ilitakiwa uende Ulaya au sehemu nyingine. Leo ndani ya Tanzania hii teknolojia hiyo ipo, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaambiwa mpaka jana watu waliotoka nje ya Tanzania kuja kutibiwa kwa maana ya Kenya, Rwanda, Zambia, Comoro na sehemu nyingine kwa mwaka huu wamefika ni 10,931. Maana yake ni nini? Uwekezaji aliouwekeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Sekta ya Afya haujatatua tu matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hawa watu 10,000 walitakiwa watoke Comoro, Zambia na Rwanda waende Ulaya na India. Leo wanakuja karibu hapa Tanzania. Maana yake uwekezaji aliouwekeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Sekta ya Afya umefika mahali ukajaa halafu ukasaidia na majirani zake. Maana yake ameleta *solution* ambayo imevuka mipaka ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo badala ya watu kulipa nauli kubwa kwenda India leo wamekuja, *solution* zao ziko Tanzania. Ninyi ni mashuhuda mliona Spika wa Bunge la Comoro alikuja hapa na juzi walimuona Waziri wa Ulinzi wa Comoro alikuja hapa na wote wanakuja kwa ajili ya kuingia mikataba watu wao watibiwe Tanzania. Maana yake kazi ya huyu Rais ni kubwa kiasi

kwamba siyo tu kwamba inaleta suluhu Tanzania bali inaleta suluhu na nje ya mipaka ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie, tofauti ya Tanzania kwenye Sekta ya Afya na nchi ambazo zimetuzunguka kama Kenya ni moja tu, sisi *public sector* ina nguvu sana. Sisi wakikushindwa *private sector* unaletwa Serikalini unakuja kusaidiwa.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda majirani zetu *private sector* ndiyo ina nguvu kuliko *public sector*. Huyo ndiye Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye tunataka kusema tunaondoka kwenye Bunge hili zawadi ambayo tunatakiwa kumpa tukienda, turudi na 100% ya vijiji Chama Cha Mapinduzi tumeshinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan huyu, ninyi Wabunge ni mashahidi haijawahi tokea kwa wakati mmoja zikagawanywa *ambulance* 727. Tumeshindwa kumaliza *ambulance*. Mpaka jana Mheshimiwa Mzee Lukuvi hapa ndiyo alichukua *ambulance* yake, bado hatujamaliza, zinaendelea kugawanywa. Huyo ndiye Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tulikwenda nae Marekani wakati Rais wa Marekani akikutana na Marais wa Afrika na Marekani walitaka wajenge kituo kimoja cha kansa cha umahiri kwa Afrika kwa ajili ya nchi zote za Afrika. Walikuwepo Marais wengine lakini jinsi ambavyo Rais wetu anajua kucheza tuliibuka kidedea na kituo hicho kinajengwa Tanzania na kinajengwa hapa Dodoma; tayari ujenzi umeanza na mkitaka kutembelea nendeni Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mashine ambayo inaitwa *proton therapy* yenye thamani ya shilingi bilioni 178 na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshakubaliwa na inakuja ndani ya Tanzania kutibu Watanzania na kwa Afrika

tutakuwa ni nchi ya kwanza kuwa nayo. Maana yake Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anapozungumzia *Royal Tour* ya utalii wa kuangalia wanyama, anaupiga mwingi tena kwenye *tour* ya utalii wa tiba ndani ya Tanzania. Anaenda kuigeuza Tanzania iwe ni *hub* ya Afrika kwa maana ya eneo la tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaweza kutokea uvimbe chini kwenye uvungu/sakafu ya ubongo; ilikuwa ukipata uvimbe kama huo inabidi upelekwe India au Ulaya, lakini alipoingia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta mashine na leo tukitaka kutoa uvimbe chini ya uvungu wa ubongo wako tunaingia tu kwenye pua tunakutoa unanyanyuka kwenda kukuta familia yako unaanza kuongoza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa mtu akipata *stroke* inabidi tukufungue kichwa kizima ili tukuhudumie na tufungue fuvu lote, lakini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia amenunua mashine, sasa tunaenda kwenye mshipa mkubwa mguuni halafu tunatembea tunaenda kichwani kwako tunakutibu tunakwambia, rudi na ukaseme Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umeona Tanzania tumekuwa tuna watu wengi wenye vibiongo. Unazaliwa mgongo umepinda unakuwa namna hiyo hiyo na unaishi maisha yako namna hiyo. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amenunua *microscope* maalum yenye thamani ya shilingi bilioni 21 imeunganishwa kwenye mashine nyingine. Ukizaa mtoto mwenye kibiongo unakuja Muhimbili kwa hisani ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunakunyoosha unakuwa kama binadamu mwingine yeyote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kumalizia kwa kusema, ninyi wote mnajua na wengine mko hapa, ugonjwa wa *sickle cell* (seli mundu), ilikuwa ukipata seli mundu inakuwa ni ugonjwa ambao utaishi maisha yako yote. Ni ugonjwa ambao huwezi kufanya kazi. Wengi hawapitishi umri wa miaka 48,

lakini Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, siyo tu amenunua vifaa, lakini ametoa fungu kwa ajili ya kuwatibu watoto bure. Ndani ya Tanzania hii haijawahi tokea ukimzaa mtoto mwenye seli mundu anatibiwa ndani ya Tanzania na anapona na anaishi kama binadamu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu kwenye tiba hii tumekuwa tukitumia uroto, maana yake tunatumia *stem cell,* tunaingia tunaondoa zako tunachukua za ndugu yako halafu tunaingiza zile ambazo hazina, halafu unaendelea, amesema twende kwenye *gene therapy*. Maana yake hata kama unaumwa, sasa tunakuja na teknolojia ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameanza kututayarishia ambayo sasa tunaenda kule kwenye *gene* zako...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** ... ile sehemu ambayo inasababisha itokee hiyo *sickle cell* inaenda inaondolewa halafu unanyanyuka unaendelea na shughuli zako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, tunaye dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, ni jembe limeshika kasi. Nataka kuwaambia tutaenda kuwashangaza kwenye eneo la afya kwa sababu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan yupo na niwahakikishie Wabunge wenzangu, haya ni makubwa. Hakuna sababu ya kumaliza Bunge kesho halafu tukaenda majimboni wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaondoka nikiwa ninajiamini. Waliochukua fomu kutokea vile vyama vingine wanagombea kwenye jimbo langu naenda kuwapokea wote wanarudi CCM halafu tunarudi na 100% ya ushindi na naomba sote tukafanye hilo. Tunyooshe mambo tumalize mambo mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hayo makofi ndiyo maua ya Mama Samia. Namwita Mheshimiwa Profesa Mkenda, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Profesa Mbarawa jiandaeni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Maua mengine ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan yanakuja kwenye elimu. Kwanza kabisa, naomba niunge mkono hoja. Vilevile, niwapongeze sana watoa hoja, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Kamati yetu ya Bunge na Wabunge wote ambao wamechangia katika hoja iliyombele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kueleza kwenye elimu, lakini jambo ambalo limezungumzwa kwa namna moja ama nyingine ambalo linahusisha elimu, ujuzi na ajira, limezungumzwa kupitia Bodi ya Mikopo, mfumo wa elimu na kadhalika. Nitajaribu kulielezea kwa yale ambayo yanafanyika sasa hivi kwa ajili ya kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ingawaje elimu ni kitu muhimu. Unaweza ukahitaji elimu hata kama huhitaji ajira wala kujiajiri. Ukweli ni kwamba wengi wanaosoma, matarajio yao wakimaliza ni kupata ajira. Vijana tulionao ni wengi zaidi, watoto ni wengi zaidi. Huko tunakoenda, kweli tunavyoambiwa *demographic dynamic* yetu kama hatukujipanga vizuri badala ya idadi ya watu tulionao kuwa ni baraka itakuwa ni changamoto moja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kabla sijaeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais na utekelezaji wake katika suala hili, tujue kwamba hapa duniani sasa hivi elimu na ujuzi ni kivutio, siyo cha uzalishaji mali tu katika nchi lakini cha kuvutia uwekezaji. Misamaha ya kodi sawa, miundombinu sawa, huduma za kiuchumi sawa, lakini wataalamu wanasema uwekezaji katika masuala ya teknolojia ya hali ya juu na uwekezaji unaoajiri vijana wengi unahitaji nchi ambayo vijana wake wamesoma vizuri, wana ujuzi mkubwa na hivyo wanaajirika kirahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli changamoto zilizoelezwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba elimu yetu ikidhi matakwa hayo ya kuandaa vijana wetu kwenye ujuzi ni jambo muhimu sana kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tunakumbuka Mheshimiwa Rais wetu alivyokuja kuhutubia Bunge hapa tarehe 22 Aprili, 2021, takribani mwezi mmoja na kitu tu tangu aapishwe kuwa Rais wetu. Katika ahadi alizozitoa kwa Watanzania aliahidi kwamba Serikali yake itapitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2024 pamoja na mitaala kwa ajili ya kuboresha elimu na kuandaa wanafunzi wahitimu wenye ujuzi utakaowawezesha kujiajiri na kuajirika. Baada ya ahadi hii ya Mheshimiwa Rais wetu, kazi imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nieleze kidogo mageuzi haya ya elimu ambayo kwa kweli ni maagizo ya Mheshimiwa Rais wetu na maono yake. Kwenye mfumo wetu na sera na jinsi ambavyo utatupeleka kutatua changamoto hii ya kutoa elimu ambayo wahitimu wanapata shida kujiajiri na kuajirika na hii ni pamoja na mitaala ambayo tumeibadilisha. Tuanze na mfumo wa elimu tulionao sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu unaitwa (1) 7 + 4 + 2 + 3 + maana yake ni kwamba Elimu ya Awali mwaka mmoja, Elimu ya Msingi miaka saba, miaka minne sekondari ya chini, miaka miwili sekondari ya juu, halafu mitatu kuendelea na elimu inayofuata. Ni mfumo wetu huu ambao kuna baadhi ya changamoto nitajaribu kuzieleza ambazo tunajaribu kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa kwenye mfumo huu ni kwamba elimu ya lazima Tanzania tunayoifanya sasa hivi ni miaka saba. Kila mtoto ni lazima kwa amri akae shuleni mpaka amalize Darasa la Saba. Akiondoka shuleni, tunahangaika na mzazi na mtoto na umri wa kuanza shule ni miaka sita. Kwa hiyo, mtoto akianza na miaka sita akimaliza Darasa la Saba ana miaka 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto huyo akiacha shule tutajaribu kumtafuta, kama anataka kwenda sekondari tutapambana na mzazi aende, lakini hakuna sheria inayomlazimisha kusoma, inayomlazimisha mzazi kuendelea kumpeleka shuleni. Kwa hiyo, anamaliza elimu ya lazima akiwa na miaka 13 halafu tunasema elimu hii imwandae kuajiriwa na kuajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yetu hairuhusu kuajiri mtoto wa miaka 13. Kwa hiyo, elimu yetu ya lazima na umri wa kuanza shule kwa kweli haumwandai mtoto kuajiriwa labda aende sekondari, lakini sheria haimlazimishi kwenda sekondari, huu ndiyo mfumo tulionao sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mpya baada ya Sera ya Elimu na Mitaala sasa hivi elimu yetu itakuwa na mfumo ufuatao: huu utaanza kutekelezwa rasmi mwaka 2027/2028, Elimu ya Awali mwaka mmoja, kwa sababu tunajitahidi kusambaza iweze kuwa ya lazima. Sasa hivi ni muhimu lakini hatuwezi kuilazimisha. Elimu ya Msingi itakuwa miaka sita, Elimu ya Sekondari ya chini miaka minne, Elimu ya Sekondari ya Juu miaka miwili au mitatu nitaeleza, na baada ya hapo kwenda kusoma tena miaka mitatu na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Msingi miaka sita, lakini elimu ya lazima sasa itakuwa siyo miaka saba tena, itakuwa ni miaka 10. Maana yake ni kwamba mtoto atakapoanza Darasa la Kwanza itakuwa ni lazima asome amalize Elimu ya Msingi miaka sita na ni amri aendelee kukaa shuleni kuanzia *Form One* mpaka *Form Four*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtoto haendi shule, tunabadilisha sheria, tunahangaika na mzazi tutamtafuta mtoto arudi shuleni asome. Huyu mtoto akianza na miaka sita shule ambayo ndiyo umri wa kuanza Darasa la Kwanza, akimaliza *Form Four* atakuwa na miaka 16. Angalau tumemsogeza karibu zaidi na umri ambao anaweza akajiajiri, kuajiriwa na *norms* za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wenzetu elimu ya lazima ni miaka 10, Kenya sasa hivi nadhani ni miaka tisa. Kwa wastani duniani nchi zote zinakimbilia elimu ya lazima miaka tisa, 10 au 12. Sisi miaka saba kwa kweli tumechelewa sana kusonga mbele huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litaanza kwa wale watoto ambao wako darasa la tatu sasa hivi, ambao wameanza na mtaala mpya. Wakienda darasa la nne, la tano, la sita wamemaliza shule ya msingi. Kwa hiyo, mwaka 2027 wale itakuwa

ni lazima waende *form One* na kuendelea. Ndiyo maana uwekezaji kwenye shule, miundombinu hasa kupitia wenzetu wa TAMISEMI ni mkubwa na utaongezeka kuwa na shule ya sekondari katika kila eneo ambalo mtoto anaweza akatembea na kufika shuleni kusoma ili wote wamalize shule wakiwa na hiyo miaka 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla sijafafanua zaidi nieleze kidogo katika mitaala na hayo ndiyo maono ya Mheshimiwa Rais wetu, maana alisema tufanye elimu tuhakikishe mtoto anaajiriwa. Aliyasema haya kabla hata hajahutubia Bunge hapa, alizungumza tarehe 6 Aprili, 2024 katika Elimu ya Msingi, na hili limezungumzwa humu ndani, Kiingereza kitaanza darasa la kwanza, kitafundishwa kimawasiliano zaidi halafu baadaye ndiyo kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kuanza kukazia kanuni, unamweleza *verb, adverb, noun, past tense, present participle tense*, mtoto anakaa haelewi lakini ukienda sasa hivi kwenda kujifunza Kimasai ukajifunza mawasiliano utaanza kuongea Kimasai. Matokeo yake, mtoto anamaliza darasa la saba haongei Kiingereza. Tunaanza darasa la kwanza na tunabadilisha namna ya kufundisha kimawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lugha sasa hivi kuna *options* unaweza ukaongeza lugha ya kigeni. Ukiacha Kiswahili, Kiingereza unaweza kuongeza Kifaransa kama unataka na walimu wapo na tutajitahidi wawepo. Unaweza ukasoma Kiarabu kama kuna mwalimu utaenda kusoma pale. Unaweza ukasoma Kichina, tumeongeza *options* kwa ajili ya ukalimani, nalo lilisemwa hapa ili watoto wakimaliza waweze kwenda duniani mahali popote kutafuta ajira, lakini Kiingereza bado kitafundishwa vizuri zaidi na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kumaliza Elimu ya Msingi, sekondari inagawanyika mikondo miwili, mkondo wa elimu jumla na mkondo wa elimu ya amali. Amali ni masuala ya kazi. Mafunzo ya kazi ndiyo yale tunayoita sasa hivi ufundi na ufundi stadi. Ufundi ni kama *Technical Secondary School* tunayoizungumzia, ni mambo ya uhandisi. Ufundi stadi ni mafunzo

mengine ya kazi kama mapishi, *sports academy*, *music academy*, *fisheries*, kushona nguo na kadhalika. Kwa hiyo, mafunzo ya amali ni seti kubwa, humo ndani kuna ufundi na kuna ufundi stadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyoongea tayari tumeanza ujenzi wa shule 100 za ziada za ufundi Tanzania. Siyo amali, ni amali ufundi na tumezipeleka kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao katika wilaya zao, *VETA* inajengwa kwa Mheshimiwa Mbunge mwenzake, yeye hana chochote. Yeye tunampelekea *Technical Secondary School*, siyo *secondary school* ya amali tu lakini ni amali ya ufundi. Huyu akimaliza *form four*, mafunzo ya amali ana cheti cha *form four* na ana cheti cha *NACTIVET*, watu wanakiita cha *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kama umejifunza *wiring* unamaliza *form four* tayari unaweza kwenda kazini, unaweza ukafanya *wiring* kwenye nyumba. Umejifunza ufundi magari, tayari unaweza kuingia kufanya shughuli za ufundi magari na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu akimaliza mkondo wa amali, labda niuelezee zaidi, akienda *form five* akasoma miaka mitatu atatoka na *Diploma* na cheti cha *form six*. Kama ilivyokuwa *Dar Tech* leo tunakamilisha taratibu za kujenga *polytechnics*. Moja Mwanza, nyingine Kigoma, nyingine Mtwara, nyingine Zanzibar, hapa Dodoma tumemaliza kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kama ilivyokuwa *Dar Tech*. ya kutoa tu *Diploma* lakini waliomaliza *form four* mafunzo ya amali hasa yale ya ufundi wataenda kule kupata *Diploma* kwa sababu ukweli ni kwamba nchi yetu bado inahitaji sana *technicians*. Tumeona wakati wa kujenga bomba hili kutoka Uganda kwenda huku, viwanda vingi vinapokuja wanasema hapa kwenu tunahitaji *technicians* lakini tunapata shida sana kuwapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nchi imejiandaa kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu kwenda humo. Huyu atakapomaliza anaweza akaenda kufanya shughuli nyingine

zozote mahali popote. Kwa hiyo, hizi *polytechnics* mpya ambazo zipo kwenye *blueprints* tutakamilisha, fedha zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, fedha zimeshatengwa kujenga hizo *polytechnics* nne. Waheshimiwa Wabunge siku moja nitawaalika mje mkaione Shule ya Ufundi Dodoma. Tumeikamilisha tumekabidhi *DIT* lakini ita-*specialize* kwenye *Diploma* tu. Watakaomaliza sekondari za ufundi kwenda kupata *Diploma* na cheti chao cha *Form Six*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hivyo, kama mnavyofahamu sasa hivi kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu mikoa mingine yote ambayo ilikuwa haina kampasi ya chuo kikuu tunajenga matawi ya chuo kikuu. Hata hivyo, kule tutaenda kupeleka *degree* ambazo ni za amali siyo *academic*. Zina mwelekeo wa kuandaa mtu haraka kwa kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Njombe – *UDOM* inakwenda, Singida – *Tanzania Institute of Accounts*, Manyara - Arusha *Institute of Accounts*, Ruvuma hiyo hiyo. Mwanza Chuo cha *ARI*, Kigoma tuna *MUHAS*, udaktari pamoja na kwamba ni *academic* lakini kwa kweli ni amali. Unajifunza huku unatumia *cadaver* kupasua na kujifunza kila kitu, ukimaliza una ujuzi wa kwenda kuanza kazi tofauti na *academic degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwelekeo wote huko tunakoenda huko, Kigoma, Kagera, *University of Dar es Salaam;* Tanga Mzumbe wanakwenda; Katavi, *SUA;* Lindi, *UDSM;* Rukwa tunaenda *MUST* pale Mbeya, yunaenda, Tabora, Shinyanga, Simiyu. Upande wa Zanzibar, *University of Dar es Salaam* imeenda ile *Institute of Marine Science* kwa ajili ya kuipanua kwa sababu hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, kwa upande wa Mtwara vile vyuo viwili vya Ualimu, Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi, navyo vinaunganishwa vinakabidhiwa *MUST Mbeya* kwa ajili ya kuwa kampasi ya chuo kikuu, lakini na yenyewe itakuwa inatoa *degree* za elimu amali na amali ufundi kwa ajili ya kuandaa vijana wetu kwenye ajira. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni matunda ya maono ya Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu tusipoanza sasa hivi *population dynamics* ya nchi yetu na *Sub-Suharan Africa* huko mbele kwa kweli hali ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojiandaa hivi kwa mfumo wetu wa elimu, dunia itakuwa ni uwanja wa ajira kwa vijana wetu. Hata wakati wawekezaji wanakuja hapa, vijana wetu wanaweza wakatoka kwenda kupata ajira mahali popote duniani, maua yake Mheshimiwa Rais wetu kwa kuliona hili mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie, baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyotoa hapa Bungeni, Umoja wa Mataifa wakatangaza Mkutano Mkuu wa Viongozi wa Nchi wa Elimu Duniani. Walivyokuja kutuambia, tukasema mnataka kudandia treni imeshaanza mwendo, tutakwenda na ninyi lakini tutatangulia. Afrika mwaka huu ni mwaka wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona mazungumzo haya haya ambayo kwa kweli sisi tayari tumeshajiandaa, wote wanasema tujiandae kuongeza ujuzi katika elimu jambo ambalo Mheshimiwa Rais wetu alishatoa maelekezo, utekelezaji umeanza, tunamshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarawa na Mheshimiwa Bashungwa ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango. Pili, natumia nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawapongeza sana Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa *document* waliyoileta

mbele yetu katika Bunge hili ikiwa ni Mpango wa mwisho kabla ya kuwa na Mpango wa Miaka 25 inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia baadhi ya maeneo. kwanza, natumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri na maoni yao. Mengi tutaendelea kuyafanyia kazi polepole kadri ambavyo Mwenyezi Mungu anatujaalia na uwezo wa kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani, ni Bunge hili hili ndiyo liliiomba Serikali ianze jitihada za kubadili bajeti ya Wizara ya Kilimo. Maeneo makubwa ambayo Bunge hili lilishauri ni kuwekeza kifedha kwenye maeneo ya utafiti, uzalishaji wa mbegu, ugani, tuanze kutoa huduma za umwagiliaji, tuhangaike na tatizo la upotevu wa mazao, tufungue masoko na kuwahakikishia wakulima wanapata masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitisha bajeti ya kwanza kutoka shilingi bilioni 294 kwenda shilingi bilioni 750, ukuaji wa sekta ya kilimo ulikuwa 2.7%. Leo tunapoongea mwaka 2023/2024 ukuaji wa sekta ya kilimo umefika 4.2%. Wakati tunaanza utekelezaji wa bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Sita, uzalishaji wa chakula katika nchi yetu ulikuwa ni jumla ya tani milioni 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 mabadiliko yaliyofanyika kipindi cha miaka miwili uzalishaji wa chakula umefika tani milioni 22, asilimia 128. Lengo letu la mpango wa miaka mitano kwa mwaka 2025/2026 tufike asilimia 130 ya *food security* katika nchi yetu. Tutafikia lengo hili mwaka mmoja kabla ya mwaka ambao mpango ulituwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ninataja hizi takwimu ili ziweze kukaa kwenye kumbukumbu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge tuna matamanio, nami nayaunga mkono sana kwamba ni lazima fedha za Serikali ziwekezwe katika sekta hii. Hii ni kauli ya Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania na matamanio yenu na ndiyo sekta iliyoajiri watu

wengi. Mwaka 2021/2022 *export value* ya sekta ya kilimo ilikuwa ni Dola bilioni 1.2, mwaka 2023/2024 tumefika Dola bilioni 2.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tumekuwa tukijadili suala la tija, uzalishaji wa zao la mahindi mwaka 2021 wastani *per hector* ilikuwa ni tani 1.9. Leo tunamzungumzia mkulima mdogo, kwa takwimu za msimu wa kilimo ulioisha tumefika *per hector* tani 2.5, lengo letu ni kufika wastani wa tani 4.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mazao ya kibiashara, wakati tunaanza bajeti ya kwanza uzalishaji wetu wa zao la kahawa ilikuwa ni wastani wa tani 65,000, mwaka huu uliokwisha tumefika tani 85,000. Bei ya mkulima imetoka wastani wa shilingi 700 mpaka 1,000 hadi kufika wastani wa shilingi 6,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilitolee mfano ni tumbaku. Mwaka 2021 tulikuwa tunazalisha wastani wa tani zisizozidi 60,000 mwaka 2023, msimu wa kilimo uliokwisha tumezalisha tani 120,000 na Tanzania kuwa *recorded* ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa tumbaku Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mkulima imeongezeka kutoka wastani wa dola 1.6 mpaka wastani wa dola 2.2. Hatua hizi tulizofikia ni za muda mfupi. Sote tunafahamu matumizi yetu ya mbolea. Mwaka 2021 tulikuwa tunatumia tani 360,000, mwaka huu msimu wa kilimo uliokwisha nchi yetu imetumia jumla ya tani 920,000 za mbolea. Sababu ni moja, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia alivyoamua kuweka ruzuku kwenye bei ya mbolea. Sasa tumeanza kuweka ruzuku kwenye eneo la mbegu na tumeanza na zao la kwanza la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anatoa hotuba hapa alituambia haiwezekani tukabadili sekta hii ya kilimo bila kuwekeza katika umwagiliaji. Nami natumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na ninalihakikishia Bunge lako Tukufu na Watanzania kwamba katika *Vision 2025 - 2050* inayokuja, moja ya sekta iliyopewa kipaumbele ni sekta ya kilimo. Tume-*develop masterplan* ya 2030 – 2050, yeyote atakayekuja

katika nchi hii mpaka mwaka 2050, kuna *clear vision*, *clear plan* na *resource allocation* mpaka mwaka mwaka 2050 katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhamira ya Serikali iliyoko madarakani. Utumiaji wa mbolea kwa wakulima wetu *per hector* tulikuwa *the lowest* kwa *SADC*. Tulikuwa na wastani wa kilo 15, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi anafahamu, msimu wa kilimo uliopita wastani wa matumizi ya mbolea kwa wakulima yamefika *per hector* kilo 24. Malengo yetu tunatakiwa kufika kilo 50, ndiyo tuliyojiwekea 2025/2026 na ninaamini tutafikia huko ambako tunataka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ilikuwa ina tatizo la *extension services* kwa kipindi cha miaka miwili, leo kila halmashauri imepelekewa mashine ya kupimia afya ya udongo na imekuwa huduma ya bure. Suala la *soil health* katika nchi yetu, siku zote lilikuwa ni *donor funded*. Kwa mara ya kwanza miaka hii miwili, mikoa 26 ya Tanzania Bara, mikoa 18 zoezi la upimaji wa afya ya udongo limekamilika, tumebaki na mikoa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatupeleka kwenye hatua gani? Tumejiwekea lengo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu 2025/2026 kupiga marufuku matumizi ya mbolea za *generic*. Haya maneno *DAP, Urea*, kuanzia 2025/2026 tunaenda kutumia mbolea kutokana na mahitaji ya afya ya udongo ya eneo husika na ekolojia inayohusika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la umwagiliaji, na nimesikia Mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, nami nawaelewa matamanio yao, tunataka matokeo leo kwenye eneo la umwagiliaji. Nataka ku-*convince* wenzangu, toka tunapata Uhuru mpaka mwaka 2021/2022, tulikuwa na mtandao wa umwagiliaji ambao ulikuwa ni jumla ya hekta 600,000 na kidogo karibu laki saba. Leo ndani ya miaka miwili tunatekeleza miradi 700 yenye jumla ya hekta 520,000, lakini miradi hii ni ya namna gani? Siyo miradi ya mifereji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tusirudie makosa ambayo tumewahi kufanya huko

nyuma ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji ya mifereji ambayo mkulima anamwagilia masika badala ya kuzalisha mara mbili au mara tatu. Taifa hili lilikuwa halina *feasibility study* na *detailed design* ya mabonde yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kutoa mfano mdogo, mwishoni mwa miaka ya 1960, Kadinali Rugambwa, Askofu Kibira na Sheikh Suleiman wa Kagera walifanya *feasibility study* na *detailed design* ya Bonde la Mto Ngono. *Document* tuliyoenda kuitumia sisi Wizara ya Kilimo ilifanywa na wazee hawa ambapo tumeichukua *document* ile kuifanyia *review* na imekamilika na sasa tunatangaza Mradi wa Ngono. Hatuwezi kuujenga Mradi wa Ngono kwa mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Mradi wa Rufiji. Rufiji Chini baada ya Mwalimu Nyerere, tunatekeleza miradi ya mabwawa mawili yenye jumla ya gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 220. Hatuwezi kujenga kwa mwaka mmoja, haiwezekani. Tunajenga Bwawa la Msagali ambalo ndilo litakuwa bwawa kubwa la kilimo nchi hii lenye *cubic metre* 92,000,000 na tunatumia zaidi ya shilingi bilioni 22, hatuwezi kulijenga kwa mwaka mmoja. Miradi yote hii tumemaliza upembuzi yakinifu wa Bonde la Lukuledi, tumeanza kutangaza miradi. Tutajenga bonde lile kwa miaka mitatu mpaka mitano kukamilisha maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunamaliza *feasibility study* ya Bugwema; Mradi huu wa Bugwema aliuanza Baba wa Taifa. Namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Muhongo na Mheshimiwa *Eng*. Chamuriho, baada ya kwenda kutembelea kule kukuta mabomba, nikauliza tatizo ni nini? Kwa nini Mwalimu alikwama kwenye huu mradi wa kutumia maji ya Ziwa Victoria? Tuipongeze sana Serikali, nami nampongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuyatumia maji ya Ziwa Victoria, inahitaji roho ngumu. Leo tunaenda kutekeleza Mradi wa Bugwema ambao aliuanza Baba wa Taifa ukaishia njiani. Miradi hii inahitaji fedha. Leo tunaanza kutekeleza mradi wa mabwawa matano, kila siku tunalalamika mafuriko ya maji hapo karibu na

Chalinze Nyama ambapo ili tuyaondoe mafuriko yale, tunahitaji kujenga mabwawa matano mpaka Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha kutoka *World Bank* dola 52,000,000 ambazo tunaenda kuziingiza kwa ajili ya kujenga hayo mabwawa matano. Miradi hii haiwezi kwisha kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu hili lilifanya mabadiliko ya Sheria ya *Export Levy*. Mheshimiwa Rais alianza kutoa ruzuku, na ninavyoongea hivi sasa, msimu huu, zao la korosho litaenda kuvunja rekodi na historia ya nchi hii. Tunatarajia kuzalisha jumla ya tani 500,000, mpaka leo minadani ndani ya mwezi mmoja mauzo yamefika shilingi bilioni 924. Haya mabadiliko hayawezi kutokea siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebadili mfumo wa kuuza kahawa na kakao. Kakao ya mkulima ilikuwa inanunuliwa shilingi 3,000/=. Mabadiliko yaliyofanyika ndani ya miaka miwili, leo kakao inanunuliwa zaidi ya shilingi 25,000/= mpaka shilingi 30,000/= kwa kuwaondoa watu wa kati na tunatumia Mfumo wa *TMX* na uzalishaji umefika zaidi ya tani 14,000 ndani ya kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, uwekezaji kwenye eneo la kilimo siyo jambo la muda mfupi. Siyo sawasawa na ujenzi wa darasa, haifanani kabisa, ni *long term investment* na ni lazima kama Taifa tuwe na uvumilivu wa kuwekeza kwa muda mrefu kwenye sekta ya kilimo ili tuanze kupata matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nataka kutumia Bunge hili Tukufu na mbele ya Watanzania, mimi sio mzoefu sana Serikalini, wala sio mzoefu sana ndani ya Bunge. Nina *term* mbili, lakini kuwa na kiongozi ambaye anasikiliza na anatoa fursa ya kufanya maamuzi magumu, *decision* ambayo ameizindua mwezi wa Nane ya kuanzisha *Mechanization Centre* katika nchi hii kwa ajili ya wakulima wadogo, Taifa letu siku zote tumekuwa tukihubiri kwamba wakulima wamiliki trekta. Mkulima wa Tanzania ni nani? Anamiliki wastani wa hekta moja ambayo ni

ekari 2.5, huyu hawezi kumiliki trekta la shilingi milioni 70, au shilingi milioni 80, ni kumtia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua gani? Mheshimiwa kaenda India, karudi hapa, kazindua mradi wa trekta 10,000, *power tiller* 10,000 na kuanzisha *Mechanization Centre* katika maeneo ya uzalishaji ambayo wakulima wadogo watakuwa wanakodi trekta kwa bei ya ruzuku isiyozidi shilingi 40,000 kwa ekari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayofanyika na hivi ninavyoongea kwenye eneo la ukanda la pamba tumeshasambaza jumla ya trekta 400 na hivi sasa tunafanya utaratibu wa kupeleka Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Rukwa trekta zaidi ya 100. Tunaanza kupeleka *combine harvester* na *power tiller* kwenye mabonde ya Mbarali. Haya yanahitaji kuchukua muda na sisi sote tuweze kufanya hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia, leo hii Serikali inampatia mkulima ruzuku ya mbegu, Serikali inampatia mkulima ruzuku ya mbolea, Serikali imepeleka magari, pikipiki na mashine za kupimia afya katika ngazi ya halmashauri, lakini mkulima soko liko wapi? Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katoa idhini ya *NFRA* kuwa mnunuzi mkubwa wa mazao ya mpunga na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto, haiwezekani tukakosa changamoto. Changamoto ya kwanza ambayo tumekutana nayo mwaka huu ni maghala, uwezo wa uhifadhi wa *NFRA*. Ni jukumu letu kama Serikali na tumeongea na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunaweka kwenye bajeti ya mwaka kesho kuongeza uwezo wetu wa uhifadhi. Kwa msimu wa mwaka 2023 na mwaka 2024, *NFRA* kanunua jumla ya tani 820,000 za mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizokuwa *allocated* inabidi tufanye *reallocation* ndani ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo mwezi Desemba ili tupate fedha za ziada tuweze kuisaidia *NFRA* iweze kuendelea kununua mahindi ya wakulima kwa sababu bila ya kuwahakikishia soko la mazao yao, wakulima hawa watakuwa

hawana mahali pa kupeleka. *NFRA* ikiondoka sokoni, bei ya mahindi itarudi shilingi 200, au shilingi 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutumia Bunge lako Tukufu kuwaambia wakulima, *NFRA* haitofunga mlango, tutahangaika na namna ya kupata fedha lakini mazao ya wakulima yataendelea kununuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *integration*, Waheshimiwa Wabunge wameongea sana kuhusu ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Wizara ya Mifugo. Kila bwawa linalojengwa na Wizara ya Kilimo, lina matoleo na *water trough* kwa ajili ya mifugo. Sasa hivi tunafanya pamoja na Wizara ya Maji kwa ajili ya kuingiza *components* ya *irrigation* kwenye kuyatoa maji Ziwa Victoria kuyafikisha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutayatumia maji yale na ile *network* itakayobeba maji kutoka ziwani kwa sababu kilimo hakihitaji maji yaliyosafishwa, sisi tunahitaji *raw water* kama ilivyo. Tumeshaanza kufanya *survey* katika Mkoa wa Simiyu ili ku-*link* katika mradi ulioko Mkoa wa Simiyu uweze kuhudumia maji ya kunywa, lakini vilevile uweze kuhudumia umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imejadili Luiche miaka nenda rudi, Mheshimiwa Makamu wa Rais akiwa Waziri wa Fedha, kwa mara ya kwanza tumekaa tunasubiri hela ya Kuwait, Mheshimiwa Dkt. Samia akasema hamna sababu ya kusubiri hela ya Kuwait, tangazeni mradi. Mkandarasi anajenga Luiche, mradi ambao toka Serikali ya Awamu ya Kwanza ulikwama, mradi wa Mkomazi, sasa hivi kuna Mkandarasi anajenga Mradi wa Mkomazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mkomazi hauwezi kwisha kwa mwaka mmoja au miwili, miradi hii itachukua zaidi ya miaka miwili, au miaka mitatu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe, malizia.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka tu kukisema, lengo letu kama Serikali ni kuhakikisha *investment* ya *irrigation* inafika shilingi trilioni moja kwa mwaka. Huu ndiyo mpango wa Serikali na kwenye *masterplan* inaonesha *one trillion for ten years* ili tuweze kufika angalau 50% ya ardhi inayotumiwa na wakulima kwa ajili ya kutumika kwa ajili ya umwagiliaji. Haya yote yanahitaji *patience*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, matamanio ya kila Mheshimiwa Mbunge kama Wizara na Serikali tunayafahamu. Tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha tunafikia matarajio ya Watanzania. Sekta hii ilipokuwa, siyo ilipo leo. Juzi Mheshimiwa Rais akiwa Marekani, Tanzania imekuwa *recognized* na kasomeni kwenye *Journal* ya *African Development Bank* kwamba ni *modal* ya *transformation* ya *agriculture* katika *Southern Saharan*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia mkutano huo, tumepata dola 130,000,000 kwa ajili ya mradi wa vijana na akina mama. Namshukuru sana na ninampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kagera na ninawaomba Wakuu wa Mikoa wengine waige mfano wa Mheshimiwa Fatma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye *issue* ya *value addition*. Ninawahakikishia, Serikali imeweka fedha kwenye Mradi wa Maranje shilingi bilioni 10, tumeshapeleka shilingi bilioni saba, tumeshaanza kujenga viwanda vya ubanguaji wa korosho. Sasa hivi Serikali inapiga marufuku *export* ya *pyrethrum raw* kwenda nje, viwanda tunavyo, vina uwezo wa ku-*process* tani 12,000, kuanzia mwaka kesho hakuna *pyrethrum* itakayokwenda nje ya nchi hii ambayo haijaongezwa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hatua tunachukua, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Morogoro, tuendelee kuisukuma Serikali nami ninakubaliana nao kabisa katika matamanio yao. *Feasibility study* ya *Kilombero Basin* inaendelea, itakamilika mwaka huu na mwaka huu itatangazwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na tutaanza ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia tu kwa kumshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amekuwa msikivu yeye na Wizara yake. Changamoto za *resources* zipo, lakini tunaenda kukaa, tunaongea na tunagawana kasungura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hiyo inaitwa jaza, ujazwe. Mheshimiwa Profesa Mbarawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Bashungwa, halafu jiandae Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge letu Tukufu nami kuweza kuchangia hoja hizi mbili zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Prof. Kitila pamoja na timu yote ya wataalamu kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutayarisha hoja zetu hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza vizuri, kutusimamia vizuri na kutoa kipaumbele cha kipekee kwa miradi ya mikakati kwa sekta ya uchukuzi, kwani tunafahamu sekta ya uchukuzi ni sekta wezeshi kwa sekta nyingine zote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natumia fursa hii kuwashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, na michango yote tumeichukua na tunaenda kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja iliyoko mbele yetu hapa ya Mpango, imezungumzwa vizuri kuhusu mipango mbalimbali inayohusu miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Mpango ambao umeeleza kwa kina kabisa ilikuwa ni Mradi wa Reli ya Kisasa *(SGR)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba Mradi wa *SGR* unatengenezwa au unajengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa kutoka Dar es Salaam – Mwanza yenye urefu wa kilometa 1,200. Kipande hiki cha kutoka Mwanza – Dar es Salaam au Dar es Salaam – Mwanza kinagharimu takribani shilingi trilioni 16.97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umegawanyika katika vipande vitano, kipande cha kwanza ni kutoka Dar es Salaam – Morogoro chenye urefu wa kilometa 300 na ujenzi umefikia 99% na kwa sasa mradi umeanza kufanya kazi na sote tunafaidi matunda ya usafiri wa *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha pili ni kutoka Morogoro – Dodoma chenye urefu wa kilometa 422 na mradi umefikia 98.6% na sasa mradi unatoa huduma na sote tumeanza kufaidi matunda hayo kutoka Dar es Salaam – Dodoma tunakwenda kwa kutumia treni za *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha tatu ni kutoka Dodoma – Tabora chenye urefu wa kilometa 368, mkandarasi yuko *site* na mradi umefikia 14.39%. Kipande cha nne ni kutoka Tabora – Isaka chenye urefu wa kilometa 165 na kazi imefikia 5.63%, Mkandarasi yuko *site*. Kipande cha mwisho ni kipande cha kutoka Isaka – Mwanza ambacho kina urefu wa kilometa 341 na mkandarasi amefikia 66% na sasa yuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mradi huu umegawanyika kwenye awamu mbili, awamu ya kwanza ni kutoka Dar es Salaam – Mwanza na awamu ya pili ni kutoka Tabora – Kigoma. Kipande hiki kimegawanyika katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni kutoka Tabora – Kigoma chenye urefu wa kilometa 506, ujenzi umefikia 4.9% na Mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni kutoka Uvinza – Msongati – Gitega – Burundi ambayo ina urefu wa kilometa 367, hatua tuliyofikia ni hatua ya manunuzi na tunaamini itakapofika mwisho wa mwezi wa Desemba, mkandarasi atakuwa amepatikana kwa ajili ya kipande hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ni mara ya kwanza Mheshimiwa Rais anaitoa reli nje ya mipaka ya nchi yetu, reli ya *SGR*, tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais. Jumla ya kilometa 1,560 za ujenzi wa *SGR* zimeanzishwa na kutekelezwa ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo hii inafanya iwe sawa na 68.4% ya ujenzi wa Mradi wote wa *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna budi kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo kubwa. Gharama ya mradi huu wote ni shilingi trilioni 23.3 ambazo tunaendelea kutekeleza. Kwa kipande cha kwanza kutoka Dar es Salaam – Mwanza na maeneo mengine, tayari shilingi trilioni 10.53 zimetumika, tumewalipa Wakandarasi kutokana na *certificates* mbalimbali ambazo wamewasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha kipande cha kutoka Dar es Salaam – Dodoma chenye urefu wa kilometa 722 ambazo imejumlisha njia kuu pamoja na njia za kupishana. Hivi sasa tunavyozungumza sote tumeona Reli ya *SGR* inasafiri kutoka Dar es Salaam – Dodoma kwa masaa sita. Leo tunavyozungumza, tunazo *route* nne kwa siku, tunaamini mwakani tutakuwa tunaenda zaidi ya *route* sita kwa siku. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kila baada ya masaa mawili, kutakuwa na treni kati ya Dar es Salaam – Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendea kazi, jambo moja ni kujenga njia ya treni; jambo la pili na muhimu ni kuwa na vitendea kazi. Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya manunuzi ya vitendea kazi mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumenunua mabehewa ya mizigo 1,430 ambayo awamu ya kwanza itawasili mwezi Desemba mwaka huu, pamoja na mwakani. Baada ya kuwasili mabehewa hayo, tutafanya majaribio na baada ya hapo tutaanza kazi ya kusafirisha mizigo kati ya Dar es Salaam na Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali ya Awamu ya Sita imenunua seti za treni za kisasa ambazo tunaziita mchongoko. Treni sita zimefika hapa nchini na zimeanza kufanya kazi. Mwezi huu hivi ninavyozungumza tutapokea treni mbili na baadaye treni mbili za mwisho zitapokelewa mwezi Desemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumenunua mabehewa 89 pamoja na vichwa vya treni 17 ambavyo vimeanza kutoa huduma kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Gharama ya vitendea kazi vyote hivi ni takribani shilingi trilioni 1.147.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujua umuhimu wa sekta binafsi, Serikali ilifanya mabadiliko kupitia Bunge lako tukufu, kubadilisha Sheria ya Reli Na. 10 ya Mwaka 2017, ili kuruhusu *private sector* kwa kutumia utaratibu wa *open access.* Kuanzia mwakani tutaruhusu *private sector* wenye vichwa vyao na mabehewa yao kuja kuwekeza kwenye mitandao yetu ya *SGR* pamoja na *meter gauge*. Hii tutaitumia reli yetu kikamilifu, pia, itakuwa na ufanisi mzuri na Shirika litapata mapato zaidi kuliko tunavyofanya kazi hivi kwa kutumia vitendea kazi vya *TRC* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanza safari za reli kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Kabla ya safari ya Dar es Salaam na Dodoma kuanza Watanzania walikuwa wanatumia kati ya saa saba mpaka tisa kusafiri kati ya miji hii miwili. Leo hii tunapoongea Watanzania wanatumia kati ya saa nne mpaka tatu kwa kutumia *SGR.* Wale wanaopanda *express train* wanatumia saa tatu na wale wanaopanda treni ya kawaida wanatumia saa nne. Kutoka saa tisa mpaka saa tatu hili ni jambo kubwa, hatuna budi kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafirishaji wa abiria, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2024 shirika limeweza kusafirisha abiria 842,853 kwa kutumia *SGR.* Hii ni sawa na wastani wa abiria 700,000 kwa kila siku wanaosafiri kwa kutumia njia ya *SGR* kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo makubwa yamepatikana. Tangu kuanza kutumika kwa *SGR* tarehe 14 Juni, 2024 hadi Oktoba, 2024, takribani shilingi bilioni 22.38 zimekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, tumeona mafanikio makubwa mpaka sasa. Wafanyakazi wapatao 940 wameajiriwa na reli yetu ya kisasa kwenye huduma za *SGR*. Tunategemea itakapofika mwisho wa mradi huu, hasa kati ya Dar es Salaam na Dodoma, wafanyakazi 2,460 wataweza kufanya kazi kwenye reli yetu ya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepata mafanikio makubwa kwenye utunzaji wa mazingira. Uendeshaji wa *SGR* unatumia nishati ya umeme na kwa hiyo, umesaidia sana kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na pia tumefanikiwa kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida treni hizi zinatumia mafuta ya *diesel,* lakini *SGR* yenyewe inatumia umeme na umeme wenyewe ni kutoka kwenye maji ambayo yanapatikana hapa nchini. Kwa hiyo, tume-*save* fedha nyingi sana za kununua mafuta ya *diesel* kwa ajili ya kuendesha reli hii ya kisasa kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Mwaka 2023, mwezi Desemba, katika Bunge lako tukufu tulipitisha mkataba hapa kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kati ya gati namba tano mpaka namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuripoti mafanikio yaliyopatikana kutokana na uwekezaji wa *DP World* katika gati namba tano mpaka namba saba. Mara baada ya *DP* kuanza kazi Bandari ya Dar es Saalam amewekeza dola za kimarekani milioni 250, sawa na shilingi bilioni 675 katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, *DP World* imenunua mitambo ya kisasa yenye thamani ya shilingi bilioni 214.45.

Mitambo hii kama hatukuwekeza au kama hatukumleta *DP World* tusingeweza kuinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo *DP World* amewekeza ni ukarabati wa mitambo iliyokuwa inatumiwa na *TPA*. *DP World* katika kipindi alichokuwepo cha miezi mitano ameweza kufanya usanifu na usimikaji wa mifumo ya kisasa ya TEHAMA na sasa kazi inafanyika Bandari ya Dar es Salaam katika maeneo hayo niliyoyataja, yaani gati namba tano mpaka namba saba, ufanisi wa utendaji umekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwekezaji wa *DP World* tumeweza kushuhudia mafanikio yafuatayo kwenye Bandari ya Dar es Salaam katika gati namba tano mpaka namba saba. Wastani wa muda wa meli kukaa sasa umepungua. Kabla ya uwekezaji wa *DP World* meli zilikuwa zinakaa nangani kwa siku 46, lakini leo hii tunapozungumza, meli za makasha hazikai nangani tena. Ikiingia meli ya makasha inakwenda moja kwa moja gatini. Kwa meli za mizigo ya kichele, zamani zilikuwa zinakaa siku 46, leo hii meli hizo zinakaa siku 12 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa meli za mizigo mchanganyiko, zamani zilikuwa zinakaa nangani siku 46, lakini leo hii meli zinakaa nangani kwa siku 10 tu. Pia, tumeona kuna ongezeko kubwa la idadi ya makasha baada ya uwekezaji wa *DP World.* Kampuni ya *DP World* imeongeza ukuaji wa idadi ya makasha wastani wa 38.17% ikilinganishwa na wakati wa *TPA* ambayo yenyewe ilikuwa, wastani wa ongezeko la makasha ni 9.8%. Hii imesababisha wastani wa idadi ya makasha kwa mwezi kufikia 17,626 ikilinganishwa na makasha 12,727 wakati *TPA* inafanya kazi kwenye gati namba tano mpaka namba saba ya Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ongezeko la shehena mchanganyiko. Kampuni ya *DP World* imeongeza kiasi cha shehena kinachohudumiwa hadi kufikia wastani wa tani 168,336 kwa mwezi ikilinganishwa na tani 141,889 wakati magati hayo matatu yalipokuwa yanahudumiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ongezeko la shehena, kutokana na uwepo wa *DP World,* mapato ya *wharfage* yameongezeka kwa wastani wa 9.9% kwa kipindi cha miezi mitano ikilinganishwa na wakati wa …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarawa, hebu rudia tena. *Wharfage* anakusanya nani?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, *wharfage* inakusanywa na *TPA,* wao ndio wenye mamlaka kisheria. Bunge lako Tukufu lilipitisha hapa kuiruhusu *TPA* kukusanya *wharfage* kwa ajili ya uendelezaji wa Bandari za Tanzania. Kupitia ongezeko la shehena kutokana na uwepo wa Kampuni ya *DP World,* mapato ya *wharfage* yameongezeka kwa wastani wa 9.9% kwa kipindi cha miezi mitano ikilinganishwa na 6.5% kwa kipindi kama hicho, wakati magati hayo matatu yalipokuwa yanafanya kazi chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kubadilisha shughuli ya uendeshaji wa gati namba tano mpaka namba saba kuwa chini ya Kampuni ya *DP World,* matumizi ya uendeshaji wa gati namba tano mpaka saba yamepungua kwa 2.7% kwa kipindi cha miezi mitano ikilinganishwa na wakati magati hayo yanasimamiwa na Mamlaka ya Bandari, matumizi yalikuwa yanaongezeka kwa 15.1%. Wakati wa *DP World* matumizi yamepungua, lakini wakati wa *TPA* matumizi yalikuwa yanaongezeka kwa 15.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita, kutoka mwezi wa Februari hadi Septemba, Serikali imepata jumla ya shilingi bilioni 325.3 ikiwa ni mapato yatokanayo na shughuli za ufanyaji kazi wa *DP World* katika gati namba tano mpaka namba saba. Hii imetokana na makusanyo ya pango *(land rent),* tozo ya mrahaba, pamoja na tozo ya *wharfage* ambayo yenyewe inakusanywa na *TPA.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufanisi huo uliosababishwa na kuja kwa Kampuni ya *DP World,* sasa Mamlaka ya Bandari inatekeleza miradi yenye thamani ya shilingi trilioni 1.22. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mradi wa ujenzi wa kituo cha kupokea mafuta ambao ujenzi unaendelea na unatekelezwa kwa shilingi bilioni 578, mkandarasi yuko *site*. Ujenzi wa bandari ya kisiwa, mgao unaendelea na mkandarasi yuko *site* na unatekelezwa kwa shilingi bilioni 434.5. Ujenzi wa Gati la Malindi *Wharf* hivi karibuni tutapata mkandarasi, kwa ajili ya ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 500 ambalo litagharimu shilingi bilioni 540.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Bandari ya *Mbamba Bay* unaendelea, mkandarasi yuko *site* na mradi huu utagharimu shilingi bilioni 80. Ujenzi wa Bandari ya Kemondo na Bukoba Mjini, mkandarasi yuko *site* na unagharimu shilingi bilioni 40. Mwisho ni Mradi wa Mwanza *South* ambao unaendelea, mkandarasi yuko *site* na mradi huu unagharimu shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hii isingeweza kutekelezwa kama hatukuweza kumleta *DP World* kwenye Bandarai ya Dar es Salaam. Matokeo yake leo miradi hii mingi ya kimkakati inatekelezwa kwa ufanisi na kwa kasi ambayo tumejipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niongelee kuhusu suala la *TAZARA*. Reli ya *TAZARA* ni muhimu sana, ni reli inayounganisha Tanzania na Zambia. Serikali ya Tanzania, Zambia na China tulisaini mkataba mwezi Septemba, kwa ajili ya kumpata mwekezaji ambapo Kampuni ya CCC iliteuliwa kufanya kazi hiyo. Hivi ninavyozungumza leo, timu yetu ya wataalam kutoka Tanzania na Zambia wako Dar es Salaam, kwa ajili ya kuzungumza kuhusu *concession agreement*. Tunaamini wiki inayokuja timu ya wataalam Watanzania na Zambia…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watakaa pamoja na timu kutoka China.

**MWENYEKITI:** Mnayo nafasi tena kuja kutoa majibu kwenye hili. Ahsante sana.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Innocent Bashungwa, jiandae Mheshimiwa Awesso, kisha Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Mavunde watafuatia.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja mbili ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Daktari Mwigulu Lameck Nchemba na Mheshimiwa Profesa Mkumbo. Naomba nianze kwa kuwapongeza kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa mwelekeo mzuri wa mjadala ambao tumekuwanao wiki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango na ushauri mzuri kwa Serikali. Pia nawapongeza Mawaziri wenzangu kwa ufafanuzi ambao wameutoa toka kwenye hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge walijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani zangu za kipekee kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa na kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuendelea kuiwezesha Wizara ya Ujenzi kutimiza wajibu wake wa kujenga barabara, madaraja, vivuko pamoja na nyumba za watumishi kupitia *TBA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto ambazo mmetueleza kupitia michango yenu, yapo mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kupitia sekta ya ujenzi. Wakati wa kipindi cha bajeti, kulikuwa na mvua kubwa ambazo zilikuwa zinaendelea za *El-Nino* pamoja na kimbunga Hidaya, lakini kupitia michango yenu mizuri tulikuwa wasikivu tukakubaliana kwamba, wakati wa mvua turudishe mawasiliano ya muda ili wananchi wetu kwenye majimbo yetu, kwenye wilaya zetu na mikoa, waendelee kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini

mvua zitakapoisha turudishe miundombinu ya kudumu kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza niwashukuru kwa ushirikiano ambao mlitupatia kipindi kile kigumu cha mvua za *El-Nino* na kimbunga Hidaya. Namshukuru sana Rais wetu Dkt. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, tayari ametuwezesha. Baada ya mvua kuacha, tunazo shilingi bilioni 868.56 kwenda kujenga madaraja na makalavati kwenye maeneo yote ambayo yaliharibiwa na mvua za *El-Nino*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hili, tuliona tukitumia hizi shilingi bilioni 868.56 kwenda kukwangua barabara, mvua zitakaponyesha tatizo litarudi pale pale. Kwa hiyo, tumeona tutumie fedha hizi shilingi bilioni 868.56 kwenda kujenga makalavati na madaraja kwenye maeneo ambayo yameharibika ili mvua zitakaponyesha madaraja haya yaweze kutumika. Vilevile, tutakapojenga kiwango cha lami, madaraja na makalavati haya ni viwango vikubwa ambavyo hata ujenzi wa lami hatutahitaji kujenga madaraja mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana, mmefuatilia kwa jitihada kubwa kuhakikisha tunafikia hatua hii. Kipekee tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hizi shilingi bilioni 868.56 ni fedha za dharura ambazo tulikuwa hatujajipanga kwa kuwa hatukujua kwamba tutapata mvua za *El-Nino* na kimbunga Hidaya, lakini kwa jitihada nzuri za Mheshimiwa Rais fedha hizi zimepatikana, zikiwemo shilingi bilioni 130 ambazo tulizitumia kipindi cha mvua za *El-Nino* ili kuweka mawasiliano ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika madaraja na makalavati ambayo tunaenda kujenga, fedha hizi pia zingeenda kujenga miradi mipya, lakini kwa sababu ya athari kubwa ambazo zilijitokeza, nadhani mnakubaliana nami kwamba, ni bora tukajenga miundombinu hii na baadaye kwa kadiri fedha zitakapokuwa zinapatikana ndiyo tuweze kwenda kwenye miradi mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kwenda kwenye miradi mipya, barabara zikiharibika wananchi wetu wanasubiri mawasiliano ya kudumu yarudi halafu tunakuwa hatuyarudishi. Kwa hiyo, tumeona ni vyema tukajikita kwenye kujenga madaraja na makalavati halafu kadiri fedha zitakapopatikana tukaendelea kutekeleza miradi mipya, ambayo ilikuwa kwenye bajeti, lakini fedha hii ikatumika kwenye kurudisha miundombinu ambayo iliharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafanikio pia tunamshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Tunajivunia kwamba, katika kipindi ambacho amekuwa madarakani tumekamilisha miradi ya barabara 25 yenye jumla ya kilometa 1198.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunayo miradi 87 yenye jumla ya kilometa 3,140.7 ambayo ipo hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika mjadala, Wabunge mmezungumzia changamoto za ukandarasi kusuasua katika utekelezaji, ninawahakikishia kwamba jitihada kubwa zinaendelea chini ya Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, kuhakikisha kadri fedha zinavyopatikana tunaendelea kulipa wakandarasi ili miradi hii 87 yenye jumla ya kilometa 3,140.7 iweze kuendelea. Kwa hiyo, ningependa kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge Serikali hii ni sikivu, tunatambua changamoto zilizoko huko *site* na tutafanya kadri ya uwezo wetu ili kuhakikisha wakandarasi hawa wanaendelea kulipwa ili kazi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mkakati wa kupunguza foleni kwenye majiji. Nikianzia na hapa Dodoma, Dodoma ni Makao Makuu ya nchi yetu panapokua kwa kasi kwa sababu Watanzania wanakuja kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kuwajulisha kwamba kazi nzuri ambayo Rais wetu alituanzishia ya kujenga barabara za mzunguko wa pete - *ring road* kilometa 112.3 kwa *network* ya kutoka Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa yenye kilometa 52.3 tuko 85% ya utekelezaji, kwa maana imebakia 15% na kufika

Januari, mwakani Mkandarasi atakuwa amekamilisha ujenzi wa hizi kilometa 52.3 kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kipande kingine cha barabara hii ya pete ambacho kinatoka Ihumwa – Matumbulu – Nala chenye urefu wa kilometa 52.3. Sasa hivi utekelezaji upo 80% na tunatarajia kufika mwezi Machi, mwakani hiki kipande pia kitakuwa kimekamilika. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutuwezesha, wakandarasi wanapata fedha kwa wakati na kazi zinaendelea vizuri, sambamba na ujenzi wa *airport* ya Kimataifa ya Msalato na yenyewe kazi inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika kujenga Makao Makuu yetu ya nchi hapa Dodoma, zimekuwepo na foleni hapa mjini, lakini katika Mpango huu ambao tumeujadili, tunapanga kujenga barabara ya njia nne mpaka sita kuanzia hapa Kimbinyiko, hapa nje ya Bunge kwenda hadi njia panda ya kwenda Ikulu – Chamwino kilometa 32. Sehemu nyingine zitakuwa ni njia nne, sehemu nyingine ni njia sita kulingana na usanifu ambao tumeufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapanga kujenga barabara ya njia nne kuanzia *round about* ya kuelekea Singida pale Machinga *Complex* kwenda mpaka eneo la Msalato ambapo barabara *ring* inakutana na hii barabara ya kutoka mjini kwenda Arusha. Vilevile kutoka Singida *round about* hapa mjini kuelekea Iringa *Road* tunapanga kujenga barabara ya njia nne mpaka kwenye barabara ya pete ambayo inatoka kule Ihumwa – Matumbulu kuelekea Nala. Mipango ni mizuri, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kwamba mipango hii iwe ni moja ya vipaumbele katika kusaidia kujenga Makao Makuu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Barabara ya *Inner ring road* ambayo tunategemea kuijenga kuanzia pale Machinga *Complex* - Iringa *Road* itapita maeneo ya kule juu ya jengo la Takwimu kuunganisha na kule upande wa Makulu ili kupunguza foleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie baadhi ya barabara ambazo kwa kipindi cha mwezi uliopita tumepata *advance payment* ya shilingi bilioni 53.9. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuwezesha. Pia namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuendelea kutupa ushirikiano mkubwa, kwa sababu barabara hizi ni barabara ambazo mmezisubiri muda mrefu, ni sehemu ya barabara ambazo zinahitaji shilingi bilioni 166 ili ziweze kupata *advance payment* kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea shilingi bilioni 53.9, tayari mkandarasi ameshapewa fedha kuanza ujenzi wa barabara ya Ubena - Zomozi – Ngerengere kwa Mheshimiwa Babu Tale na Mheshimiwa Innocent Kalogeris na barabara ya Ifakara – Bungu yenye kilometa 62.5 kwa Mheshimiwa Asenga pamoja na Mheshimiwa Kunambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Barabara ya Ndungu – Mkomazi kule Same – Kilimanjaro kwa Mheshimiwa Mama yangu, Mheshimiwa Anne Kilango; Barabara ya Kibanda – Mwasonga – Kimbiji kule Kigamboni tayari mkandarasi ameshapata *advance payment* ameanza ku-*mobilize,* na barabara ya Nachingwea – Ruangwa yenye urefu wa kilometa 57.6 mkandarasi ameshapata *advance* kwa ajili ya kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kyerwa – Omurushaka kilometa 50 kwa Mheshimiwa Innocent Bilakwate; pia barabara ya Singida – Sabasaba – Sepuka – Ndago kule Singida – Kizaga, barabara katika Mji wa Mbeya kwa Mheshimiwa Spika pale na penyewe kuna changamoto kubwa ya foleni, napo mkandarasi tumempa fedha ili aendelee na kazi ya barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma eneo la Uyole – Ifisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa Dar es Salaam, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wiki mbili zilizopita tumesaini na tumemkabidhi mkandarasi kuanza ujenzi wa Daraja la Jangwani. Daraja ambalo mvua zikinyesha Dar es Salaam sehemu ilikuwa inafunga lakini tunaenda kusahau, kwa sababu tunaenda kujenga daraja lenye urefu wa

mita 390 na barabara za maungio mita 700 sawa na shilingi bilioni 97.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tunao Mpango huu ambao tumejadili wa kujenga, kupanua barabara kutokea Mbagala Rangi Tatu kuelekea Vikindu. Mheshimiwa Ulega pamoja na Mheshimiwa Chaurembo na Wabunge hata wa Mikoa ya kule Lindi na Mtwara, pale eneo lina changamoto kubwa ya foleni. Hivi ninavyozungumza, kwenye shilingi bilioni 868.56 ipo *package* ya kwenda kujenga pale Daraja la Mzinga ili kuondoa *bottleneck* ya foleni ambayo iko eneo la Mbagala Rangi Tatu kuelekea Vikindu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya baadaye, mpango wetu ni kujenga barabara *lanes* za kutosha kama ilivyo barabara ya kutoka Kimara kuja Kibaha, basi kuanzia Mbagala Rangi Tatu mpaka eneo la Mwanambaya kule ili kuweza kufungua Jiji la Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Lindi pamoja na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Miradi ya *BRT* wakandarasi wako *site,* kazi inaenda vizuri na barabara ya kuelekea Bagamoyo eneo la Basihaya Mheshimiwa Askofu Gwajima najua amefuatilia sana, tumefanya *addendum* ya kumwongezea mkandarasi kusanifu lile eneo la Basihaya tusahau mambo ya mvua ikinyesha mawasiliano ya barabara kukatika. Itajengwa vizuri pale ili maji yaendelee na safari yake ya kwenda baharini huku wananchi wakiendelea na mawasiliano ya usafiri na usafirashaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza adha ya foleni kwa Mkoa wa Dar es Salaam, vilevile barabara ya Mwai Kibaki tunao mpango wa kuijenga njia nne kuanzia Morocco kwenda Mikocheni kule Kawe kuunganisha Lugalo, na kwenda nayo mpaka kule njia ya kuelekea *White sands* na kupandisha mpaka Afrikana, tunaamini mipango hii itasaidia sana kuifungua Dar es Salaam sambamba na kupanua barabara kuanzia Ubungo kwenda Kimara ili iungane na ile barabara ya njia nane kutoka Kimara kuelekea Kibaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mikakati yetu ya kupunguza foleni, ipo barabara ya Victoria – Mpiji - Magohe – Bunju kwa Mheshimiwa Askofu Gwajima, pamoja na Ndugu yangu Mbunge wa Jimbo la Kibamba tunaendelea na mipango hiyo pamoja na barabara ya Kimara Bonyokwa na yenyewe iko mikakati yetu ya kupunguza foleni ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa vivuko, najua Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoka maeneo ambayo wananchi wetu wanahitaji vivuko wamekuwa wakifuatilia kwa muda mrefu. Habari njema, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha wiki iliyopita tumepata shilingi bilioni 8.87 kwenda kukamilisha vivuko ambavyo viko kwenye ukarabati na vivuko ambavyo vinajengwa vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, ziara ambazo amekuwa akizifanya kwenye maeneo haya, alitoa maelekezo kwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ametufanyia wepesi tumepata fedha hii tunaenda kukamilisha vivuko vipya; Kisolya – Lugezi ambacho… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia…

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwilo – Bukondo – Mafia – Nyamisati – Nyakaliro – Kome – Buyagu – Mbalika na vilevile tunaenda kukamilisha ukarabati wa vivuko *MV. Nyerere – MV. Kome II – MV. Kilombero II – Mv. SabaSaba – MV. Old Ruvulu* na *MV. Ukala One*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aweso, jiandae Mheshimiwa Ulega, jiandae Mheshimiwa Mavunde, jiandae Mheshimiwa Mchengerwa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini nianze kwa kusema asiyeshukuru watu hata Mungu hawezi kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii moja kumpongeza sana sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Maji kwa Mpango mzuri pamoja na kaka yangu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Ninachotaka kukisema, nimesoma Mpango ambao nataka nilithibitishie Bunge na Watanzania kwamba Mpango umepangika kweli kweli, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii nayo kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri katika Mpango, pia katika suala zima la eneo letu la maji. Niseme kwamba maoni na ushauri tumepokea na tunajipanga kwa ajili ya utekelezaji zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote lazima liwe na mwelekeo unaojulikana na unaotabirika. Taifa lolote lazima liwe na dira kujua limetoka wapi liko wapi na linataka kufika wapi? Taifa lolote lazima lione kesho likiwa leo, ndiyo maana Tanzania chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina dira, ina mwelekeo na sasa inachora ramani kwa ajili ya Tanzania kubwa tunayoitaka na maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, tunapozungumzia suala la maji, huko nyuma na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, ilikuwa ikifika suala la maji katika hili Bunge lako Tukufu palikuwa hapatoshi. Bajeti ya Maji ilikuwa zikikataliwa siyo mara moja siyo mara mbili. Mwenyekiti ni shahidi, ipo miradi ambayo ilitolewa fedha nyingi sana hasa miradi ya vijiji 10, Mheshimiwa Katibu Mkuu Mstaafu kaka yangu Dkt. Kitila analifahamu miradi ambayo ilikuwa inafadhiliwa na *World Bank*. Ilifikia hadi wakati baadhi ya magari kwa maana ya wenzetu wa Wizara ya Maji, Wahandisi kila sehemu walikuwa wakipigiwa kero na kupewa lawama mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tarehe 22/4/2021 Dkt. Samia Suluhu Hassan alihutubia katika hili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alitoa maelekezo mahususi juu ya Wizara yetu ya Maji, alisema kwamba yeye ni mama na asilimia kubwa wanaoteseka juu ya adha ya maji ni akinamama. Hataki kusikia, hataki kuona wamama wa nchi hii wanateseka juu ya adha ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie ndugu zangu Wabunge, ukitaka kujua umefanikiwa ama haujafanikiwa, lazima ujifanyie tathmini wapi ulipotoka? Nataka niseme, kwa kipindi kifupi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kazi kubwa imefanyika chini ya uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania kwa mujibu wa TAMISEMI, tuna vijiji takribani 12,318. Kutokana na changamoto kubwa sana hasa eneo la vijijini mkaona haja juu ya uanzishwaji wa Wawakala wa Maji Vijijini kwa maana ya *RUWASA*, kwa kipindi hiki cha muda mfupi tumeshafika takribani vijiji 10,000 tumebakiza vijiji 2,000. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, niliwahi kwenda Simanjiro kwa Mheshimiwa Olesendeka Mzee wangu, tuliwahi kuona akimama wanatembea zaidi ya kilometa 40 kwa punda hawana maji. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani kwa muda wake mfupi, zaidi ya shilingi bilioni 42 zimewekezwa Simanjiro kwenye mradi wa Orkesument, Wanasimanjiro wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kakonko hali ilikuwa ni mbaya. Moja ya changamoto kubwa sana ni suala zima la maji, kwa muda mfupi ambao Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia ndani ya miaka mitatu, leo Kakonko hana sababu ya kuukosa Ubunge. Hii ni kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda maeneo mbalimbali ya Longido, maeneo ambayo wananchi kule ni wafugaji ambao

wanateseka, wanahangaika juu ya adha ya maji wao pamoja na mifugo yao, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza shilingi bilioni 16 Wanalongido leo wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ambacho nachotaka kukisema? Wizara ya Maji huko nyuma ilikuwa Wizara ya kero na lawama, haya mageuzi ambayo yamefanywa, yamefanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2022, umeitangaza Wizara ya Maji ndiyo Wizara namba moja kwa kufanya vizuri hasa kwenye Miradi ya Maji. Mwaka huu *World Bank* ilianzisha programu ya *P4R,* zimeitwa nchi 42 tu zilishindanishwa na wakaitwa Mawaziri wa Fedha akiwemo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Waziri wa Maji zaidi ya nchi 42. Nchi ya Tanzania imetangazwa na *World Bank,* ndiyo nchi kinara kwa miaka miwili mfululizo juu wa uwekezaji wa miradi ya maji nchini Tanzania hasa maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge tusione haya, tusione aibu kuzungumza ndani ya Bunge, nje ya Bunge kazi kubwa iliyofanywa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Bunge hili litaingia katika historia hasa katika suala zima la maji. Leo tumebakiza vijiji 2,000. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mama anajua changamoto wanazopata akinamama wenzie, kwa hivi vijiji 2,000 akaniambia mimi Waziri wa Maji, sihitaji asilimia, ninachotoka vijiji vyote vya Tanzania viweze kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alitupatia fedha za UVIKO. Tumefanya miradi katika kila Jimbo kuhusu miradi ya UVIKO, lakini akaona haja na maelekezo yake tununue mitambo ya uchimbaji wa visima. Nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo hii, katika kila Mkoa uwe na mtambo wake. Nini maana yake? Ni kwamba katika kila kijiji ambacho hakina maji twende tukachimbe maji. Namshukuru

sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, Waziri wa TAMISEMI kwa ushirikiano wake mkubwa, naamini kwa ushirikiano huu tunakwenda kumaliza matatizo ya maji katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, achana na hilo, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameenda mbali zaidi, siyo maeneo yote ukichimba kisima utapata maji. Yapo maeneo aina ya Chemba hayana maji chini ya ardhi lakini yanatambua nchi yetu si maskini juu ya unyeshaji wa mvua. Kuna haja juu ya uvunaji maji ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametununulia mitambo seti tano kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa katika kila Kanda ya Tanzania. Nataka niwaambie Rais aina ya Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila mahali, Rais aina ya Dkt. Samia Suluhu Hassan; hapatikani kila wakati. Tumempata ndugu zangu Watanzania, lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania katika kuhakikisha tunapata maendeleo makubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania yetu, maendeleo yetu; ili tuweze kwenda, ni sawa na gari ambayo imenasa kwenye matope, hatuwezi kumwachia Rais wetu Dkt. Samia Suluhu peke yake. Mawaziri lazima tusukume, Waheshimiwa Wabunge lazima tusukume na Watanzania lazima tusukume, tutafika mbali kwa sababu ametutengenezea mazingira makubwa katika Taifa letu tuweze kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamu yao Waheshimiwa Wabunge, wanatambua kabisa nchi yetu ya Tanzania tuna maziwa, tuna mito, kwa nini Watanzania wapate changamoto ya maji? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais wa kusema na Kutenda. Ameianza ndoto ya kuhakikisha tunatumia maji ya Ziwa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kuhakikisha watu wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *seeing is believing,* yaani kuona ni kuamini; amechukua maji ya Ziwa Victoria kutoka Mwanza ameyapeleka Tabora, ameyapeleka Igunga, ameyapeleka

Nzega na sasa hivi ametupa maelekezo maji yale tunayapeleka Sikonge, Kaliua, Urambo kwa Mheshimiwa Mama Sitta. Mnataka Mheshimiwa Rais afanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maji tunayotoa Ziwa Victoria katika Jiji la Mwanza, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia maelekezo Wizara ya Maji, unapokuwa karibu na uwaridi lazima unukie. Haiwezekani wananchi wa Jiji la Mwanza wateseke juu ya adha ya maji ilhali ziwa lipo pale. Ametupatia fedha zaidi ya shilingi bilioni 70, tumejenga chanzo kikubwa cha Butimba, mradi umekamilika. Kazi iliyobaki ni kwa ajili ya usambazaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, baada ya dhiki siyo dhiki; baada ya dhiki ni faraja na faraja ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumempata Mkandarasi ambaye tumeshaanza kusainiana naye na tunakwenda kufungua mradi ule kwa ajili ya kufanya utandazaji na Mkandarasi ni *SINOHYDRO*. Maeneo ambayo hayana maji tunakwenda kuyatandazia ili watu waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, achana na hilo, tumepewa maelekezo kwa maeneo ya Katavi, Kigoma pamoja na Rukwa tuna Ziwa Tanganyika. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais Ziwa Tanganyika lazima litumike kwa ajili ya kutatua matatizo kwa wananchi. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, tafadhali kaa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametupatia maelekezo juu ya kutumia maji ya Ziwa Tanganyika, yaende yakasaidie Katavi, Kigoma na Rukwa. Kama nilivyosema, *seeing is believing.* Mheshimiwa Kilumbe yupo, leo ukienda Kigoma tumeshayatumia maji ya Ziwa Tanganyika. Wana-Kigoma Ujiji wamepata mradi mkubwa zaidi ya shilingi bilioni 40 tumeweza

kutekeleza na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthubutu wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan unapaswa kuungwa mkono. Yalikuwa maandiko na maazimio ya Bunge kila mwaka juu ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda Tangu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kila mwaka Bunge linaazimia juu ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa muda mfupi ametoa maelekezo na uthubutu wake wakasema bwawa tutajenga kwa fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa ametoa *advance payment* na ninavyozungumza Mkandarasi yupo *site*. Mradi utaweza kuhifadhi maji zaidi ya lita bilioni 190. Wana-Dar es Salaam na Pwani suala la changamoto ya maji linakwenda kuwa *bye-bye* kabisa juu ya kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Fedha. Pamoja na mafanikio haya, wanasema ukimwona kobe juu ya mti, amepandishwa, hapandi mwenyewe. Wizara ya Fedha imefanya kazi kubwa na nzuri ya ku-*support* Wizara ya Maji kutokana na maelekezo na ushauri mkubwa wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kwamba tunatatua matatizo ya maji katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Wizara ya Maji kwa maelekezo na mienendo, lazima tukubali kubadilika. Tutumie teknolojia kwa mageuzi ndani ya Sekta yetu ya Maji. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika hasa juu ya suala zima la bili za maji. Ni haki ya mwananchi kutumia maji, lakini mwananchi naye asisahau ana wajibu wa kulipia maji. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, maelekezo yake aliyoyatoa kwamba ni marufuku kwa Mwananchi wa Tanznaia kumbambikizia bili za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi uelekeo wa Wizara ya Maji tunakwenda kutumia *prepaid meter* kama *TANESCO,* kwamba

tunakwenda kumfungia mwananchi LUKU ya maji. Mwananchi anataka maji ya shilingi 10,000 analipia shilingi 10,000, wala hakutakuwa na nongwa. Hayo ndiyo maelekezo, mageuzi na matokeo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunajua mazingira ya sasa tunakuwa na mabadiliko ya tabianchi. Ukiangalia Sera ya Wizara ya Maji ni tangu mwaka 2002. Kuna haja juu ya uanzishaji wa sera mpya. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupatia maelekezo, sasa tunakwenda kuanzisha sera mpya ya maji ambayo itaendana na mazingira ya sasa na ya kuweza kuwashirikisha vizuri wadau mbalimbali wa maendeleo na ambayo tutakwenda kufanya mageuzi makubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ulega, jiandae Mheshimiwa Mavunde. Mheshimiwa Mavunde, baada ya Mheshimiwa Ulega unafuatia wewe, unayo nguvu ya kuchangia katika kipindi hiki kwa mazingira ya huko wapi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Ulega.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nitumie fursa hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika ajenda hii iliyopo Mezani. Pia naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo, dira, uongozi wake imara na kwa namna ambavyo amedhamiria kabisa katika kujenga upya sekta hizi za uzalishaji ikiwa ni pamoja na Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyowekwa Mezani na wabobezi wawili hawa; Mheshimiwa Profesa Kitila

Mkumbo, Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na timu nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepata maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kadhaa. Wengi wameonesha namna ambavyo wangetamani mambo katika Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi yaende. Sisi tumechukua maoni haya, tunakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuonesha namna ambavyo tunakwenda kuyafanyia kazi pale mbele nitaonesha na nitaeleza namna Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ilivyojipanga kimkakati kwenye kuhakikisha kwamba Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi inafanya vyema katika kuinua hali za Watanzania na katika kuweka mchango mpana zaidi kwenye pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa ilitokea hoja, na kabla sijaendelea ningetamani sana kwa ufupi nijaribu kuiweka hoja ile vizuri. Katika wachangiaji wazalendo wanaotamani kuona kwamba, tunatumia vyema rasilimali za nchi yetu kwenye kujenga Taifa letu na kuinua hali za Watanzania, walipata nafasi ya kueleza kwamba, kwa nini tunayo maziwa, bahari kubwa na mito lakini bado tunaagiza samaki wengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Watanzania na Bunge lako kwamba, tunathamini mchango ule na kwa hakika tunajua ya kwamba, usemaji ule umetokana na ukweli wa kwamba wanatamani kwa nia zao za kizalendo waone maziwa, mito na bahari yetu tukizalisha zaidi. Tunakubaliana na ukweli huo, lakini nitoe takwimu sahihi ya kwamba, mpaka mwaka 2018, nchi hii ilikuwa ikiagiza samaki zaidi ya tani 22,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mabadiliko makubwa sana ya kimkakati. Lengo la mabadiliko yale ni kutaka kuonesha kwamba tunatoa fursa ya shughuli za ufugaji wa samaki katika nchi ili zishamiri na hizi nitazieleza huko mbele. Ndiyo maana tukatoa vizimba vingi na tunaendelea kutoa vizimba hivyo. Matokeo ya vile vizimba yako wazi. Ukienda pale Mwanza

yanaonekana wazi. Watu wa Ilemela, vijana wamefanya kazi nzuri sana na tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, imekuwa ni sehemu ya mfano. Huko mbele kidogo nitaeleza jambo hili. Ukweli ni kwamba hivi sasa katika nchi siyo zaidi ya tani 9.5 tu za samaki zinazoingia. Tena tani hizi 9.5 za samaki zinazoingia ni samaki aina maalum, wengi katika hao sisi hatuzalishi katika Taifa letu. Kwa mfano, samaki aina ya *salmon* ambao hawapatikani hapa, wanatoka katika nchi nyingine duniani. Wapo wageni wanaokuja katika Taifa letu ambao wanahitaji aina hiyo ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka tani 22,000 mpaka tani 9.5 tu, kihisabati inaelekea kama ifuatavyo: kilo moja ya samaki *imported* ana gharama ya mpaka dola 4.7. Sisi peke yetu *fisheries* tunachukua dola 2.5, bado kuna gharama za bandari, usafirishaji na kadha wa kadha inafika dola 4.7. dola 4.7 ukiibadilisha inakwenda takribani shilingi za Kitanzania 12,700 kwa kilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiichukua kilo moja shilingi 12,700 unaweza ukaona kwamba, samaki huyo ukimweka sokoni hauziki. Ndiyo maana nikasema ya kwamba, tulilifanya jambo hili kimkakati kwa lengo na dhamira ya kutoa nafasi ya ufugaji wa samaki nchini uweze kushamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tumepata rai kwa sababu mahitaji ya samaki nchini bado ni makubwa sana. Uzalishaji wetu ni takribani tani 500,000, mahitaji ni tani zaidi ya 1,000,000. Kwa hiyo, samaki wamekuwa gharama kubwa sana na watu walio wengi hawamudu kununua kitoweo cha samaki. Wataalamu wangu wamenishauri na bado tunafanya mazungumzo na wenzetu wengine hasa wadau ya kwamba nini tufanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sisi samaki tunaofuga na tunaoshamirisha kufuga hivi sasa ni samaki aina ya Sato na Kambale, lakini vipi kama vibua vikitazamwa uwezekano wa kuja kupunguza hili *gap*? Tumekubaliana ya kwamba tuendelee kufanya mashauriano na wadau mbalimbali ili kusudi tuone

uwezekano wa kuweza kuwasaidia Watanzania kwenye kupata samaki kwa bei nafuu, bila ya kuathiri shughuli zetu tunazozisimamia za ufugaji wa samaki aina ya Sato na Kambale ambao hawa tumewapa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya vizuri sana katika *export* ya samaki na tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukweli kwenye *export* ya samaki na nyama, Taifa letu linafanya vizuri sana. Hivi sasa ni fursa kubwa Waheshimiwa Wabunge na tumekuwa tukipokea wageni wengi sana wanaotaka kuwekeza kwenye eneo hili. Ukweli ni kwamba kila mmoja anajionea nyama hii leo ni fursa kubwa huko ulimwenguni ya kutoka hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia tulikuwa na tani 1,700. Leo tuna tani 14,000 nyama ya Tanzania inauzwa ulimwenguni kote. Ni mafanikio makubwa. Tunamkaribisha kila mmoja mwenye nia njema ya kutaka kuwekeza katika eneo hili, milango ipo wazi. Watu wanapenda mbuzi na nyama ya kutoka Tanzania. Karibuni tuwekeze ili kusudi tuweze kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa kuhakikisha kwamba tunachukua hii fursa na tunaitumia vyema, tulielekezwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwawezesha vijana wa Kitanzania. Miradi ya *BBT* mifugo na uvuvi imefanya vizuri sana. Wale vijana waliokuwa wanafanya unenepeshaji wa mifugo ni kwamba mpaka hivi sasa wamefanikiwa kuuza ng'ombe wote na wamepata faida zaidi ya shilingi 130,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo vijana 158 ambao tumewakopesha sasa shilingi 1,100,000,000 kupitia Benki yetu ya Kilimo. Tunakwenda kuwapa vitalu katika eneo la Kitengule kule Kagera na Kagoma. Kila mmoja ekari 10, anakwenda kufanya kazi ya unenepeshaji. Kila kikundi cha vijana kinakuwa na vijana watano na jumla ya vikundi 25. Bado tumeichukua sera hii tumeipelekea mikoani pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia tunakwenda katika Mkoa wa Tabora, Pwani, Arusha, Morogoro na Mtwara kwa sababu kule Mtwara ipo fursa ya wenzetu wa Comoro wanahitaji sana nyama ya kutoka Tanzania na kutoka Mtwara kwenda Comoro ni karibu zaidi. Kwa hiyo, tunaichukua fursa hii na kuipeleka jumla ya fedha shilingi bilioni 4.2 tumeziweka huko ili kusudi vijana waweze kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sera ya Uchumi wa Bluu. Wabunge wengi wameichangia sera ya Uchumi wa Bluu, kwa kweli tunafanya vizuri. Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko imeshafika 70% hivi sasa na tunakwenda tena kutengeneza Bandari nyingine pale Bagamoyo. Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko itakuwa na eneo la uchakataji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yetu hapa ni kuweza kuchukua fursa ile ya Bahari Kuu. Meli zinazovua kule Bahari Kuu ziweze kuja katika bandari yetu, zishushe samaki, tupate faida ya kutoa huduma mbalimbali na eneo lile litakuwa pia na Kiwanda cha Uchakataji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda vyema katika eneo hili la Uchumi wa Buluu. Kwa kumalizia tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameridhia chanjo kwa wote. Imechangiwa sana mambo ya chanjo hapa shilingi bilioni 28. Kwa muda mrefu chanjo iliachwa, ilikuwa inatekelezwa na Sekta Binafsi, Serikali haikuwa imeweka mkono wake. Hivi sasa tunakwenda kuchanja na kila mfugo utachanjwa katika Taifa letu. Fedha ya Serikali shilingi bilioni 28 imewekwa kuhakikisha kwamba, tunaondoa makanjanja. Wafugaji wa Taifa hili wamepigwa sana dawa ambazo siyo za kweli na hazina uhakika. Sasa, tunakwenda kurekebisha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia shilingi bilioni 450 ya *modernization* tunakwenda kujenga upya sekta yetu ya maziwa. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameridhia shilingi bilioni 450 zitakazokwenda katika maeneo ya uzalishaji mkubwa wa maziwa nchini ambao tutakwenda kubadilisha sana eneo hili la maziwa ili Watanzania waweze kutumia fursa ya uchumi wa

maziwa tujitosheleze wenyewe na ikiwezekana na sisi tuweze kusafirisha nje ya mipaka ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, siyo tu maziwa katika matoleo yetu na ninaamini kabisa kwa namna ambavyo dira hii imetengenezwa, tunakwenda pia kuchechemua na kuzalisha upya *breed* mpya na kuendeleza eneo la chanjo na miundombinu ya mifugo katika bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wa *World Bank* ambao utakuwa na zaidi ya shilingi bilioni 500. Hizi zitakwenda katika maeneo ambayo yanakwenda kufanya shughuli ya ng'ombe na mbuzi wa nyama tu. Lengo na dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa ni Taifa Kiongozi kwenye eneo la mifugo, uvuvi na samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mavunde, jiandae Mheshimiwa Mchengerwa.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nawashukuru sana Mawaziri wote wawili waliowasilisha taarifa yao, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango. Kipekee kabisa nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameendeleza kuikuza Sekta ya Madini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ya kiti ninaongeza muda mpaka tumalize shughuli zetu ambayo haitazidi saa 2.30 kutokana na umuhimu wa ajenda yetu na *Road Map* ya Taifa letu. Kwa hiyo, tuvumilie. Tunapata mambo muhimu ya kurudi nayo majimboni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nianze kwa kuelezea jinsi ambavyo Mpango huu umeakisi maendeleo ya Sekta ya Madini. Katika historia ya Wizara ya Madini miaka yake yote, Wizara hii haijawahi kupokea fedha

nyingi za bajeti kama ambavyo imepokea kipindi cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Madini imeongezeka kutoka shilingi bilioni 89 mpaka kwenda shilingi bilioni 231 na kiasi kikubwa cha fedha kimeelekezwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina. Pamoja na utafiti wa kina, pia kiasi kikubwa cha fedha kimeelekezwa *GST* ambayo imekuwa ni ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu *GST* ndiyo moyo wa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utafiti wa kina, pia kiasi kikubwa cha fedha kimeelekezwa *GST* ambayo imekuwa ni ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu *GST* ndiyo moyo wa Wizara ya Madini. Kwa hiyo, tunategemea kupitia *GST* baada ya kufanya utafiti wa kina tutawaongoza vizuri Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyoongezeka, zaidi ya shilingi bilioni 115 imeelekezwa kwenda *GST* ambayo itafanya kazi zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya kwanza itakwenda kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya kisasa, ambayo itajengwa hapa Dodoma, Geita, na Chunya ili kuwaongoza vizuri wachimbaji ambao wamekuwa na changamoto kubwa ya kupeleka sampuli zao, wengine kwenda mpaka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika historia ya Taifa hili, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kujenga maabara kubwa na ya kisasa hapa Dodoma ambayo itawahudumia wachimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika kulitekeleza hilo, Wizara ya Madini imejiwekea mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapima nchi yetu kwa kufanya utafiti wa kina na kuwaongoza vizuri wachimbaji. Mpaka sasa hivi tumekwisha kufanya utafiti wa kina kwa 16% ya nchi yetu ya Tanzania. Chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan,

tumewezeshwa fedha ambazo tutakwenda kununua helkopta kwa ajili ya kusaidia upimaji wa madini kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunao mradi ambao utakwenda kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa kina. Tunao mradi ambao tutautekeleza katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, ambao utakwenda kuligusa eneo la kilometa za mraba 165,934 za nchi yetu ya Tanzania, sawa sawa na 18% ya nchi nzima. Tutapima kupitia utaratibu huo. Tunaamini kabisa tukiyafanya haya, tutakuwa tumewaongoza vizuri wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Sekta ya Madini katika pato la Taifa umeendelea kuongezeka. Mwaka 2022 Sekta hii ya Madini ilichangia kwa 7.2% kwenye pato la Taifa. Leo tunavyozungumza, Sekta hii ya Madini inachangia kwa 9.0% na tumewekewa malengo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, kwamba ifikapo mwaka 2025 tuwe tunatoa mchango kwenye pato la Taifa kwa zaidi ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema ni kwamba, tumeanza hatua moja baada ya nyingine kufikia malengo hayo. Hatua ya kwanza ni kwenye hatua ya ukusanyaji wa maduhuli. Baada ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini, na tukaanzisha masoko na vituo vya ununuzi, sasa hivi nchi yetu tumeanza kuona manufaa ya Sekta ya Madini kutoa mchango wake kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015/2016, Sekta ya Madini iliingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 161 kwa mwaka mzima. Baada ya kufanya marekebisho ya sheria chini ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tukaweka na vituo vya ununuzi na masoko ya kuuzia madini, katika siku 121 tu za mwaka huu wa fedha, Sekta ya Madini imeingiza katika Mfuko Mkuu shilingi bilioni 354. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunakusanya shilingi trilioni moja kuingiza katika Mfuko Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, katika masoko yetu ya madini na vituo vya ununuzi 102, jumla ya fedha ambayo

imekuwa *transacted* ni zaidi ya shilingi 1,700,000,000,000 kwa mwaka. Hii ni kuonyesha kwamba sekta hii inaendelea kukua siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeshuhudia mchango mkubwa wa Sekta ya Madini katika upatikanaji wa fedha za kigeni. Katika mwaka wa fedha uliopita 2023/2024, Sekta ya Madini imechangia katika upatikanaji wa fedha za kigeni kwa zaidi ya 56%, na tumefanya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ya zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 3.1, ambayo imesaidia sana katika kuchochea uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo katika Mpango huu, pia tunazungumza mchango wao mkubwa katika kuimarisha Sekta ya Madini. Sasa hivi kazi ambazo tunazifanya ni kuhakikisha kwamba, kwanza tunawatengea maeneo wachimbaji wadogo, na hii inatokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu leseni, Mheshimiwa Rais alielekeza leseni zote ambazo hazifanyiwi kazi na maeneo yote ambayo yamehodhiwa na watu, tuweze kuyafuta na kuyatenga kwa ajili ya machimbaji wadogo. Tumefuta leseni zaidi ya 2,648, ambapo sasa hivi tumeyatenga maeneo hayo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia kupitia *STAMICO* tumenunua mitambo ya kuchoronga ambayo ni *Drilling Rigs*, ambazo zitafika tarehe 15 mwezi huu wa 11, 2024, na lengo lake ni kuwasaidia wachimbaji wadogo kuondokana na gharama kubwa ambayo wanaitumia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchimbaji mdogo sasa hivi akienda kuchoronga kwenye shimo la mita 100, akienda kumtafuta mtu mwenye mashine anayefanya kibiashara, atatumia zaidi ya shilingi milioni 25 kwa shimo la mita 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Mheshimiwa Rais kupitia *STAMICO*, sasa hivi mchimbaji mdogo ana uwezo wa kuchoronga

mita 100 kwa shilingi 10,700,000 na fedha inayobaki ni ruzuku ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili tuweze kuwasaidia na wenyewe pia waweze kufikia malengo. Sambamba na hilo pia hiyo inaendana na huduma za ughani ambazo tunazitoa kwa wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la Madini Mkakati. Wote tunafahamu kwamba sasa hivi dunia inauhitaji mkubwa wa Madini Mkakati. Mahitaji ya Madini Mkakati ifikapo mwaka 2050, inatazamiwa kuwa ni zaidi ya mara 150 ya mahitaji ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumebarikiwa kuwa na Madini Mkakati, na katika eneo hili, katika Madini ya Kinywe *(Graphite)* ambayo hivi sasa yana uhitaji mkubwa sana duniani, kwa zaidi ya tani 6,500,000 kwa mwaka. Nchi inayoongoza kwa uzalishaji ni nchi ya China. China wanazalisha 64% ya mahitaji yote ya *Graphite* duniani, lakini kwa Afrika, anayeongoza kwa uzalishaji wa Madini Kinywe ni nchi ya *Madagascar*, anazalisha 13% ya mahitaji yote ya Madini Kinywe duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa pili ni Msumbiji, anazalisha 10% ya mahitaji yote ya Madini Kinywe duniani, na wa tatu ni Tanzania, ambaye anazalisha 0.64%. Hii 0.64% hapa, huyu ni mzalishaji mzawa ambaye yupo kwa Msisi pale Handeni Tanga, anaitwa God Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi zaidi 10 ya Madini Kinywe ambayo haijaanza kufanya kazi. Ikianza kufanya kazi Tanzania itakuwa ni kinara wa uzalishaji wa Madini Kinywe hapa Afrika, ikiwapiku Msumbiji pamoja na *Madagascar*, kwa *reserve* ambazo tunazo ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la manunuzi ya dhahabu yanayofanywa na Benki Kuu ya Tanzania, imekuwa ni hoja ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Rais alitupa maelekezo ya kwamba, haiwezekani nchi yetu ya Tanzania imejaaliwa madini ya kutosha lakini hatuna akiba ya kutosha ya madini ya dhahabu, na hivyo kusababisha kuwepo na mtikisiko

mkubwa wa kiuchumi, na hasa kukosekana kwa Dola za Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya marekebisho ya sheria; kifungu cha 59(a) cha Sheria ya Madini kilirekebishwa na kutaka kila anayesafirisha madini nje ya nchi kutenga 20% ya madini yote kwa ajili ya kumuuzia *BoT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali palikuwepo na sintofahamu, tumeiweka sawa. Habari njema, kwa hivi sasa Afrika, anayeongoza kuwa na akiba ya dhahabu ni nchi ya Algeria ambaye ana akiba ya tani 173 ya dhahabu, lakini wa mwisho wa 10 ni Msumbiji, ambaye ana tani 3.6 za dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuanza kununua dhahabu katika nchi yetu ya Tanzania, kuanzia Oktoba tarehe mosi mpaka leo, nchi yetu imeshanunua, kwa maana ya *BoT*, dhahabu tani moja ndani ya mwezi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa sana na tunategemea kwamba ndani ya muda mchache ujao tutaingia katika 10 bora kuwa na hifadhi ya dhahabu kupitia *BoT*. Haya yatakwenda kusaidia kuimarisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ninataka nilisemee, ni kupitia *STAMICO*. Sasa hivi tunajipanga katika makaa ya mawe pale Kiwira, tuweze kuja na mradi wa uzalishaji wa umeme na tumepata kampuni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, malizia.

**WAZIRI WA MADINI:** ...ambayo itazalisha zaidi ya *megawatts* 2,000, ambayo itasaidia sana katika kuingiza kwenye gridi yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu wahudumu msaidieni maji, siyo sauti yake huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mchengerwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na *quotations* mbili; ya kwanza iliwahi kutolewa na Nelson Mandela, na *quotation* ya pili iliwahi kutolewa na Mahatma Ghandhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nelson Mandela aliwahi kusema, "Uongozi mzuri unahusisha kuwajibika kwa heshima na uaminifu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahatma Gandhi aliwahi kusema; "Uadilifu ni kufanya yaliyo sahihi, hata kama uko peke yako." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nianze na *quotations* hizi mbili. Taifa letu ni Taifa changa linaloendelea kupiga hatua. Tunatambua zipo changamoto ambazo zinaweza kuibuka katika maeneo yetu, lakini msingi wa Taifa letu, Baba wa Taifa ametuhusia, ni umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa sisi viongozi wenyewe, kwa viongozi wa kuchaguliwa na viongozi wa kuteuliwa tukavutana wenyewe kwa wenyewe, lazima tutambue kwamba matamanio ya Taifa letu hayawezi kufikiwa kwa mivutano baina yetu sisi viongozi wenyewe, hatuwezi kufikia matamanio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyakati hizi ninawaomba sana viongozi tuheshimiane, kila mmoja kwenye nafasi yake. Kwa sisi viongozi wa kuchaguliwa na viongozi wa kuteuliwa, ni vyema sana tukavumiliana na kuheshimiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi huu siyo wa kwangu, ni msingi ambao tumeachiwa na Baba wa Taifa. Ili tuweze kupiga hatua kama Taifa ni lazima tuvumiliane, ni lazima tuheshimiane kama Taifa. Nilisema nilianze hili kwa sababu Mheshimiwa

Sendeka amezungumza hapa kuhusu changamoto zilizoibuka Simanjiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua alinipigia, nami nilimpigia Mkuu wa Mkoa kujua kitu gani kinaendelea katika Mkoa huo wa Manyara, lakini niliarifiwa kwamba Mkuu wa Mkoa amepokea taarifa kutoka kwa Katibu wa CCM Mkoa pamoja na Mwenyekiti wa Chama kwamba kuna vurugu zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ilithibitishwa kwa picha za video pamoja na picha zilizopigwa katika eneo la tukio ambazo zilionyesha watu wamepasua, wamevunja ofisi pamoja na kupasuana na sime. Hali hii ndiyo ilisababisha Mkuu wa Mkoa kuamua kuchukua hatua hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuwasisitiza viongozi tuheshimiane. Ni vyema tukaheshimiana, kwa sababu msingi wa Taifa hili kesho tutaulizwa. Kama tutakuwa tunavutana na maendeleo yatachelewa. Huo ndiyo ukweli. Wewe utaamua kuvuta huku na mwingine atavuta huku, maendeleo yatachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana viongozi, hasa kipindi hiki kuelekea kwenye chaguzi mbalimbali, tuheshimiane. Nataka niwathibitishie, viongozi hawa wa mikoa na wilaya wanafanya kazi kubwa sana. Wakurugenzi wa Halmashauri wanafanya kazi kubwa sana kwa Taifa hili. Ni vyema tukiheshimiana, tutaweka mipaka ya utendaji ili kila mmoja wetu ajue wajibu wake katika kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi hii ni ya Baba wa Taifa. Ninawaomba kila mmoja wetu kujikumbusha kusoma misingi hii. Nyakati za *TANU*, wakati kinaanzishwa chama kimoja, nyakati za utawala wa chama kimoja, na hata wakati wa kuanzishwa Mfumo wa Vyama Vingi miaka ya 1990, mambo haya yalisisitizwa sana na Baba wa Taifa. Kwa hiyo, nawaomba sana viongozi tuheshimiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyakati zote za utendaji wa kazi, pale tunapowahudumia Watanzania, kama sisi wawakilishi wa wananchi, lakini pia wale waliokasimiwa mamlaka na Mheshimiwa Rais, ni vyema sote kwa pamoja tukajikita katika misingi ambayo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia amesisitiza katika nyakati zote za uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia. Nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Sisi tunatambua kwamba TAMISEMI ni Wizara nyeti na Wizara muhimu ambayo inaweza kusogeza mbele maendeleo ya Taifa letu. Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa 2025/2026, unalenga kujenga uchumi shindani, uchumi jumuishi na wenye viwanda kwa maendeleo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa miaka mitano. Mpango huu una dhamira ya kuimarisha ustawi wa wananchi kupitia ukuaji wa kiuchumi unaogusa maisha ya kila mmoja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ustawi wa wananchi umezungumzwa sana katika vitabu mbalimbali. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imezungumza kuhusu ustawi wa wananchi. Unaposoma kuanzia Ibara ya nane na kuendelea, inazungumza kuhusu ustawi wa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hulka ya kiongozi yeyote, kiongozi wa watu, hujikita katika mambo makuu yanayohusu ustawi wa wananchi wake. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema, "*The purpose of development is people*." Maendeleo ya kweli ni lazima yajikite katika misingi ya kuwaangalia Watanzania au kuwaangalia wananchi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni dhahiri kabisa, kazi anayofanya Rais wetu imejikita moja kwa moja katika kutafsiri ustawi wa Watanzania katika maeneo yao yote. Sisi tunaona namna gani Watanzania wanakuwa na furaha na Serikali yao.

Hakuwezi kufanyika maendeleo kama Watanzania au wananchi husika hawana furaha katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanafalsafa na Mwanamapinduzi Che Guevara aliwahi kusema; *"The true revolutionary is guided by great feeling of love*." Hili tunaliona kwa Rais Dkt. Samia. Mapenzi yake kwa Watanzania katika ujenzi wa shule mbalimbali, ujenzi wa vituo vya afya, na uboreshaji wa miundombinu. Eneo hili Rais Dkt. Samia amelitendea haki kwa Watanzania, na sisi ndiyo sababu tunasema kazi anayoifanya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia, ni mambo ya msingi ambayo Baba wa Taifa aliyaasisi kwa Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo Baba wa Taifa aliyapigia kelele, mimi na ninyi ni mashahidi. Wakati wa Mapinduzi mbalimbali yaliyotokea duniani, msingi wa Mataifa katika maeneo hayo ni wananchi. Wakati wa kupigania uhuru wa Taifa hili, msingi wa Taifa letu, wakati Baba wa Taifa na waasisi wa Taifa hili wanapigania uhuru wa Taifa letu, ilikuwa ni msingi kuhusu ustawi wa Taifa letu hili Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mapinduzi ya Serikali za Mitaa chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, tuliweka misingi ya uwajibikaji na utumishi ulioweka kipaumbele mahitaji ya wananchi. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema, "Uhuru wa kweli ni kuwa na uwezo wa kuwahudumia watu wetu kwa njia bora kabisa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Dhahiri, kama kuna mwakilishi yeyote wa wananchi, yeye anafikiria kuhusu maisha yake kuliko maisha ya Watanzania, basi huyo amekosea. Lazima nichukue fursa hii kuwapongeza. Sijawahi kuona Wabunge wanachangia vyema kama kipindi hiki cha kushauri Serikali kuhusu eneo hili la Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Wabunge ndiyo umesababisha mafanikio makuu ya Serikali ya Awamu ya Sita. Lazima tukiri, katika nyakati ambazo hazijapata kutokea kabisa, Serikali imefanya kazi kubwa ya kuimarisha mifumo ya utolewaji huduma kwa wananchi wa Tanzania. Leo hii hakuna Mbunge

hata mmoja hapa anayeweza kusimama akasema kwamba kipo kijiji, kijijini kwake kule katika eneo la wananchi wake, ambako Serikali haijapeleka hata senti tano, hayupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi huu ni msingi ambao Rais wetu amedhamiria kwenda kuufikisha katika maisha ya Watanzania wa kawaida kabisa, na msingi huu nimetangulia kusema kwamba uliasisiwa na Baba wa Taifa, ukaendelezwa na marais wote waliotangulia baada ya Baba wa Taifa; Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Awamu ya Tano na sasa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia anafanya mambo ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza alitamani kuyafanya katika nyakati zake. Nimeona hapa nizungumzie mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la elimu, Baba wa Taifa alizungumza sana katika hotuba zake kuhusu elimu. Kwenye eneo hili Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita amejikita katika kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata elimu. Mitazamo ya Rais Dkt. Samia ninaifananisha na mitazamo iliyowahi kutolewa na Mheshimiwa Rais wa kwanza mweusi kule Afrika ya Kusini ambaye aliwahi kusema, *"it is not beyond our power to create a world in which all children have access to a good education."* Msingi huu anaufanya Rais Dkt. Samia, na tunaona kwamba katika kila jimbo la nchi hii Rais Dkt. Samia amefika na ameweka fedha katika maeneo ya miradi ya elimu msingi na elimu sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia ameweka mpango imara wa kuimarisha na ujenzi wa shule katika maeneo mbalimbali nchini. Rais Dkt. Samia amejenga shule 380 za msingi katika maeneo mbalimbali nchini, amejenga shule za sekondari 830, lakini pia kati ya shule hizo kuna shule 26 maalum zenye vipaji kwa ajili ya watoto wa kike ili kuweza kuwajenga na kuwanyanyua. Rais Samia amejenga madarasa 4,411, amejenga madarasa ya awali 556.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, kila Mtanzania ni shahidi. Katika Taifa letu tangu tupate uhuru vituo vyetu vya afya na hospitali zetu za wilaya hazikuwahi kuwa na majengo ya dharura, wala hazikuwahi kuwa na majengo ya wagonjwa mahututi. Aliyelifanikisha hili siyo mwingine ni Rais Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii zipo halmashauri ambako kuna mitambo ya kuzalisha hewa tiba. Hewa tiba hizi tuliziona tu kwenye hospitali za rufaa na hospitali za mikoa, lakini hili limefanywa na kutekelezwa na Rais Dkt. Samia. Katika kipindi kifupi Serikali ya Rais Samia imejenga hospitali za wilaya na halmashauri zaidi ya 129, imekarabati hospitali kongwe 50, imejenga vituo vya afya 367; na kwa maelekezo yake Rais Dkt. Samia kila Mbunge inatakiwa atengewe fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo kimoja kipya cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani, leo wakati nazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amenithibitishia kwamba leo wanaendelea na vikao, lakini atatoa taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu ni lini fedha hizi zitaingia TAMISEMI ili tuweze kuzipeleka katika halmashauri zote nchini ili kila Mheshimiwa Mbunge aweze kupatiwa kituo kipya cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya miundombinu kazi kubwa imefanyika. Msingi wa uboreshwaji wa miji na majiji ni fikra za Rais wetu, Dkt. Samia. Naomba nikuthibitishie, kwamba Mheshimiwa Rais ametukabidhi zaidi ya shilingi tilioni 2.9 ambazo zinakwenda kuboresha miji na majiji, ujenzi wa masoko, ujenzi wa barabara mbalimbali na ujenzi wa stendi. Kwa Dr es Salaam ameelekeza zijengwe barabara kilometa 250 ili kila kona ya Dar es Salaam iwe na barabara kiwango cha lami. Eneo hili litagusa maeneo kote nchini katika mikoa yote 26, kwenye majiji na kwenye miji. Miradi hii ambayo ameibuni mwenyewe Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, itawahudumia Watanzania katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, lakini naomba niunge mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Haya ndiyo mambo ya Rais, Dkt. Samia. Kwetu akishinda uchaguzi, anashinda kwa haki kwa sababu ana dhamira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mkumbo, bado una *shock*? Tupo kazini jamani hapa mambo ya nje, ya Tabora Tabora tuache hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, naomba nikushukuru wewe pamoja na wasaidizi wako, kwa maana ya Wenyeviti wetu wa Bunge kwa jinsi ambavyo mmeendesha mjadala huu vizuri sana. Nawashukuru tena Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa jinsi walivyotoa maoni yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia maoni yao kwenye kurasa zote 79, kwa kweli maoni yao ni mazuri na tumeyachukua. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mpaka tunamalizia na Mheshimiwa Ole-Sendeka. Tulianza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, na tumepata wachangiaji 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa jinsi ambavyo wamejibu hoja na kutoa maoni yao na kueleza jinsi ambavyo Serikali inafanya kazi, wamefanya kazi yangu iwe rahisi sana katika kuhitimisha mjadala huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, ofisi yangu hii ambayo ninaisimamia haiwezi kufanikiwa bila uhodari na ushupavu wa Waheshimiwa Mawaziri, kwa namna ambavyo wameonesha hapa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa ushirikiano ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, Wizara ya Fedha na ofisi yangu kwa kweli ni mapacha. Tangu nichaguliwe kwenye nafasi hii Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba amenipa ushirikiano sana, tunashirikiana kwa karibu, ni mtu muungwana sana, Mungu ambariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha duniani kote anapimwa kwa *microeconomic fundamentals.* Tangu awe hapo uchumi wetu ni tulivu, na hizo ndizo sifa kubwa za kumpima Waziri wa Fedha popote duniani. Kwa hiyo, mnyonge mnyongeni, lakini haki yake lazima apewe. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba amefanya kazi nzuri katika kusimamia uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi Waheshimiwa Mawaziri walivyozijibu hoja hapa, walivyotoa maoni yao na walivyopokea michango ya Waheshimiwa Wabunge utakubali kwamba una Serikali imara sana. Yote haya ni kwa sababu tunaye kiongozi shupavu ambaye anatusimamia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaenda kisekta kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri wameshakueleza. Tumepokea michango na mapendekezo 96 kutoka kwenye Kamati yetu ya Bajeti, na yote ni ya maana. Tumepokea michango 84 kama nilivyosema ambapo maoni hayo yapo katika sekta mbalimbali. Kwenye maoni ya Waheshimiwa Wabunge unaona kabisa kwamba yanaakisi aina ya vipaumbele ambavyo Serikali inavitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea maoni mengi zaidi kuliko yote kwenye eneo la kilimo, mifugo na uvuvi. 15% ya michango yote imekwenda huko, inafuatiwa na barabara pamoja na miundombinu 13%, tunakwenda kwenye nishati, madini, uchumi, uwekezaji, viwanda na biashara pamoja na elimu, yote hiyo inaakisi aina ya vipaumbele ambavyo tunavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza wakati ninawasilisha mapendekezo haya na jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameeleza, Mpango huu ambao tunaupendekeza utakuwa ni wa mwisho katika kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano, lakini pia ni Mpango wa mwisho kwenye kutekeleza Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Hivyo ni muda mwafaka wa kufanya tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuja mwezi wa Nne wakati wa bajeti tutaeleza tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano. Kupitia kikao hiki, Waheshimiwa Mawaziri wameshaeleza mafanikio kwenye sekta mbalimbali. Niongeze matatu tu katika ya yale ambayo wameyasema. La kwanza, kwenye *aspect* ya maendeleo ya watu, ambao ni sehemu kubwa sana ya Mpango, ni muhimu kuzingatia tumetoka wapi na tupo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotoka. Ni kwamba, kati ya wanafunzi 100 waliokuwa wanamaliza darasa la saba ni wanafunzi 20 pekee ndio waliokuwa wanajiunga na shule ya sekondari. Tunapozungumza leo kati ya wanafunzi 100 wanaomaliza shule za msingi hapa Tanzania, wanafunzi 70 wanakwenda sekondari. Yote hii ni kwa sababu mbalimbali, lakini moja ya sababu kubwa ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliamua kufuta ada za sekondari, kwa hiyo, ikaondoa kikwazo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri kujitolea mfano, lakini naomba nijitolee mfano. Mwaka 1989 nikiwa *form two,* mimi nilifukuzwa shule kwa sababu ya kukosa ada, shilingi 2,000. Kwa hiyo, jambo hili ambalo Serikali ya CCM imelifanya limekuwa ni jambo kubwa, limeokoa watoto wengi wa Kitanzania walio maskini. Mimi isingekuwa wasamaria wema walionisaidia, pengine nisingekuwa Profesa leo. Kwa hiyo jambo hili ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili la haraka sana kwenye hilo ni kwamba, tumetoka kwenye 32% ya *coverage* ya maji vijijini, mpaka leo mdogo wangu Mheshimiwa Aweso, anatamba na 79%. Wakati tunaanza kutekeleza dira, pato la mtu mmoja Tanzania lilikuwa Dola za Kimarekani 384 ama shilingi 384,000. Leo tunazungumzia Dola za Kimarekani 1,200, zaidi ya shilingi milioni tatu. Wachumi wote ambao wamefanya tathmini ya uchumi wa Tanzania wanasema katika miaka 20 ukuaji wa uchumi wa Tanzania katika Bara la Afrika umekuwa siyo wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mwaka 2000 ilikuwa ukiitafuta Tanzania kwenye ligi za kiuchumi Afrika ilikuwa ni

lazima uanzie chini. Tanzania ilikuwa *ranked* miongoni mwa nchi za Kiafrika tatu za chini kiuchumi. Leo ukitafuta nchi 10 za kiuchumi lazima Tanzania uipate. Tunazungumzia kutoka Dola za Kimarekani bilioni 13.37 mwaka 2000 hadi leo ambapo pato la Taifa ni Dola za Kimarekani bilioni 80. Kwa hiyo, ni jambo kubwa, na wakati mwingine tunajifanyia tathmini ambayo siyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchakato huu wa dira tumefanya tathmini ya ndani na nje. Tulipomleta mtu wa nje kufanya tathmini ya dira yetu ya miaka 25, alisema mkibaki hivi bila ya kuongeza jitihada zozote, uchumi wenu unaweza kukua mara mbili na nusu katika miaka 20 ijayo. Mmekuwa katika kiwango ambacho ni kizuri. Mkiweka bidii kidogo ifikapo mwaka 2050 mtakuwa *upper middle-income country*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote haya yametoka wapi? Mambo haya yanatoka wapi? Mafanikio haya ni kielelezo cha usahihi wa sera za CCM. Mafanikio haya ni kielelezo cha ushupavu wa CCM katika kuisimamia Serikali. Mafanikio haya ni ushupavu wa kiongozi mkuu anayeiongoza nchi hii, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mafanikio haya ni kielelezo cha ushupavu wa Bunge lako katika kuisimamia Serikali hii ambayo tunaiongoza. Kwa hiyo, hili ni jambo la muhimu sana kuendelea kulizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee ufafanuzi mambo mawili tu kwa sababu hatua tuliyonayo sisi hapa ni kupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha mapendekezo ya Mpango tulionao ili tuwe na Mpango mzuri zaidi. Kwa hiyo, hapa hatuna sababu yoyote ya kueleza moja moja kwa kila Mheshimiwa Mbunge. Mapendekezo yao tumeyapokea na tunaamini Mpango utakaokuja mwezi wa Sita utakuwa bora zaidi kuliko ambao tumeuleta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kutolea ufafanuzi ni mawili. Kwanza ni miradi mikubwa ya kimkakati ambayo tunaitekeleza ambayo Waheshimiwa Wabunge wameizungumzia hapa; Liganga na Mchumchuma pamoja na *LNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye dira ijayo moja ya kibebeo cha kuchochea uchumi wetu ni hii miradi. Mradi wa *LNG* tunaoouzungumzia utaingiza Dola za Kimarekani katika uchumi wetu shilingi bilioni 40, nusu ya *GDP* ya leo. Hakuna Serikali yoyote duniani ambayo ingeweza kufanya mchezo na mradi kama huu. Ni mradi muhimu ambao ni lazima Serikali iukumbatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri pale kwamba mradi huu tunao na Mheshimiwa Rais anao, hatuwezi kuuachia, na bado tunazungumza na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mikubwa kama hii ambayo ikiingia katika uchumi itatikisa, inahitaji umakini, haihitaji ku-*rash,* lazima tupatie, kwa sababu tukikosea tunakuwa tumekosea kwa muda mrefu sana. Imechukua muda mrefu kwa sababu ni mradi mkubwa na hivyo ni lazima tuhakikishe kwamba utakapoanzwa kutekelezwa nchi yetu ni lazima ifaidike kwa sababu ni rasilimali za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kwa mradi wa Liganga na Mchuchuma, tayari tunaye mwekezaji, Maganga Matitu pale Liganga. Kwa hiyo, tumeshaanza wakati tukisubiri mradi mkubwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba miradi hii mikubwa yote ikiwepo hii miwili, Serikali inayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho la kulifafanua hapa ni suala la hali ya umaskini nchini. Waheshimiwa Wabunge wengi, na pia kwa umakini mkubwa Mheshimiwa Mulamula amehoji takwimu za hali ya umaskini nchini, akionesha kwamba ni za siku nyingi mno kwa sababu ni za mwaka 2017/2018; kwanza tunapopima takwimu za hali ya umaskini Tanzania tunaangalia mambo manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umaskini wa kipato, umasikini wa mahitaji muhimu, umasikini wa huduma duni za jamii pamoja na umaskini hata wa kukosa kauli. Ndiyo maana kuna *aspect* ya *governance,* na tunapima kila baada ya miaka mitano. Tangu tuanze, tumeshapima hali ya umaskini mara tano kuanzia mwaka

1991. Kwa hiyo takwimu za mwisho ambazo tunazo ni za mwaka 2017/2018, miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tupo kwenye mchakato wa kuzifanya nyingine, na tunatarajia tupate takwimu mpya ya mwaka 2025. Kwa hiyo, tutakapokuja Bunge lijalo, kwa maana ya Bunge la Bajeti, tutatoa taarifa ya hali ya umasikini iki-*reflect data* mpya ambazo *NBS* wanakwenda kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, takwimu hizo ndivyo zilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tunakwenda wapi kutoka hapa? Kama nilivyosema kwamba uchumi wetu umekua vizuri sana, wastani wa 6.7% katika kipindi cha miaka 20, ukiondoa miaka ya *COVID* kote huku nyuma ulikwenda vizuri sana. Lengo letu lilikuwa tufike asilimia nane katika kipindi hiki cha kuelekea mwaka 2025. Wote mnafahamu kuwa tuliyumba kutokana na hali ya *COVID* pamoja na ukweli kwamba nchi yetu haikuyumba sana ukilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tumekuwanayo ni ujumuishi, na ndiyo maana unaona Mpango uliopo tunazungumzia neno ujumuishi. Ni lazima uchumi wetu ukue katika hali jumuishi ili tuongeze kasi ya kupunguza umaskini. Kwa sasa ukiangalia takwimu za mwenendo wa ajira za *NBS* kwa Tanzania Bara za mwaka 2024, uanzie mwaka 2020 mpaka mwaka 2024 unaona kwamba 61% ya ajira zetu zipo kwenye kilimo, 11.4% hivi zipo kwenye biashara za jumla na biashara rejareja, 6.3% utazikuta kwenye huduma za malazi na chakula na huduma nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka Kwenda, moja, bado kilimo kitaendelea kuwa sehemu muhimu ya uchumi wetu. Kwa hiyo, ni lazima tuendelee kuwekeza katika suala la kilimo. Tunashukuru kwamba Mheshimiwa Rais katika kipindi chake hiki tumeongeza sana bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo hatulizungumzi, ambalo Mheshimiwa Rais na Waziri wa Kilimo wamelifanya, nalo ni kufanya kilimo kianze kupendeka kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mapinduzi mengi kwenye kilimo lakini kwangu mimi mapinduzi makubwa sana ni kukifanya kilimo kianze kupendwa. Sasa Mkulima wa Tanzania anaweza akajibainisha kwamba mimi ni mkulima bila wasiwasi. Lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwenye eneo hili. Kipekee lazima tumshukuru sana mdogo wangu Mheshimiwa Hussein Bashe, kwa jinsi ambavyo amekisimamia kilimo kwa *passion* ya hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *structure* yetu ni hiyo ya kwenda mbele, tunataka tutoke kwenye kilimo twende kwenye uchumi wa uzalishaji viwandani. Uchumi wowote ambao unakua unafika mahali watu wanapungua kutoka kwenye kilimo wanapungua kwenda wapi? Lazima wapungue siyo kwenda kwenye huduma tu, au kwenye biashara ndogo ndogo, tunataka wapungue watoke hapo kwenda kwenye uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona mikakati ambayo tunayo na dira inayokuja itatuelekeza kuwekeza nguvu nyingi sana kwenye *manufacturing* kwa kuanzia na *agro-processing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka kwenye *agro-processing* twende kwenye rasilimali zetu za asili. Tunataka kwa mfano, madini yetu yasitoke mashimoni moja kwa moja kwenda bandarini *(from the pit to the port), no*. Iwe *from the pit to industries then to the port*. Kutoka kwenye shimo kwenda viwandani kisha bandarini. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais, ameelekeza na ameshamwelekeza Waziri wa Madini na ndivyo mipango yetu inavyosomeka na ndivyo dira itakavyosomeka kwamba, tunataka tufike mahali madini yetu yasisafirishwe nje ya nchi bila ya kuongezewa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeendelea kwa kusafirisha malighafi nje ya nchi. Nchi zinaendelea kwa kusafirisha mali ambazo zimeongezwa thamani na huo ndiyo mwelekeo wa kisera wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *then,* ukitoka kwenye viwanda ndipo uende kwenye huduma, uende kwenye teknolojia na nyingine. *So,* huo ndiyo muundo wa uchumi wetu ambao tunakwenda nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe moja kwamba, mafanikio yote ya kisera na kiutendaji ni matunda ya Chama imara, Tunacho Chama imara, Chama Cha Mapinduzi na hili jambo Waheshimiwa Wabunge tuliseme waziwazi bila kificho. Utulivu mnaouona, amani mnayoiona, *governance* mnayoiona ni matunda ya uimara wa chama cha siasa kinaitwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mnayoyaona ni matunda ya ushupavu wa Kiongozi Mkuu wa Nchi. Kiongozi wetu wa nchi alipokea nchi siyo katika mazingira ya kawaida, unaweza ukamhukumu kwa yote, lakini jambo moja ambalo huwezi kumnyang'anya ni ukweli kwamba kiongozi huyu ameipokea nchi katika mapito magumu, lakini amehakikisha kwamba nchi yetu imebaki kuwa salama na imebaki kuwa tulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo nchi nyingi hizi changa kama ya kwetu ambazo zinaondokewa na Mkuu wa Nchi katikati ya safari bila kutarajia, zikabaki salama. Tunamshukuru Mungu kwa kutupa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amefanya nchi yetu imebaki kuwa tulivu. Hata ukayasahau yote, lakini kumbuka tuna Taifa ambalo bado ni salama lina umoja na amani kwa sababu tuna Kiongozi Mkuu aliye shupavu, hilo ni jambo la msingi. Mafanikio haya ni matunda ya Serikali imara. Wote mmeshuhudia kwa jinsi ambavyo Waheshimiwa Mawaziri wamejieleza hapa, utatilia shaka vipi uimara wa Serikali hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho muhimu sana, mafanikio haya ni matunda ya Bunge imara ambalo linaweza kutunga sheria sawa sawa; Bunge ambalo lina uwezo wa kuhoji Serikali mambo ya maana na Serikali ikayajibu. Kwa hiyo, kwa ujumla wake tuwahakikishie Watanzania kwamba nchi yetu ipo salama, ipo mikono salama, ipo vizuri kisera, ipo vizuri kiutekelezaji na tunajipanga vizuri zaidi kwenda mbele. Tuendelee kumuunga

mkono Mheshimiwa Rais, endeleeni kuiunga mkono Serikali ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia na kuhitimisha. Awali ya yote, kama ambavyo kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila alitangulia kusema, tumepokea hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia pamoja na hoja za Kamati, tumezipokea na tunakwenda kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia, tunashukuru Kamati ikiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Njeza, tunakushukuru wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuendesha mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wataalam wetu wa Wizara zote mbili kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Prof. Kitila, kaka yangu tunafanya kazi kwa pamoja vizuri sana, naye ni Mwalimu wangu, tunaendelea kushirikiana vizuri, ndiyo maana mnaona hata hoja tunazozileta zina ushirikishwaji mpana wa Wizara zetu ambazo zina mambo yanayofanana, lakini pia na Kamati ambazo zinatusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuja hoja nyingi na nyingi zilikuwa zinaboresha Mpango pamoja na Mwongozo na sisi tumepokea, tutaenda kuyafanyia kazi mambo hayo yote ya msingi ambayo yametolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo machache tu ambayo ningependa kuyasema, moja ikiwa ni Serikali, itenge bajeti kwa ajili ya kukamilisha majengo ikiwa inamaanishwa maboma ikiwemo majengo ya vituo vya afya pamoja na upande wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa sekta ameliongelea vizuri, ni kweli tumeongea vizuri na tunaendelea kujipanga ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaunga mkono jitihada za wananchi katika maeneo ambayo wananchi wamejenga maboma na tunaamini tutatoa utaratibu wa namna ya kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba katika maeneo mengi tuna maboma ya vituo vya afya, maboma ya zahanati na madarasa, tumelijua hili, tunalijua hili tumelipokea na hata sasa tunaendelea kulifanyia kazi. Tunakamilisha taratibu za kifedha na punde taratibu za kifedha zitakapokamilika tutazipeleka TAMISEMI kama Waziri alivyosema ili ziweze kuwafikia Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alishaelekeza Wilaya zote zitakapopokea fedha hizi Wabunge wajulishwe ili muweze kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wake, kwa sababu ni mambo ambayo mmeyasemea sana na mmeyafuatilia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mmesema Serikali ilipe fidia kwa ajili ya wananchi wanapopisha miradi. Ni dhahiri kwamba katika Serikali ya Awamu ya Sita tumejitahidi sana kulipa fidia, kuna maeneo ambayo tayari tumeshalipa fidia yakiwemo yale ambayo yalishakaa siku nyingi sana bila fidia hizo kulipwa. Fidia hizo zimeshalipwa, pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye alisema tulipe fidia hizi katika maeneo ambayo yanaenda kutumika kwa maslahi mapana ya Serikali na tunaendelea kulipa katika maeneo mengine yaliyosalia. Kwa hiyo, Wabunge wote ambako wana masuala yanayohusu fidia wajue kwamba Serikali tunaenda hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusingeweza kulipa siku moja kwa sababu maeneo mengine ni ya siku nyingi na yanahusisha fedha nyingi na ni lazima maeneo mengine pia yanayohitaji fedha yaendelee kutekelezwa. Ishara kwamba Serikali ipo *committed* kwenye masuala haya ni kwamba kuna maeneo mengi na yanahusisha mabilioni ya fedha tayari tumeshaanza kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tumelipa kwa Mkoa wa Njombe, tumelipa kwa Mkoa wa Mara tumelipa na maeneo mengine mengi. Hata sasa nakumbuka jambo ambalo limekuwa likifuatiliwa sana la Dar es Salaam, Kipunguni tunakumbuka na fedha, *exchequer* tulishatoa na maeneo mengine mengi Waheshimiwa Wabunge ambayo wamekuwa wakifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufanyi makusudi wala hatuwadharau wananchi lakini ni kwamba taratibu za kuweza kutekeleza mambo yote ambayo ni ya muhimu kwa wananchi wa Tanzania ndiyo yanayotufanya tumegemege maeneo tofauti tofauti na tutangulize maeneo tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliwahi kusema Mwanafalsafa mmoja kwamba, kwenye nchi zetu hizi maskini zinazoendelea, lugha aliyotumia wakati ule, kila kitu ni kipaumbele. Hata sisi hapa leo hii tukisema tuchukue tu maeneo matano ndiyo tuseme kipaumbele, mtaona jinsi ambavyo shughuli itakavyokuwa ngumu, kwa sababu kila kitu kinatakiwa kuendelezwa kwa maana hiyo ndiyo inayoleta changamoto kwenye kugawa fedha iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pongezi ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ameongeza bajeti kwenye kila sekta, na siyo kuongeza bajeti tu na fedha kwenye maeneo hayo zimeongezeka. Ninyi ni mashahidi sasa hivi siyo jambo la ajabu kusikia kwenye kijiji zimekwenda shilingi bilioni saba, kwenye kijiji zimekwenda shilingi bilioni 15, kijiji zimekwenda shilingi bilioni 30. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuhamisha kutoka kwenye kasungura na ametupeleka kwenye tembo. Ni vile tupo wengi ndicho ambacho kinafanya bado tuendelee kuwa na uhitaji mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipunguze matumizi ya kawaida, hiki ni kipaumbele na Mheshimiwa Rais kila wakati anatuelekeza kwamba kipaumbele cha kwanza ni miradi ya maendeleo. Ukiona kuna sehemu matumizi ya fedha zimekwenda kwenye matumizi ya kawaida zimekwenda kwenye utekelezaji wa miradi, ni kwa sababu miradi pia haiwezi kujiendesha yenyewe

lazima miradi itekelezwe na inatekelezwa na wanadamu. Kwa hiyo, kunakuwepo na sehemu ya uendeshaji na sehemu hiyo inakwenda kwenye matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vingi ambavyo vinahusika na utekelezaji wa miradi, lakini katika dirisha la masuala ya uhasibu yanaingilia kwenye fedha za matumnzi ya kawaida. Kipaumbele kikubwa ambacho tunakizingatia ni miradi ya maendeleo na ishara kubwa ambayo inakwambia kwamba tupo makini kwenye masuala ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na fedha za miradi ya maendeleo ni hii miradi ya kimkakati ambayo imeweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote ambayo haipo makini, haiweki *focus* kwenye fedha kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo. Nawahakikishia, haiwezi ikatekeleza miradi mikubwa kama hii ambayo Tanzania imetekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ambayo inatekelezwa Tanzania hakuna nchi za *SADC* wala *EAC* wala hapa Afrika inatekeleza miradi mingi kwa mara moja kama inayotekelezwa hapa Tanzania, hakuna. Ninyi nendeni mkafuatilie na hata wenzetu wanaotufuatilia wanashanga kwamba tumewezaje kutekeleza miradi mikubwa ya aina hiyo katika nchi ya Tanzania na katika kipindi ambacho dunia nzima inapita kwenye msukosuko wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea, reli ni moja ya mradi wa kielelezo ambao umetekelezwa Tanzania na itakapokamilika itakuwa miongoni mwa reli tano ndefu zaidi duniani. Nchi tano zenye reli ndefu na Tanzania itaingia; kwa Afrika itakuwa ya kwanza. Hili siyo jambo dogo, Watanzania wanatakiwa watembee kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tunalo Daraja la Kigongo - Busisi ni moja ya mradi wa kielelezo na wenyewe upo hatua za mwisho. Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mradi mwingine wa kielelezo ambao bajeti yake ya mara moja wakati upo kwenye *peak* ya utekelezaji ni fedha nyingi. Hiyo inaonesha ni nchi ambayo ina kiongozi ambaye yupo *committed* kwenye

kupeleka fedha kwenye masuala yanayowahusu wananchi wake kama ambavyo amefanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *certificate* moja ilikuwa inatokea tunalipa takribani shilingi bilioni 400, shilingi bilioni 300, shilingi bilioni 400 mpaka shilingi bilioni 450, dola milioni 130, dola milioni 140 kwa *certificate* moja ya mwezi mmoja. Hii inawezekana tu kwenye nchi ambayo kiongozi wake kipaumbele chake kikubwa ni maisha ya wananchi anaowaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imetoa mfano na maeneo tunakozunguka kule wanaitolea mfano, viongozi wa sekta wamesema lakini kila tunapokaa Mawaziri wa Fedha, Tanzania inajitokeza ya mfano kwenye miradi ya maji. Hivyo vinakuwa vinahusisha Mawaziri wote wa Afrika, inajitokeza nchi ya mfano kwenye mageuzi ya elimu na hii inajitokeza kwenye nchi zote za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia inajitokeza nchi ya mfano kwenye masuala ya umeme, zinakuwepo nchi zote za Afrika; inajitokeza nchi ya mfano kwenye afya, kwenye mageuzi ya kilimo, kwenye mageuzi ya mifugo na uvuvi na sekta nyingine. Hapa tumetaja chache kwa sababu ya maslahi ya muda, lakini tuna sekta nyingine nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni mambo yanayohusisha fedha na hiki ndicho ambacho kimekuwa kikimfanya Mheshimiwa Rais mara zote akose usingizi, azunguke huku na kule mara zote awe macho kuhakikisha kwamba miradi hii yote inasonga mbele kama alivyosema wakati anaapishwa na alichokisema sasa hivi Watanzania wanakiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia siku moja nilipata bahati ya kuongozana na Mheshimiwa Rais kwenye moja ya ziara katika kipindi ambacho kilikuwa na ibada, yupo kwenye mfungo ikatokea tunatakiwa tuwe na kikao wakati wa kufuturu, alikwenda kufuturu kwa maji ili tu Watanzania wapate maji, wapate Barabara na vituo vya afya. Huko ni kujitolea kwa kiwango cha juu ambacho Tanzania inaonesha kupitia kiongozi wake Mkuu na

Serikali yake anayoongoza na uimara wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liliongelewa jambo lingine linahusisha Lugha ya Kiswahili. Kwa kumalizia, upande wa taasisi za kifedha tayari tumeshapata ruhusa ya Kiswahili kuanza kutumika kwenye vikao vya Benki ya Dunia. Sasa hivi tunakamilisha kuhusu utaratibu ufanyike, kuhusu kupata wakalimani watakaokuwa wanafanya kazi ya ukalimani kutoka Kiswahili kwenda kwenye lugha nyingine ambazo zinatakiwa zitumike katika mikutano hiyo. Hii ni moja ya jambo lingine kubwa kwenye diplomasia ambayo imetokana na umahiri wa Mheshimiwa Rais wetu ambao ameufanya katika kuifungua nchi yetu kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liliongelewa jambo la mifumo, tumelipokea na kama nilivyosema, kazi inaendelea kufanyika, tunaendelea kukamilisha mifumo yote ya upande *customs* pamoja na mifumo ya kodi za ndani. Yote hii itatuhakikishia kuongezeka kwa mapato ya Serikali na itatuongezea utaratibu mzuri wa masuala ya makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mengine yaliyoongelewa kuhusu masuala ya utawala wa kodi pamoja na mifumo ya kikodi Mheshimiwa Rais, alishaunda Tume ambayo inaendelea kufanya kazi kama nilivyosema wakati natoa hoja. Tume hiyo itakapomaliza kazi, itakuwa imetusaidia kuhusu utaratibu wa masuala mazima ya kiutawala ya kodi, viwango vya kodi na namna ya kuongeza wigo wa kodi ili kodi iweze kulipwa na watu walio wengi na hivyo kupunguza mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo ni ya kiutawala tumeshapata mwongozo ambao tunaendelea kufuatilia kuhusu matumizi ya risiti za kielektroniki. Kwenye jambo hili tunaendelea kutengeneza na utaratibu wa kuongeza hamasa pamoja na elimu. Siku siyo nyingi tutakuja na utaratibu ambao utaongeza hamasa kwa Watanzania wao wenyewe kudai risiti wanapofanya manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja na utaratibu tutautangaza utakapokuwa umekamilika, lakini upo hatua za manunuzi ambao utaleta bahati nasibu za kuweza kuongeza kasi ya Watanzania wao kwa wao kudai risiti wanapokuwa wamefanya manunuzi na kila wanapouza waweze kutoa risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilikuwa limeongelewa lilihusisha masuala ya TEHAMA. Mheshimiwa Rais alishatoa siku ya mwisho kwa ajili ya mifumo kusomana. Jambo hili linahusisha na Wizara nyingine, kazi inaendelea, kazi inaendelea ngazi ya wataalamu na ni jambo la muhimu ambalo tumelipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine waliongelea kuhusu kushusha *VAT,* ni moja ya mambo ambayo yataongelewa punde tutakapokwenda kupokea taarifa ya Timu yetu ya Wataalam. Itahusisha watu wengi, naamini hata upande wa Bunge, kama siyo Bunge lote kwa uwakilishi wa Kamati, naamini maoni yenu nanyi yatakwenda kwenye Kamati ili mweze kutoa maoni hayo na kuweza kuboresha utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liliongolewa lingine kuhusu bajeti ya mafungu iende sambamba na uidhinishwaji wa miongozo ya bajeti. Tumeyapokea sambamba na maoni mengine kama ambavyo yalitolewa, tumeyapokea na sisi tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimia Mwenyekiti, mambo mengine yaliyokuwa yametolewa yalihusiana na kutenga fedha kupitia ruzuku ya maendeleo kwa ajili urejeshwaji wa mwaka wa fedha, tumelipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yalihusisha utaratibu wa matumizi ya nishati safi na *incentives* ambazo zinahusisha matumizi ya gesi, tumeyapokea na tumeshaanza tangu mwaka wa fedha huu wakati tunapitisha Sheria ya Fedha ya mwaka huu. Hiyo na yenyewe tumeipokea na tutaendelea kuiboresha ili kuweza kuvutia zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo liliongelewa ilikuwa kuhusu madeni ya wazabuni. Hili ni eneo la muhimu sana na Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mkazo sana. Kinachotokea siyo kwamba Serikali hailipi wazabuni, kinachotokea, tunapata kazi ya kugawanya kuhusu kulipa madeni ambayo yalishalimbikizwa muda mrefu na haya mapya. Kwa hiyo, tunaendelea kulipa ambayo yalishalimbikizwa na tunalipa ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao mna wazabuni marafiki, waulizeni watawaambia. Kuna wengine walikuwa na madeni ya mwaka 2014, mwaka 2015 na mwaka 2016 sasa hivi wamepokea fedha zao. Kuna wengine ambao wanaendelea na kazi, wanaendelea kupokea fedha zao, kwa sababu katika nchi pia hatuwezi tukakaa mwezi mmoja, wa pili na wa tatu tunalipa madeni tu, nchi lazima iendelee na kazi za uzalishaji za sasa lazima ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayohusiana na kulipa madeni imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, bajeti iliyopo kwenye mafungu ya kisekta na bajeti ambayo ipo kwenye Wizara ya Fedha, bajeti ya kulipa wakandarasi imeongezeka. Tulianza na shilingi bilioni 200, mwaka uliofuata tukaenda shilingi bilioni 400, mwaka uliofuta tukaenda shilingi bilioni 600 na mwaka huu uliopita bajeti yake iliongezeka kwa zaidi ya 100%. Hii yote ni kwa sababu tu wigo ulikuwa mpana sana, tunaendelea kuhakiki na tunaendelea kuyalipa madeni ya wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais mara zote ameelekeza kwamba tuelekeze fedha kulipa wazabuni, watoa huduma na wakandarasi ili kuweza kuongeza fedha kwenye mzunguko wa fedha hapa ndani ya nchi. Hili linafanyika ndiyo maana katika maeneo mengi mnaweza kuona jinsi ambavyo viashiria vingine vimepokea kama kupungua kwa mikopo chechefu ni ishara kwamba wale wanaofanya kazi ndani ya nchi wanapata malipo, nao wanaweza kurejesha mikopo kwa wale ambao walikuwa wamepata mitaji kwa kupitia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya uhimilivu wa kiuchumi, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila, ameshasema, tutaendelea

kuyafanyia kazi kama tulivyokuwa tumeahidi wakati tunasoma Bajeti ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *windup*.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi, nawashukuru sana Wabunge, niwahakikishie kwamba tumepokea hoja zote na tukitoka hapa tutazifanyia kazi hoja hizi na Wizara ya Fedha tufanyia kazi pia utoaji wa fedha kwenye maeneo ambayo mmeyaongelea ambayo mmesema yapate fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, wakati natoa hoja niliomba tuiombee Simba, nikasahau Yanga. Naona huko nako hali inakuwa mbaya, naomba tuiombee Yanga na yenyewe maana hali imekuwa siyo hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, Mpango na maoni yenu yameshapokelewa na Serikali. Serikali nendeni mkayafanyie kazi na kwa kifupi *go and work the talk. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana, kwa kipindi cha siku tano mmeonesha ukomavu mkubwa sana, mmechangia mambo muhimu kwa Taifa letu na ushauri wenu Serikali imeahidi itaufanyia kazi. *(Makofi)*

Ninawashukuru upande wa Serikali, nikushukuru Mheshimiwa Waziri Lukuvi kwa kuomba hili tulilolifanya leo hapa halijawahi kutokea Tanzania. Bunge limewapa takribani masaa matatu na nusu Serikali peke yenu kusimama kueleza tulipotoka, tulipo na tunakokwenda chini ya miongozo ya Mheshimiwa Rais,

Mheshimiwa Dkt. Samia na *4R* ambayo ametupa ndiyo dira na *roadmap* ya Taifa letu sasa hivi. Hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kushinda chaguzi ni ajenda. Mmeona kuna chaguzi hivi karibuni, mmoja alikuwa na ajenda mwingine hakuwa na ajenda. Mama Mheshimiwa Dkt. Samia ana ajenda ya Taifa hili, ana dhamira za dhati kuhakikisha kuwa Taifa hili linakwenda mbele. Mungu ampe uzima na afya nasi tukirudi Majimboni kuanzia kesho haya ndiyo ya kwenda kusema. Ukikosa maji umepata umeme, ukikosa umeme umepata darasa, ukikosa darasa umepata mbegu, umepata na mbolea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haijawahi kutokea Tanzania mambo kama haya, tumshukuru na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais peke yake hawezi kufanya, tusimsifie mwenye mbio, tumsifie na yule anayemfukuza ambaye ni Serikali, Wabunge, Chama cha Mapinduzi na wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.46 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 8 Novemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*